

Toleo la
2024

Umilisi wa FASIHI SIMULIZI



Bin Gitonga (Malenga)

Msanifu wa mradi: *Kingsford Munene (Shule ya Wasichana ya Kyeni, Embu)*

Kimechapishwa na:

Williams Publishers Limited

Barua Pepe: williamspublishersltd@gmail.com



© Bin Gitonga (Malenga)

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa, ni hatia kuiga, kunakiri, kupiga chapa au kukiiga kitabu hiki kwa njia zozote bila idhini ya Bin. Gitonga.

Kimechapishwa mara ya kwanza: 2024

ISBN: 978-9914-50-371-5



0710 369 970



Umilisi wa Kiswahili / Mwalimu Bin Gitonga



Umilisi wa Kiswahili / Mwalimu Bin Gitonga

YALIYOMO

Kutabaruku-----	iv
Shukrani-----	iv
Dibaji-----	v
Utangulizi-----	vi
Mwongozo kwa msomaji-----	vi
1. KAZI YA KITADO CHA 1 -----	7
• <i>Maana Ya Fasihi</i> -----	8
<i>Makundi ya Fasihi</i> -----	10
2. FASIHI SIMULIZI -----	15
<i>Istilahi Katika Fasihi Simulizi</i> -----	18
3. TANZU ZA FASIHI SIMULIZI-----	22
Utanzi wa Hadithi -----	24
→ <i>Maswali - Jitathmini 2</i> -----	37
Utanzi wa Semi -----	38
→ <i>Maswali - Jitathmini 3</i> -----	61
Utanzi wa Ushairi Simulizi-----	62
→ <i>Maswali - Jitathmini 4</i> -----	82
4. KAZI YA KIDATO CHA PILI-----	82
Utafiti wa Fasihi Nyanzani-----	82
Hatua za kukusanya data-----	82
Mbinu za kukusanya na kuhifadhi data-----	87
→ <i>Maswali - Jitathmini 5</i> -----	91
5. KAZI YA KITADO CHA 3-----	92
Utanzi wa Mazungumzo -----	93
Vipera vya mazungumzo -----	93
→ <i>Maswali - Jitathmini 6</i> -----	101
<i>Utanzi wa Maigizo</i> -----	102
Vipera vya maigizo-----	103
→ <i>Maswali - Jitathmini 7</i> -----	114
6. KAZI YA KIDATO CHA 4-----	115
Mchango wa Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi-----	115
Usasa katika Fasihi Simulizi-----	120
Mwingiliano wa vipera vya fasihi simulizi -----	121
→ <i>Kichocheo- vipera tatanishi</i> -----	122
<i>Marejeleo</i> -----	123

KUTABARUKU

Kitabu hiki ni zawadi adimu na hidaya tunu kwa wanafunzi wangu wapenzi wa Shule ya Upili ya Mabinti ya Materi – Meru.

SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuyaandika matini haya. Pili, nawashukuru wahadhiri wangu walezi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta. Aidha, nitakuwa mchache wa fadhila iwapo sitawashukuru walimu wenzangu kwa jumla katika Idara ya Kiswahili, Shule ya Upili ya Wasichana ya Materi.

Hali kadhalika, hisani ya Gitonga Bongo, Bishop Karau, Eng.Mwandiki, Prof.Kirimi, Eng. Frank na Gitonga Festus katika kuchapisha kazi hii sio lelemama ni babukubwa.

WALIOCHANGIA:

Msanifu wa mradi huu wa Fasihi Simulizi

- Kingsford Munene (Shule ya Kitaifa ya Wasichana Kyeni, Embu)
(Alihakiki vitahiniwa vya Fasihi Simulizi kwa mujibu wa silabasi)

Wahariri wa muswada

- Geoffrey Gitonga (Shule ya Wasichana ya Materi)
- George Rucha (Shule ya Mabinti ya Materi)
(Walifanya uhariri wa Isimu na Sarufi)

Watathmini wa muswada huu

- Bi. Karani *(Shule ya Kitaifa ya Wasichana ya Chogoria)*
- Francis Wanjohi *(Shule ya Upili ya Mubao)*
- Amstrong Mutura *(Shule ya Wavulana ya Chogoria)*
- Nashebanda Jean Viva *(Shule ya Wavulana ya Nyangwa)*

Wakusanyaji wa data ya Toleo la pili 2024

- Lawson Muchiri - *Naibu wa Mwalimu Mkuu, Shule ya Upili ya Mutiiguru*
- Kimson Mukumu – *Shule ya Wasichana ya Kanjalu, Tigani West*

Mjunbe wa Shule za Sekondari ya Awali

- Bw Kimathi Mpuko - *Mwalimu Mkuu, Shule ya Msingi ya Bweni Muraga*

DIBAJI

Fasihi Simulizi imefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa waalamu hao ni M.M. Mulokozi (1996) anasema Fasihi Simulizi ni fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi.

Kamusi ya TUKI (2004) Fasihi Simulizi ni kazi ya fasihi inayohifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo kama vile: hadithi, ngoma na vitendawili.

Balisidya (1983) anasema Fasihi Simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo katika kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwa wasikilizaji na watumiaji wake.

Wanjara (2011) anasema Fasihi Simulizi ni sanaa ambayo vyenzo kuu ya utunzi, uwasilishaji na usambazaji wake ni sauti pamoja na vitendo. Fasihi Simulizi ni sanaa inayotumia mazungumzo na vitendo kisanii ili kuwasilisha maarifa au ujumbe fulani kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa ujumla, Fasihi Simulizi ni sanaa inayobuniwa kuwasilishwa na kusambazwa kwa (lugha ya) mdomo, na vyombo vyake vikubwa ni mdomo na sauti ya binadamu katika hali ya kuimba, kusimulia, kuiga, kughani, kutamba na kutega kama vile vitendawili vinavyotegwa kwa hadhira.

Kuzuka na kukua kwa sayansi na teknolojia kumeathiri pakubwa maana ya Fasihi hii, Fasihi Simulizi ya jamii ijuayo kusoma na kuandika ni tofauti sana na fasihi simulizi ya jamii isiyo na uandishi, kwa vile imeathiriwa na ujuzi wa kusoma na kuandika na mitindo ya masimulizi yake hayaendi sambamba na mitindo ya masimulizi yasiyoathiriwa na uandishi. Hata hivyo, utamu wa Fasihi Simulizi ungali upo.



Prof. Wendo Nabea

(Profesa wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Laikipia)
Mei, 13th, 2024

UTANGULIZI

Katika kazi yoyote ya fasihi ni lazima pawepo na ustadi wenye kuleta mvuto fulani kwa hadhira (wasikilizaji au wasomaji) husika. Ustadi (ufundi) huo unaovutia hadhira huitwa fani, ambayo hujumuisha mambo mengine vile:

Muundo - ni mtiririko/msuko/mpangilio wa matukio /visa.

Mtindo - ni mbinu inayotumiwa na fanani ili atofautiane na fanani mwingine.

Wahusika - ni watu au vitu vyenye uhai au visivyo na uhai ambavyo hutumiwa na fanani katika kazi yake.

Mandhari - ni eneo ambalo fanani hulitumia kujenga matukio na mtiririko katika kuumba kazi yake au maeneo anayoyatumia fanani kuakisi jamii anayoilenga.

Matumizi ya lugha - ni lugha anayotumia fanani katika kujenga wasifu wa wahusika kishaiba katika kazi yake.

MWONGOZO KWA MWANAFUNZI WA GREDI YA 7, 8, 9

MTAALA WA UMILISI - CBC

Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa kwa mwanafunzi wa Sekondari ya Awali.

Mwanafunzi aelekezwe:

- Kushiriki na wenzake kueleza kikamilifu maana ya fasihi katika jamii.
- Kutambua tungo za fasihi simulizi (k.v. **hadithi, semi, mazungumzo, ushairi simulizi na maigizo**) na fasihi andishi (k.v. novela, riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi) kutoka simulizi za moja kwa moja au kwenye matini za kidijitali.
- Kuwawasilishia wenzake utungo wa fasihi (k.v. hadithi za wanyama) ili waitolee maoni.
- Kushiriki na kutafiti kuhusu tanzu za fasihi simulizi na andishi katika jamii yake.

GREDI YA 7

1. Maana ya Fasihi - Tanzu za fasihi
2. Nyimbo - Nyimbo za Watoto, Bembelezi, za Kazi, za Dini.

GREDI YA 8

1. Hadithi - Mighani, Visasili, hurafa na hekaya

GREDI YA 9

1. Semi - Tashbihi, sitiari, methali, vitendawili na nahau
2. Mazungumzo - Malumbano ya Utani, Uzungumzaji katika Sherehe, Mawaidha.

Kidato Cha

1

Na

1

MTAALA WA KICD

SHABAHA:

1. Kufikia mwisho wa kidato cha 1, mwanafunzi awe na umilisi wa:

- ✓ *Maana ya Fasihi*
- ✓ *Aina za Fasihi*
- ✓ *Dhima ya Fasihi*
- ✓ *Tofauti za fasihi simulizi na Fasihi Andishi*
- ✓ *Umuhimu wa Fasihi Simulizi*
- ✓ *Tanzu za Fasihi Simulizi*
 - *Hadithi*
 - *Semi*
 - *Ushairi Simulizi*

2. Kufikia mwisho wa kidato cha 2, mwanafunzi awe na umilisi wa:

- *Mbinu za kuainisha tanzu za Fasihi Simulizi*
- *Umilisi wa:*
 - *Vipera vya Hadithi*
 - *Vipera vya Semi*
 - *Vipera vya Ushairi Simulizi.*
- *Utafiti wa Fasihi Simulizi nyanjani*
- *Njia mbalimbali za kukusanya data*
- *Vifaa vya kukusanya na kuhifadhi data*
- *Mbinu za kuhifadhi Fasihi Simulizi*

MAANA YA FASIHI

MAANA YA FASIHI

Ni sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaomhusu binadamu.

SANAA

Ni ufundi wa kuwasilisha fikra na hisia za binadamu kama vile Lugha, maandishi, uchoraji, uchongaji, ufinyanzi n.k.

VIPENGELE VYA SANAA	Uchoraji	Uchongaji	Fasihi	Ufinyanzi	Ufumaji	Utarizi	Ususi
Nyenzo ya kuwasilisha	Rangi/ kalamu	Mawe / gogo la mti	Lugha	udongo	Nyuzi	Uzi	

***Tanbihi:** Katika silabasi ya shule za sekondari tutajikita katika kipengele cha Fasihi pekee yake.

Uchongaji



FASIHI NI SANAA KWA VILE:

Usanaa wa fasihi, unajidhihirika katika mambo yafuatayo;

a) Uteuzi mzuri wa lugha;

Kwa kawaida kazi za fasihi, iwe fasihi simulizi au fasihi andishi huwa na lugha yenye ufundi, lugha hii huwavutia hadhira katika kuisikiliza au kuisoma kwake. Lugha ya kifasihi ni lugha iliyojaa matumizi ya methali, misemo, nahau na tamathali mbalimbali za semi na kadhalika.

b) Mpangilio wa wahusika;

Wasanii wa kazi za kisanaa hutumia ufundi wa kuwapanga wahusika ili wasaidie kufikisha ujumbe kwa hadhira zao. Wasanii huweza kuwachora wahusika halisi au wahusika wa kubuni na kuwapa majukumu yenye ufundi mkubwa kwa hadhira.

c) Msuko wa visa na matukio;

Mara nyingi wasanii wa kazi za kifasihi hupanga matukio yao katika kazi zao Kwa kutumia ufundi mkubwa. Wasanii wanaweza kupanga kazi zao moja kwa moja au kwa mtindo changamano. Kitendo hiki hufanya baadhi ya wasomaji kuweza kuburudika zaidi pindi wanaposoma kazi hizo.

d) Ubunifu;

Mawazo aliyonayo msanii wa kazi za kifasihi yanatumia ubunifu mkubwa katika kuyawasilisha kwa hadhira. Mawazo hayo yanaweza kuibua furaha au huzuni kwa msomaji au msikilizaji.

e) Uteuzi mzuri wa mandhari;

Hata katika kuiteua mandhari katika kazi ya fasihi huhitaji ufundi. Wasanii huweza kutumia mandhari halisi au ya kubuni. Maranyingi, wasanii huchora

mandhari, hata yakiwa ya kubuni lakini husadifu mandhari ya kawaida. Kitendo hicho hudhihirisha usanaa wa fasihi.

f) Huwasilisha ujumbe kuhusu binadamu mfano: utamaduni na uchumi.

g) Huwa na umbo mahususi. Mfano:

- Hadithi huwa na mwanzo, kati na mwisho
- Mashairi huwa na beti, mishororo, n.k.

TOFAUTI KATI YA FASIHI NA SANAA NYINGINE

Fasihi ni kipengele mojawapo wa vipengele vya Sanaa. Je, Sanaa ya fasihi inawezaje kutofautiana na sanaa nyingine?

a) Lugha: Ni kitu pekee kinachoweza kutofautisha kati ya fasihi na sanaa kama vile, uchongaji, ususi, ufinyazi na kadhalika. Ili iwe kazi ya fasihi ni lazima itumie lugha, iwe lugha ya mazungumzo au maandishi. Lakini sanaa kama uchongaji haitumii lugha katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira husika.

b) Utendaji: Kazi ya fasihi, huwa na utendaji yaani vitendo halisi hupatikana. Mfano, maigizo, miviga na kadhalika. Utendaji huu wa kazi za fasihi hushirikisha fanani na hadhira kwa wakati mmoja hasa katika fasihi simulizi. Tofauti na sanaa nyingine ambazo huwezi kuupata utendaji na ushirikishwaji wa fanani na hadhira kwa wakati mmoja.

c) Fani na maudhui: Kazi yoyote ya fasihi ni lazima iwe na maumbo mawili ambayo ni fani na maudhui. Hakuna kazi ya fasihi ambayo haina fani na maudhui. Tofauti na sanaa nyingine ambazo si lazima kuwa na vipengele hivyo vya fani na maudhui.

d) Wahusika: Katika kazi ya fasihi wahusika wanaweza kuwa ni viumbe hai au visivyokuwa na uhai hasa katika fasihi simulizi. Sanaa nyingine haina uwezo wa kutumia viumbe hai na wasiokuwa na uhai.

e) Mandhari: Katika fasihi mandhari yanaweza kuwa halisi au ya kubuni. Katika sanaa nyingine inaweza kuwa na mandhari ya aina moja tu au kukosa kabisa mandhari.

***Tanbihi:** Fasihi ni tawi la Sanaa linalotumia nyenzo ya lugha katika kufikisha ujumbe wa msanii kwa hadhira husika.

AINA/MAKUNDI YA FASIHI

Fasihi ndiyo aina pekee ya sanaa inayotumia lugha kujitambulisha au kujitofautisha na aina nyingine za sanaa.

Kuna Aina Mbili Kuu Za Fasihi. Nazo Ni:

- 2) **Fasihi Simulizi** – Ni fasihi ambayo ubuniwa na huhifadhiwa akilini kisha kuwasilishwa na kusambazwa kwa lugha ya mazungumzo/masumilizi kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine.
- 3) **Fasihi Andishi** – Ni fasihi ambayo huhifadhiwa kwa maandishi vitabuni na kuwasilishwa kwa lugha ya maandishi (kwa njia ya kusoma)

KUNA TANZU NNE KUU ZA FASIHI ANDISHI, NAZO NI:

1. **Novela** - Ni utanzu wa fasihi bunilizi ambao si mrefu kama ilivyo riwaya na wala si mfupi kama hadithi fupi.
2. **Riwaya** – utanzu wa fasihi andishi, ambayo huwa ndefu kuliko hadithi fupi.
3. **Tamthilia** - kazi ya fasihi andishi inayowasilisha mchezo wa kuigiza kitabuni.
4. **Hadithi Fupi** – kazi ya fasihi andishi isiyokuwa ndefu sana kama riwaya.
5. **Ushairi Andishi** - mashairi yaliyochapishwa vitabuni utanzu wa Fasihi Andishi.

Fasihi hizi zina dhima sawa katika jamii ingawa ni tofauti. Tofauti kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi hujitokeza katika uwasilishwaji wake katika jamii husika. Fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia yam domo nayo fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.

KUFANANA KWA FASIHI SIMULIZI NA FASIHI ANDISHI

Kimsingi, Fasihi ni moja ingawa imegawanyika katika sehemu kuu mbili, yaani, **Fasihi Simulizi** na **Fasihi Andishi**. Mbali na mgawanyiko huo, kuna mambo ambayo yanafanana katika Fasihi zote mbili. Mambo hayo ni pamoja na:

- 1) Zote hutumia ufundi wa **lugha** ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira husika
- 2) Zote zina **wahusika** ambao ni fanani na hadhira
- 3) Zote mbili hushughulikia masuala yanayohusu **maisha ya binadamu**.
- 4) Zote mbili huwa na vipengele viwili vikuu, **maudhui** na **fani** (jumla ya mbinu msanii alizotumia kuwasilisha maudhui).

- 5) Zote mbili huwa na **majukumu/umuhimu** sawa k.v. kuburudisha, kuadilisha, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, n.k.
- 6) Zote mbili zina **utendaji**- Andishi ina utendaji pale tamthilia na riwaya zinapoigizwa jukwaani.
- 7) Zote mbili **huzaliwa**, hukua na hufa kutegemea **mabadiliko** ya wakati.
- 8) Zote mbili huwa na wawasilishaji/**fanani** k.m. mtambaji/mganaji au manju/yeli kakati Fasihi Simulizi na mwandishi upande wa Fasihi Andishi.
- 9) Fasihi Andishi **imekopa** tanzu za fasihi simulizi k.v. methali, mashairi, n.k.

• **TOFAUTI KATI YA FASIHI SIMULIZI NA FASIHI ANDISHI**

	KIPENGELE	FASIHI SIMULIZI	FASIHI ANDISHI
1	Uwasilishaji	Fasihi Simulizi huwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo. Huandamana na utendaji k.v matumizi ya ishara, nyimbo, makofi, kuimba, kubeba zana katika majigambo	Fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi bila vitendo
2	Umri	Fasihi Simulizi ni kongwe kuliko Fasihi Andishi, ilianza enzi za mababu zetu	Fasihi Andishi ni changa kuliko Fasihi Simulizi, ilianza baada ya binadamu kujua kuandika.
3	Umilikaji	Fasihi Simulizi humilikiwa na jamii nzima, ni mali ya jamii	Fasihi Andishi humilikiwa na mwandishi, ni mali ya mwandishi
4	Tanzu	Fasihi Simulizi ina tanzu na vipera vingi kuliko Fasihi Andishi	Fasihi Andishi ina tanzu tatu pekee; Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi
5	Hadhira	Hadhira yake ni hai, yaani uwasilishwa mbele ya hadhira,	Hadhira inayosoma vitabu haina uhusiano wa moja

		hadhira ina uhusiano wa moja kwa moja na fanani.	kwa moja na fanani
6	Mabadiliko	Fasihi Simulizi hubadilika haraka kutegemeana na mahitaji ya hadhira na wakati. fanani anapowasilisha (ufaraguzi)	Fasihi Andishi haibadiliki haraka kutegemeana na mahitaji ya hadhira na wakati
7	Utunzi	Fasihi Simulizi hutungwa kwa muda mfupi au papo hapo	Fasihi Andishi hutungwa kwa muda mrefu
8	Mazingira ya uwasilishaji wake (mandhari)	Huambatana na tukio maalumu la jamii na wakati maalum k.v. usiku au kipindi fulani cha mwaka. mahali maalum k.v jandoni, matangani, arusini,	Mandhari ya kusomea huwa mahali popote.
9	Marekebisho	Mtunzi/msimulizi anaweza kurekebisha kazi yake wakati wa kuwasilisha au baadaye kidogo	Kitabu kikishaandikwa ni vigumu kukifanyia marekebisho mpaka toleo jipya litakapoandikwa
10	Uhifadhi	Huhidhiwa akilini (kichwani) kwa sehemu kubwa	Huhifadhiwa kwa njia ya maandishi (vitabu)
11	Gharama	Fasihi Simulizi ina gharama ndogo ukilinganisha na Fasihi Andishi	Fasihi Andishi ina gharama kubwa ukilinganisha na Fasihi Simulizi
12	Wahusika	Fasihi Simulizi ina wahusika wa kila aina k.v binadamu, wanyama na ndege, mazimwi na majitu, miungu, mizimu, mashetani na vitu visivyo na uhai k.v. mawe na miti	Fasihi Andishi hutumia wahusika wa kubuni ambao mara nyingi ni binadamu
13	Uhai	Fasihi Simulizi ni hai kwa sababu huwasilishwa ana kwa ana kwa vitendo	Fasihi Andishi si hai kuliko fasihi Simulizi

TOFAUTI KATI YA HADHIRA YA FASIHI SIMULIZI NA FASIHI ANDISHI

1. Hadhira ya fasihi andishi ni wasomaji (**msomaji**) lakini hadhira ya fasihi simulizi ni **msikilizaji** au mtazamaji.
2. Hadhira ya Fasihi Simulizi huweza kuwasiliana **moja kwa moja** na mwasilishaji ilhali ile ya Fasihi Andishi sio lazima iwasiliane na mwandishi.
3. Hadhira huchangia katika uwasilishaji wa Fasihi Simulizi k.v kwa kuimba, kupiga makofi n.k (**hadhira tendi/hai**) ilhali hadhira ya Fasihi Andishi haichangii katika uandishi.
4. Hadhira ya Fasihi Simulizi **huonana** na fanani (lazima iwe hapo) ilhali ile ya Fasihi Andishi si lazima ionane na mwandishi.
5. Hadhira ya Fasihi Simulizi ni **kubwa** kuliko ile ya Fasihi Andishi kwani huhusisha hata wasiojua kusoma na kuandika.
6. Hadhira ya Fasihi Simulizi ni **hai** yaani inajulikana na fanani ilhali ile ya Fasihi Simulizi si hai yaani haishirikiswi moja kwa moja na mwandishi.
7. Hadhira ya Fasihi Simulizi **hainunui** kazi ilhali ile ya Fasihi Andishi hununua kazi.
8. Hadhira ya Fasihi Simulizi yaweza **kumiliki** kazi ya fanani lakini ile ya Fasihi Andishi haiwezi kumiliki kazi ya mwandishi.
9. Hadhira ya Fasihi Simulizi **hubagua** kwa kulenga watu wa rika au jinsia fulani (mfano, miviga ya tohara) lakini Fasihi Andishi inaweza kusomwa na mtu yeyote ajuaye kusoma.
10. Hadhira ya fasihi simulizi ni **pana** (ni kila mtu katika jamii) lakini hadhira ya fasihi andishi ni ya wasomi pekee na wale wana uwezo wa kununua vitabu (inamtenga mtu ambaye hajui kusoma).

SIFA AMBAZO HUPOTEA FASIHI SIMULIZI INAPOANDIKWA

- i. **Sauti** – kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti hupotea. Hivyo, hisia na toni ya fanani hupotea.
- ii. **Uhai wa hadhira**- mbinu za ushirikishaji wa hadhira hupotea kwa vile hadhira hamwoni fanani moja kwa moja.
- iii. **Utendaji** – uigizaji, ishara za mwili, miondoko ya jukwaani na uchezaji hupotea.
- iv. **Maleba** – mavazi ya uigizaji hayapo katika mandishi, hivyo hupoteza taswira halisi.

FASIHI SIMULIZI

Fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo hubuniwa na huhifadhiwa akilini kisha kuwasilishwa na kusambazwa kwa kutumia mazungumzo ya mdomo (lugha na sauti) ili kufikisha ujumbe kwa hadhira.

- **Chimbuko La Fasihi Simulizi**

Aina hii ya fasihi ndiyo iliyokuwapo tangu zamani kabisa mwanadamu alipoanza kuishi, yaani ilianza pale mwanadamu alipochangamana na wenzake katika kufanya mambo mbalimbali, mfano, shughuli za biashara, kilimo, na nyinginezo. Mathalani, Jamii za wasasi na wachungaji huwa na fasihi simulizi inayohusiana na mazingira na kazi zao, nayo jamii ya wavuvi wa baharini ina fasihi simulizi inayohusu shughuli za uvuvi na baharini. Hususani kila jamii ina fasihi simulizi yake ingawa zote zina majukumu sawa. Fasihi simulizi ilianza kwa mazungumzo ya mdomo kisha ilianza kushirikishwa ngoma na ala nyingine za muziki, baadaye ikahifadhiwa kwa maandishi na mabadiliko makubwa zaidi ni kutumia vyombo vya kisasa kama vile redio, video, sinema n.k.

- **SIFA ZA FASIHI SIMULIZI**

1. Fasihi Simulizi ina sifa ya **utendaji** ambao hushirikisha fanani na hadhira kwa wakati mmoja. Hii humfanya fanani aweze kuonyesha baadhi ya matendo katika usimulizi wake kama vile kutumia viungo vya mwili kwa kucheza midomo, kukunja uso, kubinya macho, kucheza mabega n.k.

2. Fasihi simulizi ina sifa ya **kuwepo kwa fanani** ambaye huweza kusimulia kwa kuimba, kusoma kwa sauti au kubadilisha mtindo wa usimuliaji wake. Fanani huweza kufanya yote hayo ikiwa ataona hadhira yake imechoka kusikiliza. Pia ana uwezo wa kuona kama ujumbe wake umeeleweka au la!

3. Fasihi Simulizi Ina sifa ya kuwepo kwa washirikishwaji wa fanani na hadhira. **Hadhira hushiriki** kwa kuuliza maswali, kupiga makofi na kuimba kutegemea jinsi atakavyoishirikisha.

4. Fasihi Simulizi zina sifa ya kwenda na **wakati na mazingira**. Tabia hii inatokana na jinsi fasihi simulizi inavyoenea wasikilizaji huwa wengi na hata kama tanzu za fasihi simulizi zilipitwa na wakati zinaweza kubadilishwa na fanani ili zisadifu mazingira maalumu ya wakati huo.

5. Fasihi Simulizi **huzaliwa, hukua, huishi hata kufa**. Hii inasababishwa na mabadiliko ya mazingira ambayo hufuata mfumo wa kihistoria wa jamii, mfano kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ya kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi ya fasihi simulizi huonekana chapwa kwa sababu ya mambo kama vile miondoko au ngoa, vinakuwa havimo.

6. Fasihi simulizi ina sifa ya kuwa na **uwanja maalumu wa kutendea**. Fasihi simulizi huwa na sehemu kwa ajili ya aina fulani ya Fasihi Simulizi itakayofanyika na wahusika, mfano, tambiko huwa na sehemu maalumu ya kutambikia kama vile sehemu yenye pango, kwenye mti mkubwa kama vile mbuyu, njia panda, makaburini n.k. Hivyo, ni wazi kwamba Fasihi Simulizi inahitaji uwanja wa kutendea yenye kuhusisha vitendo.

7. Fasihi Simulizi Ina sifa za kuwa **mali ya jamii** nzima. Tanzu zake zote zikishatendwa humilikiwa na jamii kwa pamoja na hii ndiyo inayopatiwa uwezo wa kurithishwa kizazi kimoja hadi kingine. Hivyo huwafikia watu wengi hata wale wasiojua kusoma na kuandika.

• **MAJUKUMU YA FASIHI SIMULIZI/UMUHI MU WA KUFUNZA FASIHI SIMULIZI KATIKA SHULE ZA UPILI**

1. Kuburudisha - kustarehesha, kufurahisha, kuchangamsha, kutuliza, kulisimua na kupumbaza akili na kiwiliwili – nyimbo, hadithi, vitendawili
2. Kufunza maadili kwa wanajamii kwa kuwahimiza kuiga sifa chanya na kukataa sifa hasi za wahusika.
3. Kukuza uwezo wa kufikiri/kudadisi k.m vitendawili na chemshabongo.
4. Kufariji k.m mbolezi na methali k.m. 'Baada ya dhiki faraja

5. Vipengele vya fasihi simulizi k.v mashairi, nyimbo, nahau, hutumiwa katika uandishi wa fasihi andishi.
6. Kuhifadhi historia ya jamii k.m. mighani, visaviini, mapisi, tarihi n.k.
7. Kukejeli tabia zinazokiuka matarajio ya jamii k.v sogu, methali, n.k.
8. Kuendeleza tamaduni za jamii kwani husawiri imani na desturi za jamii. k.v kitendawili
Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini siwezi kulichuma.' – Mtu hawezi kumwoa dadake.
9. Kuunganisha watu pamoja kwa kuwajumuisha pamoja wakati wa ngoma, kuimba, utambaji, n.k.
10. Kukuza lugha k.v. misimu inapokua kimatumizi na kujumuishwa katika lugha sanifu.
10. Kukuza uwezo wa kutumia lugha kadiri mtu anapoendelea kuwasilisha k.v. hotuba na vitanza ndimi, husaidia kuboresha matamshi na kutofautisha maana za maneno.
11. Hukuza uwezo wa kubuni k.v. malumbano ya utani, vitanza ndimi na ngonjera, n.k.
12. Kukuza uzalendo kwa kufanya wanajamii kuonea fahari jamii zao na kuiga mashujaa au watu waliotendea jamii makuu.
13. Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, n.k.

● **MAMBO AMBAYO HUCHANGIA KUBADILIKA KWA FASIHI SIMULIZI**

- 1) **Hadhira** - fanani kulazimika kubadilisha mtindo wa uwasilishaji ili kukidhi mahitaji ya hadhira yake.
- 2) **Fanani** - kila fanani ana mtindo wake tofauti wa uwasilishaji. Kwa mfano matumizi ya mbinu ya ufaraguzi miongoni mwa fanani mbalimbali.
- 3) **Teknolojia** - mambo ya zamani kubadilika kutokana na athari za teknolojia ya kisasa hasa taknologia, Mfano, Video- kazi za kisanaa zilizorekodiwa hutofautiana na zile za kuwasilishwa moja kwa moja kutokana na kuathiriwa kwa sauti na picha wakati wa kurekodi.
- 4) **Wakati** - kadiri wakati unavyoendelea kupita, ndivyo mambo mengi katika maisha ya jamii huweza kubadilika. Mambo hayo huweza kuleta athari ya mabadiliko katika sanaa ya jamii.

- 5) **Mazingira** - kuhama kwa watu katika eneo fulani kunaweza kuwanyima mahali mahususi pa kuwasilishia kazi fulani, kwa mfano miviga.
- 6) **Uhamaji na uhamiaji** - kuingiliana kwa tamaduni mbalimbali kunaweza kuathiri jinsi kazi fulani ilivyokuwa tangu mwanzo iwapo kutakuwa na kukopa baadhi ya vipengele vya sanaa ya jamii moja na kuvijumuisha na vya jamii nyingine.
- 7) **Maandalizi** - Fasihi Simulizi inapohifadhiwa kwa maandishi huwa si ya mdomo tena bali ni ya kusomwa.
- 8) **Ukengeushi wa jamii** - watu wanaacha utamaduni wao na hivyo baadhi ya vipera vya fasihi simulizi huweza kutoweka au vikawa vinajitokeza kwa nadra sana, mfano, wazazi wako kazini hadi usiku hawapati nafasi za watoto ambao pia wanatoka shule na kuendelea kufanya kazi za walimu.
- 9) **Utafiti** - watu kujijazia kile wasichokijua bila kufanya utafiti wa kutosha, bila ya kwenda nyanjani ilipo jamii husika ili kupata taarifa kamili.

● **VIPENGELE MUHIMU VYA FASIHI SIMULIZI**

(a) **Fanani (Msanii)**

Huyu ni mtu ambaye anatunga na kuwailisha fasihi simulizi; mfano, kutamba hadithi, kuimba wimbo, kutega vitendawili au methali.

(b) **Wasikilizaji au watazamaji (Hadhira)**

Hawa ni watu ambao hushiriki katika kutazama au kusikiliza fani ya Fasihi Simulizi na mara nyingine huwa wanatumiwa na fanani kama wahusika katika fani yake.

(c) **Mandhari**

Hili ni jukwaa au mahali ambapo tukio la kifasihi (Fasihi Simulizi) litatendeka. Pahali au mahali hapo paweza kuwa nyumbani, uwanjani, kuzunguka moto, baharini n.k.

(d) **Tukio/Dhana inayotendeka**

Hili huwa ni tendo linalotendeka kwa jukwaa la Fasihi Simulizi. Tendo hili Laweza kuwa ni usimulizi wa hadithi, kutega vitendawili, kuimba nyimbo au wimbo au kutoa methali.

ISTILAHU KATIKA KAZI YA FASIHI SIMULIZI

- 1) **Michepuko:** Michepuko katika usimulizi wa hadithi ni namna ya kuacha kwanza kusimulia hadithi moja kwa moja na kuongelea mambo mengine

kwa ufupi. Yaani kutolea mifano ya mambo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha halisi ya jamii.

- 2) **Fantasia:** Fantasia ni hali ya ujabu au undotondoto unaojitokeza katika kazi za fasihi mf; njozi, majitu ya kutisha, nguvu zisizo za kawaida, na kadhalika. Mambo ya kifantasia sio ya kweli yaani hayawezi kutokea na hayatarajiwi kutokea isipokuwa hutumiwa kwa makusudi ili kukidhi haja fulani za kifasihi
- 3) **Ufaraguzi:** ni hali ya kuunda upya au kubadilisha usimulizi moja kwa moja wakati fanani anapowasilisha jukwaani. Ufaraguzi hutokea kwa sababu ya mabadiliko mfano; hadhira au pia fanani kusahau kipera hicho.
- 4) **Wahusika:** ni viumbe wa sanaa ambao hutumiwa wakati kazi ya fasihi kuwasilisha maswala mbalimbali.

AINA ZA WAHUSIKA

- 1) **Fanani** – ni mtu anayetunga na kuwasilisha kipera cha Fasihi Simulizi mbele ya hadhira.

<u>Aina Za Fanani</u>	<u>- Kipera</u>
1. Mtambaji/msimulizi	– Hadithi
2. Mwimbaji	– Wimbo
3. Malenga	– Shairi
4. Sogora	– Ngomezi
5. Mwigizaji	– Maigizo
6. Mlumbi	– Mazungumzo. n.k

- 2) **Hadhira** – ni watu ambao husikiliza, kutazama, kushiriki kwa kuimba, kuuliza maswali, kutegua vitendawili, kupiga makofi n.k. Wakati fanani anapowasilisha jukwaani. Kuna aina mbili za hadhira:

(i) *Hadhira tendi/hai*

(ii) *Hadhira tuli pia hadhira bubu*

- 3) **Wanyama** – ni wahusika wanaofanya kama binadamu na kuwakilisha sifa kama vile ujanja, ulaghai, tamaa na ujinga. Mifano, Ndege, Nyani, Sungura, Fisi, n.k.

Wahusika wanyama ni wa aina mbili

- a) *Wanyama wenye tabia za binadamu na wanatenda kama binadamu*
- b) *Wanyama watendao kama wanyama tu. Kila mnyama huwasilisha sifa Fulani za binadamu. Mfano;*
 - *Sungura – huwakilisha watu wadogo lakini wenye ujanja na akili nyingi.*
 - *Kobe – huwakilisha watu wapole lakini wenye busara na hekima.*
 - *Wakubwa – huwakilisha watu wenye kiburi na ujeuri lakini bila busara.*

- 4) **Binadamu** – Ni mtu aliye ndani ya kipera cha fasihi (anaweza kuwa mtu wa kweli au wa kufikirika tu)
- 5) **Mazimwi na majitu** - viumbe wenye matendo na maumbile ya kutisha kama vile jicho moja, vichwa viwili au zaidi, nusu mtu na nusu mnyama, wenye tamaa iliyokithiri ya kuweza kumeza kila kitu.
- 6) **Wahusika vitu** - (visivyo na uhai) mawe, miti, vijaluba, vibuyu-hutumiwa kuibua imani za kidini. Mbinu hii huitwa Uhaishaji
- 7) **Mizimu** - roho za waliokufa-hutembea, hula na huathiri binadamu.
- 8) **Miungu** - viumbe wenye uwezo mkubwa dhidi ya binadamu k.m. katika mighani na visasili.

UFARAGUZI

Sababu za Ufaraguzi/Kubadilika kwa Fasihi Simulizi

1. Sababu ya kuwasilishwa vibaya.
2. Fanani kusahau na kubadilisha yaliyomo na mtiririko.
3. Kubadilisha ili kukidhi mahitaji ya hadhira k.m. umri na uelewa wao- kutumia lugha nyepesi kwa watoto na pevu kwa watu wazima.
4. Mabadiliko ya mandhari/mazingira - vitu vilivyo katika mazingira halisi kukosekana katika mazingira ya usimulizi na msimulizi kutumia vitu katika mazingira yake vinavyokaribiana navyo.
5. Kutoeleweka vizuri na hivyo kuhifadhiwa vibaya.
6. Mabadiliko ya wakati k.m kitendawili cha wakati wa mkoloni kutumia mzungu na cha wakati wa mwarabu kutumia mwarabu na maana ni ile ile - Mzungu/Mwarabu amesimama kwa mguu mmoja-mwavuli.
7. Mabadiliko ya falsafa ya vizazi na maingiliano katika jamii kusababisha kurithisha tu yale ambayo ni muhimu na kuacha mengine.
8. Kila fanani huwa na mtindo wake wa kuwasilisha kisanii.
9. Ubunifu wa fanani ili uwasilishaji uweze kuvutia zaidi na uwezo wake wa lugha.
10. Teknolojia kusababisha kuhifadhiwa na hivyo kuiua.

MAJUKUMU YA FANANI

1. Kubuni/ kutunga fani ya Fasihi Simulizi, ikiwa anawasilisha fani iyo kwa mara ya kwanza.
2. Kuhifadhi kipera cha fasihi Simulizi, hivyo anasaidia kuhifadhi utamaduni.

3. Anasaidia kusambaza/ kueneza kipera hicho kwa Jamii.
4. Kutafiti habari kuhusu kipera atakachowasilisha.
5. Kuhakikisha hadhira yake iko makini kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwasilishwaji bora.
6. Fanani ndiye hutimiza majukumu ya Fasihi Simulizi kwa jumla, kama vile, kuelimisha, kuburudisha, kuonya jamii n.k.

JINSI YA KUSHIRIKISHA HADHIRA KATIKA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI

- i. Kwa kuuliza maswali na kujibu maswali, pia kutoa maoni.
- ii. Kupiga makofi, kushangilia na kuonyesha hisia (kucheka, kutabasamu au kununa).
- iii. Kuanzia wimbo na kuwaacha hadhira iimbe kibwagizo
- iv. Kuanzishia semi ambayo hadhira wanaijua na kuwachia waikamilishe
- k.v. kumamilisha methali na kutegua vitendawili.
- v. Kwa kuwauliza maswali balagha.
- vi. Kufanya mzaha, kutia chumvi na pia kumkosoa fanani.
- vii. Kuitumia hadhira kama mifano halisia wa kuelezea jambo.
- viii. Kuwaomba baadhi ya hadhira waigize sehemu za wahusika.

***Tanbihi:** Hizi ndizo sifa za hadhira hai/tendi.

TANZU ZA FASIHI SIMULIZI

Tanzu ni aina za tungo zenye muundo uliokaribia kufanana.

Mbinu zifuatazo ndizo hutumiwa ili kuainisha tanzu za fasihi simulizi.

(a) Kimtindo, (b) Uwasilishaji, (c) Kimuundo

• **Kuna Tanzu Tano Kuu Za Fasihi Simulizi, Nazo Ni:**

1. Utanzu wa Hadithi
2. Utanzu wa Ushairi Simulizi
3. Utanzu wa Semi
4. Utanzu wa Maigizo
5. Utanzu wa Mazungumzo

Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi

Kipera ni utungo wa fasihi simulizi unaowasilishwa mbele ya watu. Kila utanzu una vipera vyake

HADITHI	USHAIRI SIMULIZI	SEMI	MAZUNGUMZO	MAIGIZO
<p>●<u>Ngano za kubuni</u></p> <p>hurafa hekaya mazimwi mtanziko soga</p> <p>●<u>Hadithi za kishujaa</u></p> <p>visakale visaviini tahiri mapisi mighani kumbukumbu</p>	<p>Nyimbo</p> <p>Maghani</p> <p>Ngonjera</p> <p>Rara</p> <p>Mashairi mepesi</p>	<p>Methali</p> <p>Vitendawili</p> <p>Mafumbo</p> <p>Vitanza ndimi</p> <p>Misemo/nahau</p> <p>Lakabu</p> <p>Misimu</p> <p>Chemshabongo</p>	<p>Hotuba</p> <p>Malumbano ya utani</p> <p>Soga</p> <p>Mawaidha</p> <p>Ulimbi</p> <p>Maapizo</p>	<p><u>Maigizo ya kawaida</u></p> <p>Michezo ya kuigiza Ngonjera Vichekesho Michezo ya Watoto Majigambo/vivugo</p> <p><u>Sanaa ya maonyesho</u></p> <p>Ngomezi Miviga Matambiko Sanaa ya ngoma Ramli</p>

JITATHMINI 1

1. *Eleza maana ya istilahi zifuatazo (alama 5)*
 - 1). *fanani*
 - 2). *sanaa*
 - 3). *hadhira*
 - 4). *ufaraguzi*
 - 5). *riwaya*
2. *Fafanua aina zozote sita za wahusika katika Fasihi Simulizi. (alama 6)*
3. *Linganisha na ulinganue sifa za Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi (alama 10)*
4. *Jadili tofauti zilizoko kati ya **hadhira** wa fasihi simulizi na **hadhira** wa fasihi andishi alama (10)*
5. *Eleza mambo ambayo huchangia mabadiliko ya kazi za Fasihi Simulizi (alama 6)*
6. *Mambo gani uweza kupotea ikiwa fasihi simulizi itaandikwa. (alama 6)*
7. *Jadili mchango wa hadhira kwa kufanikisha uwasilishaji wa fani yoyote ile ya fasihi simulizi (alama 6)*

UTANZU WA HADITHI

MAANA YA HADITHI

Hadithi ni masimulizi yanayowasilishwa kwa lugha ya nathari kuhusu watu, matukio na mahali mbali mbali.

SIFA ZA HADITHI

1. Hutumia lugha ya mtiririko au nathari-kueleza matukio moja kwa moja.
2. Hurithishwa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
3. Huwasilishwa mbele ya hadhira
4. Hutambwa mahali maalum k.v. ndani ya nyumba, chini ya mti, uwanjani, n.k.
5. Huweza kutokana na matukio halisi (kihistoria) au ya kubuni.
6. Huwa na mafunzo fulani kwa jamii/hadhira.
7. Hutumia wahusika wa aina tofauti tofauti k.v. watu, wanyama, ndege, mazimwi, n.k.
8. Hutumia aina nyingine za sanaa k.v nyimbo, methali, ushairi n.k.
9. Huwa na utendaji k.v. mtambaji kuiga fisi anavyokula.
10. Aghalabu hutambwa wakati wa jioni.

SABABU ZA NGANO KUTAMBWA JIONI/USIKU

1. Ndio wakati watu walikuwa wamejumuika nyumbani baada ya kazi.
2. Utambaji ulikuwa njia ya kupitisha wakati chakula kikingojewa.
3. Wakati huu ulihakikisha mwanajamii hapotezi wakati wa kazi.

MAJUKUMU YA HADITHI

1. Kufunza maadili yaliyo nguzo kuu kwa wanajamii.
2. Kukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani.
3. Kuburudisha baada ya kazi ya kutwa.
4. Kukuza uwezo wa watoto wa kukumbuka ili kutamba baadaye.
5. Kueleza asili ya mambo k.m visaviini, visasili na ngano za usuli.
6. Kutahadharisha wanajamii dhidi ya kufanya mambo yasitofaa.

7. Kuunganisha watu katika jamii wanapojumuika pamoja kusikiliza utambaji.
8. Ngano za mtanziko hukuza uwezo wa kutathmini na kutoa uamuzi ufaao.
9. Kukuza lugha hasa kwa hadhira ya watoto.
10. Kuhifadhi na kuendeleza historia ya jamii k.v. mighani, tarihi, n.k.
11. Kuelimisha hadhira kuhusu utamaduni wao.
12. Njia ya kupokeza kizazi historia na utamaduni wa jamii.

SIFA ZA MTAMBAJI/MGANAJI BORA

1. Awe jasiri ili aweze kuzungumza hadharani.
2. Asiwe na haya ili kuweza kuzungumzia mambo ya aibu inapobidi.
3. Awe na uelewa wa mazingira na masuala ibuka katika jamii ili kuweza kuwasilisha dhana zisizopakana katika mazingira yake k.m. kutumia rais kuelezea dhana ya mfalme.
4. Awe na ufahamu mpana wa lugha ili aweze kuitumia kwa uhodari na kuwasilisha kwa wepesi.
5. Awe mchangamfu na mcheshi ili kunasa makini ya hadhira na kuzuia ukinaifu.
5. Awe na ufahamu mpana wa utamaduni husika ili kuzuia kutumia maneno na ishara zinazoweza kuwaudhi au kupingana na imani za hadhira.
6. Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira k.v. kuimba, maswali ya balagha ili hadhira isikinai, n.k.
7. Aweze kujua, matarajio, kiwango cha elimu na tajriba ya hadhira ili kuweza kubadilisha kwa kiwango kinachofaa.
8. Awe na uwezo wa kuingiliana vizuri na hadhira ili hadithi yake ivutie.
9. Awe na kumbukumbu nzuri ili usimulizi wake utiririke vizuri.
10. Awe na uwezo wa kudramatisha ili kuonyesha picha fulani k.v. kuiga toni, sauti, na kiimbo kulingana na swala analowasilisha.
11. Kubadilisha toni au kiimbo (kupandisha na kushusha sauti) ili hadhira isikinai.
12. Awe na ujuzi wa kutumia ishara za uso, mwili na miondoko kulingana na hali anayoigiza.
13. Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
14. Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazosimulia k.v. huzuni
15. Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira kwa nyimbo na maswali ya balagha ili kuondoa uchovu wa kutazama na kusikiliza.

16. Awe na uwezo wa ufaraguzi/kubadilisha utambaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika kutoka katika mazingira ya hadhira.
17. Awe na uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusesitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

AINA ZA HADITHI

1. NGANO/ HADITHI ZA KUBUNI

Ni utungo wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha nathari kwa kusudi la kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. sio za ukweli.

2. HADITHI ZA KISALUA/KIHISTORIA

Hadithi zinazosimulia matukio yaliyowahi kutendwa na wahusika waliowahi kuishi. Ni za ukweli ingawa huongezewa ubunifu ili kuvutia zaidi.

NGANO / HADITHI ZA KUBUNI	HADITHI ZA KIHISTORIA
1) <i>Hurafa</i> 2) <i>Hekaya</i> 3) <i>Visaasili</i> 4) <i>Za usuli</i> 5) <i>Mazimwi</i> 6) <i>Mtanziko</i> 7) <i>Soga</i>	1) <i>Mighani</i> 2) <i>Visakale</i> 3) <i>Visaviini</i> 4) <i>Mapisi</i> 5) <i>Tarihi</i> 6) <i>Kumbukumbu</i>

1. NGANO/Hadithi za Kubuni

Sifa Za Ngano/ Hadithi Za Kubuni

1. Zina fomyula ya kuanzia/mwanzo maalum.
2. Zina fomyula ya kumaliza/mwisho maalum.
3. Zina wahusika aina mbalimbali.
4. Zina matumizi ya nyimbo.
5. Hutumia takriri (usambamba) ili kusesitiza k.m. zimwi likakimbia, likakimbia.
6. Huwa na na maadili/mafunzo
7. Hutumia maswali ya balagha kuongeza taharuki.
8. Hutumia tanakali za sauti.

9. Zina matumizi ya fantasia au matukio yanayokiuka uhalisi/mambo ya ajabu k.v. binadamu kuruka kama ndege, zimwi kumeza watu na baadaye kutapika wote, n.k.

● **MUUNDO WA HADITHI;**

Muundo wa hadithi za Fasihi Simulizi ni wa moja kwa moja. Kimuundo, hadithi huwa na sehemu tatu (**3**) ambazo ni: mwanzo, kati na mwisho.

1. **Mwanzo**

Mwanzo wa hadithi huanza kwa maneno maalumu.

Mfano:

Mtambaji: Hadithi... Hadithi....!

Hadhira: Hadithi njoo! Utamu Kolea

Au

Mtambaji: Paukwa.....!

Hadhira: Pakawa.....!

2. **Kati**

Hapa habari zote kuhusu hadithi huelezwa katika sehemu hii. Hapa matukio muhimu husimuliwa kwa kufuata maelezo ya moja kwa moja.

3. **Mwisho**

Hapa msimuliaji wa hadithi huonyesha mafanikio au matatizo yaliyomkuta mhusika. Msimulizi humalizia kwa kusema, “Hadithi yangu imeishia hapo”.

Aina Za Fomyula Za Kuanzia/Mianza Maalum

1. Paukwa, Pakawa. Sahani. Ya mchele. Giza. La mwizi. Na kiboko je? Cha mtoto mkorofi...

2. Hapo zamani za kale/zama za kongamawe... Ilitokea...

3. Hadithi! Hadithi! ... Hadithi njoo...

4. Kaondokea chenjagaa, kajenga nyumba kakaa, mwanangu mwanasiti, kijino kama chikichi, cha kujengea kikuta, na vilango vya kupita...

5. Hapo jadi na jadudi...

Umuhimu Wa Fomyula Ya Kuanzia/Mwanzo Maalum

1. Kuvuta makini ya hadhira.

2. Kumtambulisha mtambaji kwa hadhira.
3. Kuashiria mwanzo wa hadithi.
4. Kutoa hadhira kutoka ulimwengu halisi hadi ule wa hadithi.

Aina Za Fomyula Za Kumalizia/Miishio Maalum

- 1) Hadithi inaishia hapo.
- 2) Tangu siku hiyo...
- 3) Wakaishi raha mustarehe.
- 4) Maadili, funzo... Hadithi hiyo inatufunza kuwa...

Umuhimu Wa Fomyula Ya Kumalizia/Mwisho Maalum

- a. Kuashiria mwisho wa hadithi.
- b. Kutoa hadhira katika ulimwengu wa hadithi hadi ule halisi.
- c. Kumpisha/kumpa fursa mtambaji anayefuata.
- d. Kupisha shughuli inayofuata.
- e. Kutoa funzo la hadithi kwa muhtasari.
- f. Kupa hadhira nafasi ya kupumzika baada ya kuwa makini kwa muda.

UMUHIMU WA NYIMBO KATIKA NGANO

1. Kushirikisha hadhira kwa kuimba.
2. Kuisimua hadhira na kuondoa ukinaifu
3. Kuteka makini ya hadhira.
4. Kuwasilisha mafunzo/maadili.
5. Kutenganisha matukio katika hadithi.
6. Kuburudisha hadhira.
7. Kupunguzia hadhira mwemeeo.

UMUHIMU WA TANAKALI ZA SAUTI / ONOMATOPEY A KATIKA NGANO

1. Kuongeza utamu.
2. Kusaidia msomaji kupata picha kamili.
3. Kusaidia kupata hisia halisi

AINA ZA NGANO / HADITHI ZA KUBUNI

Aina za Ngano za kubuni:
- hurafa, - hekaya - visaasili, - ngano za usuli - mazimwi, - mtanziko, - soga

1. HURAFU

- Hadithi zenye wahusika wanyama na ndege.
Hurafa ni hadithi ambazo wanyama na ndege hupewa sifa za binadamu na kufanya shughuli kama za binadamu, km, kulima, kufanya harusi. nk.

Sifa Za Ngano Za Hurafa.

1. Wahusika ni wanyama na au ndege.
2. Wanyama na ndege hupewa sifa za binadamu
3. Ni kazi ya ubunifu - sio za kweli
4. Hutoa mafunzo kwa njia ya kuchekesha na isiyomiza.
5. Huwa na ucheshi mwingi.
6. Hutumia mbinu ya uhaishaji.
7. Huwa na sifa zinazohimizwa na zinazoshutumiwa.

Umuhimu Wa Ngano Za Hurafa

1. Kutahadharisha watu dhidi ya kuwa wadanganyifu/kudanganyika kwa urahisi.
2. Kuonyesha jinsi tabia ya udanganyifu inavyoweza kujitokeza na kuathiri watu.
3. Hurafa za kijanja hufunza jinsi ya kupambana na hali ngumu.

2. HEKAYA/NGANO ZA KIAYARI

Hekaya ni hadithi ambazo huwa na mhusika mmoja mjanja au mwerefu kuliko wenzake. Mhusika huyu hutumia ujanja kujinufaisha kutoka kwa mhusika mwingine anayedanganyika kwa wepesi, kwa mfano, Hekaya za Abunuwasi, hadithi za sungura mjanja n.k.



Sifa Za Ngano Za Hekaya

1. Wahusika wakuu ni binadamu.
2. Huwa na ubunifu mkubwa.
3. Hustaababisha na kuchekesha.
4. Ujanja na uongo hujitokeza.
5. Ushindi hujitokeza.
6. Ni za kubuni.

Umuhimu Wa Ngano Za Hekaya

1. Hutahadharisha watu dhidi ya kuhadaika kwa wepesi.
2. Huonya dhidi ya matokeo yanayoweza kuwapata wanaojinyakulia mali kwa udanganyifu.
3. Kuonya dhidi ya usaliti.
4. Kukashifu viongozi dhalimu na matendo maovu.
5. Kukejeli wanaotumia nguvu badala ya akili/hekima.

3. VISASILI

Hadithi zinazoeleza asili ya matukio fulani katika jamii k.m. kifo, jua, lugha, zilizala n.k.

Sifa Za Ngano Za Visasili

1. Husimulia mambo ya kiimani na kidini.
2. Huwa na misingi ya kihistoria.
3. Hueleza asili ya matukio katika jamii.
4. Wahusika ni wanyama na binadamu.
5. Huwa na maadili.
6. Hurithishwa kizazi hadi kingine.

Umuhimu Wa Ngano Za Visasili

1. Kueleza asili ya mambo kama vile kifo, utamaduni n.k.
2. Kueleza utaratibu wa kutekeleza desturi k.v. mahari.
3. Kuhalalisha baadhi ya mila na desturi za jamii k.v. ulipaji mahari, uabudu mi, n.k.

4. Kutilia mizizi imani fulani ya watu.
5. Kupunguza athari za majanga kama vile kuhalalisha kifo.
6. Kutambulisha jamii kwani kila jamii ina aina yake ya visasili.
7. Kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii



4. NGANO ZA USULI

Hadithi zinazoeleza asili ya hali, tabia, mahusiano au wasifu. k.v. asili ya kuku kuchakura, asili ya kinyonga kwenda kwa tahadhari, n.k.

Sifa Za Ngano Za Usuli

1. Wahusika ni wanyama na binadamu
2. Ni kazi ya kubuni.
3. Hueleza kuhusu asili ya sifa, tabia au hali.
4. Hutumia mbinu ya uhuishi.
5. Huwa na maadili.

Umuhimu Wa Ngano Za Usuli

1. Kueleza sababu ya tabia, hali au sifa fulani.
2. Kuonya dhidi ya tabia hasi kama vile ulafi.

5. NGANO ZA MAZIMWI

Hadithi ambazo wahusika ni mazimwi. Viumbe wa kutisha, wanamaumbile ya ajabu kama vile, jicho moja, vichwa viwili, pembe. n.k

Sifa Za Ngano Za Mazimwi

1. Wahusika ni mazimwi
2. Mazimwi huwakilisha sifa hasi za binadamu k.m ulafi, uka li, uovu n.k.
3. Hujaa uharibifu.
4. Huwa na matumizi mengi ya fantasia.
5. Kipengele cha safari hujitokeza k.v. kwenda nchi za mbali kutafuta suluhisho.
6. Ushindi hujitokeza (mazimwi hushindwa).
7. Ni kazi ya kubuni.
8. Huwa na maadili.

9. Mazimwi huwa na sifa zinazokiuka mipaka ya binadamu k.m. kinywa kisogoni, jicho moja kubwa, n.k.

Umuhimu Wa Ngano Za Mazimwi

1. Kukashifu tabia ya uovu, ulafi, na ukali.
2. Kutahadharisha dhidi ya kuwa na ulafi, ukatili n.k
3. Kutahadharisha watu wawe makini.
4. Kutia moyo waliodhulumiwa kuwa waliowanyanyasa wataadhibiwa siku moja.

6. NGANO ZA MASHUJAA

Ni ngano ambazo zinahusu watu waliotenda matendo ya kishujaa katika jamii zao kama vile kuokoa jamii kutoka kwa janga hatari.

Sifa Za Ngano Za Mashujaa

1. Kipengele cha motifu au kusafiri nchi za mbali, kupigana na mazimwi kuokoa jamii.
2. Husawiri mapigano kati ya wema (lila) na ubaya (fila).
3. Uovu huwakilishwa na mazimwi au viongozi dhalimu
4. Hatimaye wema hushinda uovu kwa juhudi za mashujaa

****Tanbihi:** Ngano za **mashujaa** ni za kubuni ilhali katika **mighani**, mashujaa wanaaminiwa waliishi.*

Umuhimu Wa Ngano Za Mashujaa

1. Kuhimiza uzalendo na ujasiri miongoni mwa vijana.
2. Kuhimiza ujasiri miongoni mwa vijana.
3. Kusifu mashujaa katika jamii
4. Kuelimisha jamii kwa kuwapa maarifa ya kukabiliana na changamoto, inda na ila.
5. Kuhimiza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga mashujaa na kupigania jamii.
6. Kuonya dhidi ya matendo hasi k.v. ukali.
7. Kuhimiza watu kutokata tamaa

7. NGANO ZA MTANZIKO

Hadithi ambapo mhusika hujikuta katika njia-pand yaani anakabiliwa na hali ngumu ya kuamua baina ya mambo wawili au zaidi yanayomkabili.

Sifa Za Ngano Za Mtanziko

1. Wahusika ni wanyama au binadamu.
2. Ni kazi ya kubuni.
3. Mhusika hulazimika kufanya uteuzi mgumu.
4. Hali mbili au zaidi zinazotatanisha huwepo.

Umuhimu Wa Ngano Za Mtanziko

1. Hutuerevusha jinsi ya kupambana na hali ngumu.
2. Kuonya/kutahadharisha dhidi ya kujiponza.
3. Kukuza uwezo wa kupima mambo na kuteua lililo muhimu.
4. Kuonya dhidi ya kutenda bila kuwaza kwa kina.

8. NGANO ZA KIMAFUMBO

Ngano ambazo huwa na maana ya ndani/iliyofichika. Mifano; istiara na mbazi.

a. ISTIARA

Hadithi ambayo maana yake huwakilisha maana nyingine iliyofichika k.v. hurafa ambapo wanyama huwakilisha binadamu.

b. MBAZI

Hadithi fupi inayotolewa kama mfano kumkanya au kumwelekeza mtu k.v. katika biblia.

2. HADITHI ZA KISALUA/ KIHISTORIA

- Hadithi zinazosimulia matukio yaliyowahi kutendwa na wahusika waliowahi kuishi. Ni za ukweli ingawa huongezewa ubunifu ili kuvutia zaidi.

AINA ZA HADITHI ZA KIHISTORIA/ HADITHI ZA KISALUA	
- mighani,	- visakale,
- visaviini,	- mapisi,
- tarihi,	- kumbukumbu

1. MIGHANI

Hadithi za mashujaa/majagina wa jamii fulani k.m. Rwanda Magere wa Waluo, Fumo Liyongo wa Wapate, Koome Njue wa Wameru, Wangu wa Makeri wa Wakikuyu na Syokimau wa Wsakamba.

Sifa Za Hadithi Za Mighani

1. Huhusu mashujaa wa jamii fulani.
2. Wahusika hupambana na hali ngumu inayosababishwa na maadui.
3. Wahusika hupewa sifa na uwezo usiokuwa wa kawaida k.v. ukubwa wa ajabu, nguvu katika kivuli, nguvu katika nywele, kutouluka n.k.
4. Wahusika hupigania haki za wanyonge.
5. Mhusika hukomboa jamii yake dhidi ya maadui.
6. Mhusika hufa kifo cha huzuni (tanzia) kwa kusalitiwa na mtu wa karibu k.v. mwanamke au jamaa zao.
7. Mashujaa huuliwa kwa njia ya ajabu kama vile kunyolewa nywele, kivuli kuchomwa mkuki, kuchomwa sindano ya shaba kitovuni.
8. Mighani huzungumzia matukio ya kihistoria.
9. Kuna tabia ya kupiga chuku matukio yaliyo hadithini.
10. Mighani hurithishwa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
11. Huchukuliwa na jamii kama hadithi zenye ukweli na jamii hujinasibisha na mighani hiyo.
12. Husimulia mambo ya kiimani na kidini.

Umuhimu Wa Hadithi Za Mighani

1. Kutambulisha jamii kwani kila jamii ina aina yake ya mighani.
2. Kuhifadhi na kuKumbusha historia ya jamii.
3. Kusifu mashujaa katika jamii.
4. Kuhimiza ujasiri miongoni mwa vijana.
5. Kuelimisha jamii kwa kuwapa maarifa ya kukabiliana na adui au changamoto.
6. Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga mashujaa na kupigania jamii.
7. Kuonya dhidi ya matendo hasi kama vile usaliti.
8. Kuhimiza watu kutokata tamaa.

TOFAUTI KATI YA MIGHANI NA VISASILI

Mighani	Visasili
a) Husimulia kuhusu mashujaa.	a. Husimulia asili ya vitu.
b) Husimulia historia ya jamii.	b. Husimulia mianzo ya vitu au mambo.
c) Wahusika wakuu ni majagina.	c. Wahusika ni k.v. binadamu, miungu, wanyama, n.k.
d) Hueleza sifa za majagina.	d. Hueleza mianzo ya desturi.

2). VISAKALE

Masimulizi ya matukio yaliyotendeka zamani k.v.

- o vita, majanga kama njaa na magonjwa na hamahama za jamii k.v. Waisraeli kutoka Misri.

3). VISAVIINI

- o Hadithi zinazoeleza chimbuko la jamii Fulani
 - *Asili ya wakikuyu*
 - *Chimbuko la wameru*

4). MAPISI

- o Maelezo ya kihistoria yasiyo na ubunifu wowote k.v. chimbuko la kundi la wabantu kutoka Afrika ya kati na kuenea sehemu mbalimbali za Afrika.

5). TARIHI

- o Maelezo kuhusu matukio ya kihistoria kulingana na yalivyofuatana ki wakati

6). KUMBUKUMBU

- o Maelezo ya kitawasifu kuhusu mtu au jamii inayotambulika kwa kutoa mchango fulani mkubwa.

VIPERA VINGINE VYA HADITHI

1. SOGA

2. Hadithi fupi za kuchekesha zinazolenga kutania au kudhihaki.

Sifa Za Ngano Za Soga

1. Wahusika ni wa kubuni.
2. Hutaja ukweli unaoumiza.
3. Hutumia vichekesho kupunguza ukali wa dhihaka.
4. Hutumia chuku kupita kiasi.
5. Huhusu tukio moja.
6. Ni fupi.

Umuhimu Wa Ngano Za Soga

1. Kukashifu matendo hasi kwa njia ya ucheshi
2. Kuonya na kutahadharisha dhidi ya matendo hasi k.v. ulaghai.
3. Kufunza maadili.
4. Kuburudisha kwa kuchekesha.

2. VIGANO

1. Hadithi fupi zinazosimulia kuhusu matendo mabaya katika jamii na wakati uo huo kuonya na kuelekeza dhidi yayo.
2. Aghalabu huandamana na methali kwa lengo la kufafanua linalokusudiwa au kuthibitisha funzo la methali fulani.

Sifa Za Vigano

1. Huwa vifupi.
2. Husimulia kisa kimoja tu.
3. Wahusika ni binadamu na wanyama.
4. Hufunza maadili kutokana na methali.

1. KISA

Masimulizi mafupi yenye tukio moja lenye funzo kwa njia ya kufurahisha.

● MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UCHAMBUZI WA HADITHI/NGANO

1. Kueleza aina ya ngano kwa kuzingatia wahusika na maudhui
- a) Ngano yaweza kuwa ya mazimwi na ya mashujaa kwa wakati mmoja.

- b) Ngano yaweza kuwa hurafa, ya usuli na ya kiayari.
2. Kutaja wahusika
 3. Kufafanua sifa za wahusika wakuu
 4. Maadili/mafunzo yanayojitokeza katika hadithi
 5. Kubainisha sifa za ngano/hurafa/hekaya, n.k. zinazojitokeza katika hadithi.
 6. Kueleza umuhimu wa fomula ya kuanzia/wimbo uliotumiwa katika hadithi.
 7. Kubainisha tamathali za usemi zilizotumiwa katika hadithi fulani
 8. Kuonyesha jinsi ngano inavyoshughulikia maudhui fulani.
 9. Kufafanua ufaafu wa methali fulani zilizotumiwa katika hadithi.
 10. Katika ngano ya mtanziko, ungekuwa mhusika mkuu ungefanya nini?
 11. Kubainisha matumizi ya mbinu ya fantasia
 12. Kufafanua maswala ibuka/maudhui yaliyoshughulikiwa k.m. usaliti, ujinga, ulaghai, n.k.
 13. Kuchanganua utungo kifani-ploti, wahusika, mbinu za lugha, fantasia, nyimbo, n.k.
 14. Kueleza majukumu ya hadithi.

JITATHMINI 2

“Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini. Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka. Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

1. Maswali

a. Tambua utanzu na kijipera chake. (al.2)

b. Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (al.5)

c. Taja na ueleza umuhimu wa fomula:

i. Kutanguliza (al.3)

ii. Kuhitimisha (al.3)

2. Jadili mambo manne ambayo huzingatiwa katika uchambuzi wa hadithi. (alama.4)

3. Fanani anawezaje kuihusisha hadhira katika usimulizi wake? (alama 4)

4. Eleza tofauti kati ya Ngano na Hadithi za kihistoria (alama 6)

UTANZU WA SEMI

MAANA YA SEMI

Tungo fupi zinazowasilisha ujumbe kwa kufumba au kuchora picha.

Sifa Za Semi

1. Huwa fupi kwa kuwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache.
2. Ni tanzu tegemezi kwa kuwa hutegemea tanzu nyingine kama vile hadithi, mazungumzo, n.k.
3. Hazibadiliki vivi hivi.
4. Baadhi ni kielelezo cha maadili k.v. methali.
5. Hutumia lugha ya kimaumbo.
6. Huibua taswira.
7. Huwa na mchezo wa maneno.
8. Baadhi huwa na muundo maalum k.v. methali na vitendawili.
9. Nyingine ikikosa kutumika hutoweka k.v. misimu.

Umuhimu Wa Semi

1. Kuonya k.m. methali, 'Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.'
2. Kukuza uwezo wa kufikiri k.m. vitendawili na chemshabongo.
3. Kutasfidi lugha au kupunguza ukali wa maneno k.m. nahau 'jifungua' badala ya 'zaa'.
4. Kuburudisha k.m. vitendawili, chemshabongo na vitanza ndimi.
5. Kuhifadhi siri k.m. nahau, misemo, misimu.
6. Kuelimisha k.m. kutofanya mambo kwa pupa-mla kwa pupa hadiriki kula tamu.
7. Kuongeza utamu katika lugha.
8. Kuboresha matamshi k.m. vitanza ndimi.
9. Kukuza lugha k.m. misimu.
10. Kukuza utangamano katika jamii kwa kuleta watu pamoja wakati zinawasilishwa.

VIPERA VYA SEMI

AINA ZA SEMI

- *Methali, - vitendawili, - mafumbo*
- *Misemo na nahau, - Lakabu, - misimu*
- *Chemshabongo*
- *Vitanza ndimi na vichezea maneno*

1) METHALI

Semi fupi ambazo hueleza kwa muhtasari au mafumbo ukweli fulani wa kimaisha.

Sifa Za Methali

1. Huwa fupi k.m. 'Msafiri kafiri.'
2. Hutumia tamathali za usemi.
3. Hutumia lugha ya kimaumbo.
4. Huwa na maana ya ndani na nje.
5. Kunazo hufanana kimaana k.m. 'Haraka haraka haina baraka' na 'Polepole ndio mwendo.'
6. Hupingana zenyewe k.m 'Polepole ndio mwendo' na 'Chelewa chelewa utamkuta mwana si wako.'
7. Huwa na sifa za kishairi k.v. ukwapi, utao na vina -**Haba** na **haba**, hujaza kibaba
8. Sifa za utegemezi kwa kuingiliana na tanzu nyingine za fasihi.
9. Huwa na muundo maalum wa sehemu mbili:
 - ✓ *Kutoa wazo; ... 'Haba na haba...'*
 - ✓ *Kukamilisha wazo '...hujaza kibaba.'*

Umuhimu Wa Methali

1. Kukuza uwezo wa kufikiri kwani mpokezi hufikiri ili kupata maana ya ndani.
2. Kuonya dhidi ya matendo yasiyofaa k.m. 'Mchimba kisima huingia mwenyewe' na 'Ukiambiwa jiambe usijeishia kumbe.'
3. Kufariji walio katika hali ngumu, Baada ya dhiki faraja, Hakuna marefu yasiyo na ncha, Liandikwalo ndilo liwalo, Ajaliwalo ndilo apatalo.

4. Kuhimiza watu kujitahidi maishani/kuonyesha jambo jema huja kwa kufanyiwa kazi k.m. 'Mtaka cha mvunguni sharti ainame,' 'Chumia juani ulie kivulini.'
5. Kupamba lugha iwe na mvuto kwani huwa na usanii mkubwa.
6. Kuhimiza ushirikiano, 'Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, 'Jifya moja haliinjiki chungu.'
7. Kuelimisha mtu ajue jambo muhimu k.m. 'Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi,' 'Pema usijapo pema ukipema si pema tena.'
8. Kushauri k.m. 'Enga kabla ya kujenga' na 'Mchama ago hanyeli.'
9. Kufupisha maadili katika ngano.
10. Kubuni lakabu k.m. 'kikulacho.'
11. Kufunza maadili k.m. kuwa na Subira - 'Subira huvuta heri.'
12. Kuhimiza kutokata tamaa k.m. 'Bandu bandu huisha gogo, Papo kwa papo kamba hukata jiwe.'
13. Kuonyesha umuhimu wa kuthamini jamaa zako kuliko marafiki k.m. 'Damu ni nzito kuliko maji, 'Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.'
14. Kuonyesha umuhimu wa kuthamini vitu vyako - 'Usiache mbachao kwa msala upitao' 'Afadhali dooteni kama ambari kutanda,'
15. Kukashifu ubinafsi k.m. 'Mwamba ngoma huvutia kwake' 'Kila mchukuzi husifu mzigo wake.'
16. Kukashifu kiburi k.m. 'Maskini akipata matako hulia mbwata' 'Zingwi zingwi lipe nguo utaona mashauo.'

MBINU ZA LUGHA/FANI /TAMATHALI ZA USEMI KATIKA FASIHI

- Maneno au vifungu vya maneno vinavyotumiwa kutia fasihi urembo ili kufanya ujumbe ueleweke vyema zaidi.

AINA ZA MBINU ZA LUGHA

1. Tashbihi

Ulinganishi kwa kutumia viunganishi kama, mithili, mfano na sawa.

2. Stiari/ Istiara

Ulinganishi usio wa moja kwa moja.

3. Tashihisi/Uhaishaji

Kukipa kitu sifa ya uhai.

4. Taashira/ Ishara

Kitu kuwakilisha kingine.

5. Chuku/udamisi

Kutia chumvi au kufanya kitu kionekane kikubwa sana au kidogo sana.

6. Takriri

Urudiaji wa neno au mafungu ya maneno.

7. Tanakuzi

Maneno yaliyo kinyume/ yanayokinzana

8. Tabaini

Msisitizo kwa njia ya kinyume kwa kutumia kikanushio si.

9. Ritifaa

Kusemesha asiye kuwapo kama yupo.

10. Taharuki

Kuacha msomaji akiwa na hamu ya kutaka kujua kipi kitakachojiri halafu.

11. Majazi

Majina yanayooana na sifa za wahusika, vitu au mahali.

12. Mbinu rejeshi

Kukumbusha mambo yaliyopita.

13. Methali

Semi fupi ambazo hueleza kwa muhtasari au mafumbo ukweli fulani wa kimaisha.

14. Nahau

Fungu la maneno lenye maana tofauti na maana ya kawaida ya maneno hayo.

15. Misemo

Semi zinazobeba ukweli wa kijumla

16. Mdokezo

Mambo kuachwa bila kumalizwa.

17. Balagha

Maswali yasiyohitaji majibu.

18. Taswira

Ujenzi wa picha akilini.

19. Kinaya

Mhusika kutumia maneno au matendo yaliyo kinyume cha inavyotarajiwa.

20. Koja

Kuorodhesha maneno na vitenzi kwa kutumia koma.

21. Kejeli

Kudharau au kubeza.

22. Jazanda

Kufananisha vitu kwa mafumbo k.m. katika biblia.

23. Nidaa/ Siyahi

Maneno ya kuonyesha hisia za moyoni.

24. Tanakali/onomatopeya

Miigo ya sauti zinazotokea baada ya kitendo.

25. Uzungumzi nafsia

Kujisemesha mwenyewe.

26. Dayalojia

27. Utohozi/Uswahilishaji

28. Kuchanganya ndimi

Kutumia lugha zaidi ya moja katika mazungumzo.

29. Tasfida/usafidi

Kutumia lugha ya adabu au kupunguza ukali wa maneno.

30. Mkengeuko

Kwenda kinyume na matakwa ya jamii k.v. usenge, ndoa ya watu wasio wa rika moja, mapenzi nje ya ndoa.

31. ulinganuzi

Kuweka pamoja mambo yanayopingana ili kulinganisha

32. Kweli kinzani

Hoja mbili zinazopingana/kutowezekana.

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA METHALI

Sitiari

1. Mgeni ni kuku mweupe.
2. Ahadi ni deni.
3. Upweke ni uvundo
4. Ujana ni moshi.
5. Mapenzi ni kikohozi.
6. Kukopa arusi kulipa matanga.

Tashbihi

1. Kawaida ni kama sheria.

2. Riziki kama ajali ijapo huitambui.
3. Usilolijua ni kama usiku wa giza.
4. Ufalme kama mvua hupiga na kupita.

Tashihisi

1. Siri ya mtungi muulize kata.
2. Paka akiondoka panya hutawala.
3. Jembe halimtupi mkulima.
4. Ukupigao ndio ukufunzao.
5. Adhabu ya kaburi aijuaye maiti.

Takriri

1. Haba na haba hujaza kibaba.
2. Chovya chovya humaliza buyu la asali.
3. Hauchi hauchi unakucha.
4. Hayawi hayawi huwa.
5. Mtoto wa nyoka ni nyoka.
6. Bandu bandu huisha gogo.

Balagha

1. Pilipili usiyoilala yakuwashiani?
2. Angurumapo simba mcheza ni nani?
3. Wameshindwa wenye pembe seuze wewe kipara?
4. Simba mla watu akiliwa huwani?
5. Mzigo uko kichwani, kwapa lakutokeani jasho?
6. Mavi usiyoyala wayawingiani kuku?
7. Mla ni mla leo mla jana kalani?

Taswira

1. Mpanda farasi wawili hupasuka msamba.
2. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.
3. Mtupa jongoo hutupa na ung'ong'o wake.

4. Angeenda juu kipungu hafikii mbingu.

Chuku

1. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.
2. Maji ya kifuu bahari ya chungu.
3. Usipoziba ufa utajenga ukuta.

Tanakali za sauti

1. Chururu si ndondondo!
2. Ndo! Ndo! Hujaza ndoo.
3. Kiliacho pa kijutie.

Kinaya

1. Bara Hindi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wapo.
2. Kwenye miti hakuna wajenzi.
3. Asante ya punda ni mateke.
4. Kigumba kwa nguruwe kwa binadamu ki uchungu.
5. Kikiharibika cha fundi kikiongoka cha bwana Sudi.

Kejeli/dhihaka/stihizai

1. Umekuwa mumunye waharibikia ukubwani.
2. Hawi Musa kwa kubeba fimbo.
3. Ucha Mungu si kilemba cheupe.
4. Kichwa cha kuku hakistahimili kilemba.
5. Kichwa cha nyoka hakibandikwi mtungi.

Jazanda

- 1) Joka la mdimu hulinda watundao.
Mtu mwovu huwanyima wengine vitu asivyovihitaji.
- 2). Kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma.
Ni rahisi kujitia katika matata kuliko kujitoa.

Taashira

1. Kimya kingi kina mshindo mkubwa.

2. Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.

Kweli kinzani

1. Wagombanao ndio wapatanao.
2. Ukupigao ndio ukufunzao.
3. Kuinamako ndiko kuinukako.
4. Mwenye kelele hana neno.
5. Kimya kingi kina mshindo mkubwa.

Tanakuzi

1. Tamaa mbele mauti nyuma.
2. Mpanda ngazi hushuka.
3. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.

*Kuainisha methali kutokana na matumizi ya lugha ni kusema mbinu ambazo imetumia.

VIGezo VYA KUAINISHIA METHALI/ KUZIWEKA PAMOJA NA KUZICHAMBUA

Methali zinaweza kuainishwa kwa njia mbalimbali kutegemea, majukumu, mtindo, maana, mazingira, maudhui, n.k.

1) Mandhari/mazingira

- **mf 1**, mazingira ya kilimo

Ukipanda pantosha utavuna pankwisha.

Jembe halimtupi mkulima.

- **mf 2**, mazingira ya pwani

mgaa na upwa hali wali mkavu

Msafiri ni aliye pwani

2) Maudhui

- **mf1**, maudhui ya ulezi

Samaki mkunje angali mbichi.

Mcha mwana kulia hulia yeye.

- **mf 2**, maudhui ya ushirikiano.

Jifya moja haliinjiki chungu

Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu

3) Fani/tamathali

- **mf 1**, Fani ya takriri

Haba na haba hujaza kibaba.

Mtoto wa nyoka ni nyoka.

- **mf 2**, Fani ya tashibihi.

Kawaida ni kama Sheria.

Riziki ni kama ajali, ijapo huitambui

4) Jukumu

- **mf1**, Jukumu la kuonya

Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Ukiambiwa jiambie usijeishia kumbe.

- **mf 2**, Jukumu la kutenda mema.

Wema hauozi

Tenda wema nenda nenda zako

5) Maana

- **mf**, methali zenye maana sawa huwekea pamoja

Polepole ndio mwendo

Haraka haraka haina baraka.

VICEZO ZAIDI VYA KUCHAMBUA METHALI

4) Inarejelea vitu gani? K.m. Hindi ndiko kwenye nguo na waendao uchi wapo.....

Nchi - Hindi, Vitu - nguo, Watu - waendao uchi

Inakupa wazo gani kuhusu jamii husika? Utamaduni na njia za kiuchumi?

2). VITENDAWILI

Semi ambazo hutolewa kwa mtu kwa mfano wa swali ili azifumbue.

Sifa Za Vitendawili

1. Huwa vifupi kimaielezo.
2. Hutumia lugha ya kimaifumbo.
3. Hutolewa mbele ya hadhira.
4. Hutumia ufananisho wa kijazanda.

5. Kunazo huhusiana na methali k.m. Mzee amekufa vyombo vimevunjika-vunjika.
6. Huwa na wakati maalum wa kutolewa, yaani, jioni.
7. Huwa na mchezo wa maneno k.m. Ukiona njigi utadhani njege-Maziwa na tui.
8. Hujisimamia vyenyewe.
9. Kunavyo huwa na jibu zaidi ya moja k.v. Gari la kila mtu miguu, kifo au jeneza.
10. Hutumia tamathali za lugha kwa ufanifu mkubwa.
11. Huweza kuwa na fomula/muundo maalum.

- Mtegaji: Kitendawili

- Mteguaji: Tega

Mtegaji: (*Kitendawili chenyewe*) Popoo mbili zavuka mto

Mteguaji: (*jibu*) Mlango

- Mtegaji: Umenoa. Nipe mji.

Mteguaji: Ninakupa Nairobi.

Mteguaji: Nilienda Nairobi. Watu wa Nairobi wakaniambia nije niwasalimu. **Jibu ni 'macho'.**

Umuhimu Wa Vitendawili

1. Kuburudisha jioni baada ya kazi.
2. Kukuza ubunifu wa kuvitunga kwa kulinganisha vitu katika mazingira ili kuviunda.
3. Kuimarisha uwezo wa kukumbuka.
4. Kukuza uwezo wa kufikiri kwani mfumbiwa huhitaji kufikiri sana ili kupata jibu.
5. Kuleta umoja na ushirikiano katika jamii kwa kuleta watu pamoja wakati vinategwa.
6. Kuimarisha ujuzi wa kujieleza kwa lugha.
7. Kupanua ujuzi wa mazingira ya mtoto.
8. Kuendeleza utamaduni wa jamii k.m. Nyumbani mwetu mna papai lililoiva lakini. siwezi kulichuma. - Ndugu wa kiume asimuo nduguye wa kike.
9. Kukejeli au kudharau tabia mbaya k.m. Wazungu wawili wanachungulia dirishani - Makamasi

AINA ZA VITENDAWILI

1. Vitendawili Sahili

Vina muundo rahisi/maneno machache k.m
Akiona mwangaza wa jua hufa - **samaki**.

2. Vitendawili sambamba

Huwa na maelezo marefu (kama hadithi fupi) halafu jibu lake huwa ni refu pia (kama mafumbo) Kisimulizi, Masimulizi k.m. Kulikuwa na baba ng'ambo moja ya mto na bin zake wawili ng'ambo ya pili. Alikuwa na maembe mawili aliyopaswa kuyavukisha pamoja apelekee bin zake. Angefanya nini?

3. Vya tanakali

k.m. Parrrr! Mpaka Makka - utelezi.

4. Vitendawili mkufu

Huwa na vipande vinavyofuatana na kila kipande huwa na uhusiano na kipande kilichotangulia. Mfano - nikisimama anasimama, nikiketi anaketi, nikiondoka huondoka pia -kivuli.

5. Vitendawili Tata,

Vyenye majibu tofauti

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA VITENDAWILI

Tashihisi

1. Amefunika kote kwa blanketi lake jeusi - giza.
2. Akivaa nguo hapendezi, akiwa uchi hupendeza mno - ndizi.
3. Anakula lakini hashibi - kifo/mauti.
4. Amchukuapo hamrudishi - kaburi.
5. Akizungumza kila mtu hubabaika - radi.
6. Daima nasababisha mafarakano - uke wenza.

o Tashbihi

1. Boi wangu kazama kaibuka kama mzungu - mwiko wa ugali.

Stiari/Stiari

1. Bibi hatui mzigo - konokono.
2. Mamangu hachoki kunibeba - kitanda.

3. Fatuma mchafu - ufagio.
4. Saa yetu kadiri inavyotembea ndivyo inavyopunguza nguvu - moyo.
5. Mzungu kujishika kiuno - kikombe.
6. Nina mapapai yangu mawili ambayo siwezi kuyala - matiti ya mwanamke.
7. Ng`ombe wangu nisipomshika mkia hali nyasi - jembe.
8. Kitu changu kitumiwacho na wengine kuliko mimi - jina.
9. Popoo mbili zavuka mto - macho.
10. Gari la kila mtu - miguu.
11. Dada ni mrembo lakini akiguswa analia - papai.

Takriri

1. Huku ng`o na kule ng`o - giza.
2. Amezaliwa Ali, amekufa Ali, amerudi Ali - nywele.
3. Huku fungu katika Bahari - nazi

Tanakali

1. Parrr! Mpaka Makka - utelezi.
2. Huku pi kule pi - mkia wa kondoo atembeapo.
3. Ba funika ba funua (Bak bandika, bak bandua) - nyayo.
4. Tang! Yaanguka - sarafu.

Kweli kinzani

1. Ana meno lakini hayaumi - kitana.
2. Ajenga ingawa hana mikono - ndege.
3. Hukopa lakini halipi - kifo.
4. Nina shamba langu kubwa lakini nikivuna halijai hata kofi - nywele.
5. Hufa akifufuka - bahari kupwa.
6. Nameza lakini sishibi - mate.

Taswira

1. Adui tumemzingira lakini hatumwezi - moto.
2. Nyama nje, ngozi ndani, mchanga ndani - firimgisi ya kuku.
3. Wanatazamana tu lakini hawaamkiani - ardhi na bingu.
4. Askari wangu wote wamevaa kofia upande - mahindi shambani.
5. Samaki wangu aelea kimgongomgongo - merikebu.

6. Babu amebeba machicha meupe kichwani - mvi.

Stahizai/dhihaka/kejeli

1. Akivaa miwani hafanyi kazi vizuri - mlevi.
2. Mzungu anachungulia dirishani - makamasi.
3. Uzi mwembamba umefunga dume - usingizi.
4. Mtani wangu hata akiishi majini hatakasiki - chura.
5. Kisiki chetu hakikui - mbilikimo.
6. Nimemuona bi kizee amejitwika machicha - mvi.

Jazanda

1. Mungu alinipa shilingi mbili, moja nitumie nyingine niweke - ardhi na mbingu.
*Kuchambua kitendawili ni kueleza mbinu za lugha zilizoiunda.

● KULINGANISHA VITENDAWILI NA METHALI

Kufanana kwa Methali na Vitendawili

Zote mbili ni tungo fupi.

Zote mbili huwa na maana fiche.

Zote mbili hutumia lugha inayojenga taswira.

Zote mbili hupata maana kulingana na jamii.

Zote mbili Huwa na muundo maalum.

Zote mbili hufumbata ukweli fulani wa kijamii.

Tofauti kati ya vitendawili na methali

Vitendawili	Methali
1. Vina fomyula maalum ya uwasilishaji. 2. Fumbo lazima lifumbuliwe papo hapo. 3. Ni maarufu zaidi miongoni mwa watoto/vijana. 4. Hutolewa katika vikao maalum. 5. Hutumia lugha ya majibizano/pande mbili.	1. Hazina fomyula ya kuanza. 2. Fumbo halifumbuliwi papo hapo. 3. Hutumiwa sana na wazazi na wazee. 4. Si lazima zitolewe katika vikao maalum. 5. Ni kauli ya msemaji mmoja

2. CHEMSHABONGO

Maswali ambayo huhitaji mtu kutumia akili na ujuzi kuyajibu.

- Mafumbo ni kauli zenye maana iliyofichika na hujumuisha vitendawili na chemshabongo.

Mifano ya chemshabongo

1. Kilo moja ya chuma na kilo moja ya nyama ipi nzito?
2. Amada ana wafanyikazi saba, wanne hufanya kazi vizuri, wawili ni kama wamekufa, mmoja ni kama mwenda wazimu- miguu, pembe na mkia wa ng'ombe.
3. Kipungu alipita juu, mama na ndege wawili wakamwangalia. Je macho mangapi yalimuona kipungu? - manne.
4. Nina watu wangu watatu, wawili ni watoto na wawili ni baba- mtoto, baba na babu.
5. Chura alitumbukia katika shimo la futi 30 na anaruka futi 10. Aruke mara ngapi ili atoke? -Hawezi.
6. Watu watatu wanavuka mto. Mmoja aliyaona maji na kuyakanyaga. Wa pili aliyaona lakini hakuyakanyaga. Wa tatu hakuyaona wala kuyakanyaga. Watu hao ni kina nani?

Sifa Za Chemshabongo

1. Ni kauli fupi au ndefu.
2. Hutumia lugha ya kimaumbo.
3. Hutumia ufananisho wa kijazanda.
4. Huhitaji mtu kuwaza ili kupata jibu.
5. Hujengwa na vitu vinavyotokana na mazingira.
6. Hazina muundo maalum kama methali, nahau na vitendawili
7. Hupima uwezo wa msikilizaji wa kutambua jambo lililofichwa.

Umuhimu Wa Chemshabongo

1. Kuimarisha stadi ya kusikiliza.
2. Kunoa uwezo wa kufahamu.

3. Kutoa mawaidha.
4. Kufunza kuhusu maumbile.
5. Kuimarisha uwezo wa kukumbuka.
6. Kufunza mambo kuhusu mazingira na maumbile.
7. Kukuza uwezo wa kutumia lugha.
8. Kukuza uwezo wa kufikiri.
9. Kuburudisha na kuchekesha.
10. Kukuza uwezo wa kubuni.

3. VITANZA NDIMI

Sentensi zenye mfuatano wa sauti zinazotatanisha kimatamshi zinapotamkwa kwa haraka.

Mifano

1. Wataita wataita Wataita wa Taita.
2. Waite wale wana wa liwali wale wali wa liwali.
3. Kupa mpe akupao kumpa asokupa si kupa ni kutupa.
4. Shirika la Reli la Rwanda limefungwa.
5. Hilo lililoliwa ndilo nililolitaka.
6. Mchuuzi wa mchuzi hana ujuzi wa mjusi wa juzi.
7. Cha mkufuu mwanafuu ha akila hu cha mwanafuu mkufuu hu akila ha
8. Pema usijapo pema ukipema si pema tena
9. Nguo zisizotakikana zitachomwa zote.

Sifa Za Vitanza Ndimi

1. Ni kauli fupi.
2. Huwa na mchezo wa maneno.
3. Huundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi.
4. Hutumia maneno yenye maana zaidi ya moja au yenye sauti sawa.
5. Hutanza/hutatiza ndimi za wengi wakalemewa kutamka.
6. Hukanganya kimatamshi.

Umuhimu Wa Vitanza Ndimi

1. Kukuza matamshi bora mtu anapoendelea kutamka.

2. Kukuza uwezo wa kufikiri haraka ili kujua maana za maneno ili kutamka ipasavyo.
3. Kupanua ujuzi wa msamiati.
4. Kuburudisha kwa kufurahisha na kuchangamsha.
5. Husaidia kutofautisha maana za maneno.
6. Kujenga stadi ya kusikiliza.
7. Kukuza ubunifu kwa kuteua maneno yanayotatanisha kisauti na kimaana.
8. Kujenga uhusiano bora kwa ucheshi.

4. LAKABU

Jina la msimbo/kupanga/ambalo mtu hupewa au hujipa kutokana na sifa zake.

Asili Ya Lakabu

1. Tabia za kitu/mtu
2. Sifa za kimaumbile za kitu/mtu
3. Matendo ya mtu
4. Nasaba atokayo mtu.
5. Tabaka la mtu
6. Jinsi mtu anavyotamka maneno k.m. ung'eng'e.

Mifano

1. Nyayo - Moi
2. Simba wa Yuda -Haille Selassie
3. Mkuki uwakao - Kenyatta
4. Nyundo/Tingatinga -Raila
5. Baba wa taifa - Rais
6. Mama wa Taifa - mke wa Rais

Sifa Za Lakabu

1. Huwa neno au fungu la maneno kadha.
2. Huwa na maana iliyofumbwa.
3. Huoana na sifa hasi au chanya za aliyepewa.
4. Huwa za kusifu au kudhihaki.
5. Huweza kudumu hata kusahaulisha jina halisi la mtu.
6. Hutumia sitiari k.m. chui kumaanisha mkali.

7. Hutumia taswira.
8. Hushika sana kimatumizi miongoni mwa watu.

Umuhimu Wa Lakabu

1. Kufahamisha sifa za mtu kwa kifupi.
2. Huwa njia ya washairi ya kujitangaza bila kujisifu moja kwa moja.
3. Hutumiwa kama ishara ya heshima kwa anayestahili heshima k.m. kiongozi.
4. Kuficha utambulisho au jina halisi la mtu.
5. Hutumiwa katika majigambo na mhusika kuonyesha ubingwa wake.
6. Kuficha siri ili anayerejelewa asijulikane k.m. kikulacho.
7. Kukuza uhusiano bora miongoni mwa watani wanaporejeleana kwa lakabu.
8. Kusifu tabia njema kwa kumpa mtu lakabu nzuri.
9. Kudhihaki au kukashifu tabia mbaya kwa kumpa mtu lakabu mbaya
10. Kutambulisha asili ya mtu.

5. MISEMO

Semi zinazobeba ukweli wa kijumla.

Mifano

1. Binadamu ni udongo.
 2. Mwili haujengwi kwa mbao.
 3. Umaskini si kilema.
 4. Lila na fila havitangamani.
 5. Ndio kwanza mkoko ualike maua.
 6. Mambo kuzidi kushika kasi.
 7. Mgomba haupandwi changaraweni ukamea.
- Jambo halifanywi mahali pasipofaa likapendeza.

Sifa Za Misemo

1. Hutumia lugha ya muhtasari.
2. Hutoa ukweli kwa jumla.
3. Haina muundo maalum.

Umuhimu Wa Misemo

1. Kuisitiza ujumbe.

2. Kuongeza utamu katika lugha.
3. Kusisitiza jambo fulani.
4. Kufunza maadili au kuhimiza.
5. Kuchochea hisi fulani.

6. NAHAU

Fungu la maneno lenye maana tofauti na maana ya kawaida ya maneno hayo.

Mifano

1. Kuasi ukapera - kuo
2. Kupiga vijembe - sema kwa mafumbo
3. Ndege mbaya - bahati mbaya
4. Kidudu mtu - mfitini
5. Paka mafuta kwa mgongo wa chupa - danganya au hadaa mtu
6. Visha kilemba cha ukoka - mpa mtu sifa za uongo ili umpumbaze
7. Kuyavulia maji nguo - kufanya jambo ulilokusudia
8. Siku ya ndovu kumla mwanawe - Siku Kubwa

Sifa Za Nahau

1. Hutumia lugha ya kimkato.
2. Maneno huwa na maana tofauti na ya kawaida.
3. Kunazo huwa na maana zaidi ya moja k.v. kuja jamvi-kumaliza shughuli au kuondoka.
4. Huundwa kwa neno moja, mawili au zaidi.
5. Huibua taswira.
6. Zina muundo maalum/huundwa kwa aina mbalimbali za maneno.

Miundo Ya Nahau

1. Kitenzi na kitenzi (T+T)
 - kufa kupona
 - kufumba na kufumbua
2. Kitenzi na Nomino (T+N)
 - kupiga domo
 - kata kamba

3. Kitenzi na Kielezi (T+E)
 - Kujikaza kisabuni
 - kufa kiofisa
4. Nomino na Nomino (N+N)
 - donda dugu
 - domo kaya
5. Nomino na Vivumishi (N+V)
 - nyota njema
 - ndege mbaya
6. Nomino wa Kitenzi (N+T)
 - damu kumkauka
 - akili kumruka

Umuhimu Wa Nahau

1. Kukuza na kuendeleza msamiati wa maneno.
2. Kupunguza ukali wa maneno (tasfida).
3. Kuongeza utamu/ladha katika lugha.
4. Kuhifadhi siri kwani sio wote wanajua maana.
5. Kujaribu uwezo wa msikilizaji kufichua maana iliyofichika.

7. MISIMU/SIMO

Semi ambazo huzuka katika mazingira na kipindi fulani.

Aina Za Misimu

1. Inayotumika na kutoweka
2. Inayokita kimatumizi kuingizwa katika Kiswahili sanifu k.m. toa chai, chokora, n.k.

Asili Ya Misimu

1. Ufupishaji maneno
 - Daro - darasa
 - Dere - dereva
2. Utohozi
 - Fathee

3. Stiari/jazanda
 - Nyani - mlinda lango
 - fisi - mlafi
4. Tanakali
 - Mtutu - bunduki

JINSI YA KUUNDA MISIMU

1	Uundaji maneno mapya
	Hanya
2	Kupa maneno maana mpya
	chuma-gari
	toboa- faulu
3	Kugeuza maneno
	risto-stori
4	Kuboronga lugha
	ashu-ashara/kumi
	Jisikia sukari
	Kuringa
5	Mifano zaidi
a	Kaa ngumu - kuvumilia, kuto kufa moyo
b	Chongoa mtu - fanyia mtu mzaha
c	Kula njaro - kupuuza kazi
d	Piga nduthe - kimbiba/ toroka
e	Piga ngeta - kukaba koo
f	Leta diambo - zozana
g	Ingia baridi - kuogopa
h	Pewa msomo - kugombezwa

i	Kusota - kuishiwa na pesa
j	Ingia mitini - toweka, potea
k	Kung`ara - kuvaa vizuri
l	Kukuradi - kuvaa vizuri

Misimu Zaidi

- 1) Marehemu George - nguo za mitumba
- 2) Vaa chupa - vaa suruali nyembamba
- 3) Kujisikia poa - kuwa na furaha
- 4) Kula hepi - kuburudika
- 5) Lala kibahasha - tulia tuli baada ya kushindwa katika jambo

Sifa Misimu/Simo

1. Ni kauli fupi.
2. Hutumiwa na kundi dogo la watu.
3. Huzuka katika mazingira na kipindi maalum.
4. Ni lugha ya kimaumbo.
5. Hutumiwa na kundi dogo la watu katika jamii.
6. Huzuka na kutoweka baada ya muda.
7. Kunazo hudumu na kukubaliwa kama lugha sanifu k.v. matatu, bodaboda, chai, chokora, daladala, n.k.
8. Huwa na maana nyingi k.m. 'mahewa'humanisha muziki, uongo au ulevi wa dawa za kulevya.
9. Maneno yana maana tofauti na ya kawaida.
10. Si lugha sanifu na hivyo haipaswi kutumiwa katika mazungumzo rasmi.
11. Hupendeza miongoni mwa watumizi.
12. Hutoweka baada ya matumizi kwa muda.
13. Hubadilika k.m. mbuyu na buda humanisha baba.

Umuhimu Wa Misimu/Simo

1. Kuficha siri ya wanaoitumia.
2. Kupanua lugha kimsamiati ikikubalika.
3. Kurahisisha mawasiliano kwa kuondoa uchovu wa urasmi.
4. Kuonyesha ubingwa wa lugha kwa kuhisi huonyesha umaarufu wa lugha.
5. Kutenga wasio wana kikundi fulani.

6. Kutasfidi/kupunguza ukali wa maneno k.m. Amepata bol-mimba.
7. Kupamba lugha na kuifanya ivutie
8. Kufanya wanakikundi wajihisi kuwa pamoja.
9. Kujitambulisha na watu wa kikundi fulani.

8. SHIRIKINA

Semi ambazo huonyesha imani fulani ya kundi la watu.

Mifano

1. Ukijikuna kiganja cha mikono utapata pesa.
2. Ukila chakula gizani utakula na shetani.
3. Kuzaliwa ukiwa na vidole sita ni kuwa na bahati.
4. Bundi akilia karibu na nyumba mtu mmoja wa nyumba ile atafariki.

Umuhimu Wa Shirikina

1. Kukataza maovu.
2. Kuhifadhi utamaduni.
3. Kuchangia umoja wa kitaifa kwa aina moja ya itikadi kupatikana katika jamii nyingi.
4. Kutujulisha kuhusu itikadi za watu.

9. TANAKALI ZA SAUTI (ONOMATOPEIA)

Maneno ambayo huiga sauti ya jambo, tendo au tukio fulani.

Mifano

1. Boboka bobobo! - payuka ovyoovy
2. Bwakia bwaku - akia upesi upesi
3. Bwaka bwata - enda chini kwa mshindo
4. Bweka bwebwebwe! - lia kama mbwa
5. Chaga ngungundu - shikilia jambo
6. Ng'o! - kutoambulia chochote
7. Legalega lege - kosa kuwa imara
8. Chakua nyakunyaku - tafuna kwa kutoa sauti ya kuudhi
9. Bingirika bingiribingiri! - pinduka
10. Birua biru! -
11. Shindilia ndi!

Mianguko

12. Pu/kacha - tawi
13. Pu, pu, pu - mfululizo
14. Pukupuku! - mvua
15. Pwa! - kwa matope
16. Pwata! - kitu kinene
17. Anguka Tang'! - sarafu pagumu
18. Anguka Tapwi - matopeni
19. Tifu! - anguka mchangani
20. Tubwi/ chubwi - anguka majini

Sifa Za Tanakali Za Sauti

1. Ni kauli fupi.
2. Ni miigo ya sauti zinazotokea baada ya tendo fulani.
3. Hazina muundo maalum.
4. Hujumuishwa katika fani nyingine.
5. Hutumia takriri.

Umuhimu Wa Tanakali Za Sauti

1. Kuwezesha kuunda taswira ya jinsi mambo yanavyotokea.
2. Kuonyesha hisia fulani.
3. Kuongeza uzito kwa maneno.
4. Kuongeza utamu katika mazungumzo.
5. Kuisitiza jambo.
6. Kuipa lugha ladha na mvuto.
7. Kujenga tabia ya kusikiliza kwa makini ili kutambua mlilo.
8. Kukuza ustadi wa kuiga na kuigiza.
9. Ni mbinu mojawapo ya mawasiliano.

● TAKRIRI ZA MAANA

Mafungu ya maneno yanayosisitiza na kueleza maana zaidi ya kitendo.

Mifano

- Haambiliki hasemzeki
- Siku nenda siku rudi
- Tilia huku ukitolea kule
- Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini

Umuhimu Wa Takriri

1. Kutia ladha katika lugha na kuifanya iwe na mnato.
2. Kusisitiza jambo.
3. Kuonyesha ukwasi wa lugha ya mnenaji.

oTASHBIHI

Misemo ya ulinganisho

Sifa Za Tashbihi

2. Ni fupi.
3. Hutumia viungio kama, mithili ya, n.k.
4. Huwa na ujumbe wa kina.
5. Hutoa taswira ambayo husaidia kueleza hulka kikamilifu.

Umuhimu Wa Tashbihi

1. Kueleza sifa za kinachozungumziwa.
2. Kuongeza lugha utamu.
3. Kuonyesha umilisi wa lugha wa mtumizi.

JITATHMINI 3

1. Fafanua vigezo sita vinavyotumiwa kuainisha methali. (alama.6)
2. Kwa kutolea mifano, eleza aina tatu za vitendawili (alama 3)
3. Eleza utaratibu unaofuatwa wakati wa kutega na kutegua vitendawili. (al6)
4. Kwa kutolea mfano mwafaka, onyesha jinsi vipera vya semi huingiliana (al 10)
5. Linganisha na ulinganue methali na vitendawili (alama 10)

4. UTANZU WA USHAIRI

SIMULIZI

Maana ya ushairi simulizi: Ni Utanzu wa fasihi simulizi unaotumia lugha ya mkato inayoeleza maudhui yake kwa ufupi.

SIFA ZA USHAIRI SIMULIZI

1. Hutumia lugha ya kimkato.
2. Huwasilishwa mbele ya hadhira.
3. Huwasilishwa na mtu mmoja au kundi la watu.
4. Huwa na muundo maalum k.v. beti, vipande na vina.
5. Hutegemea sauti iliyo kipengele muhimu.
6. Huandamana na ishara za mikono, uso n.k.
7. Una mpangilio maalum wa maneno.

8. Una uteuzi maalum wa maneno.
9. Uwasilishaji wake huandamana na vitendo/uigizaji.
10. Hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa mdomo.
11. Huandamana na shughuli maalum k.v. matanga, kazi n.k.
12. Huwa na mapigo ya kimuziki au huweza kuimbika.
13. Huweza kuambatana na ala za muziki.
14. Hadhira hushiriki katika uwasilishaji wa ushairi simulizi.

MAJUKUMU YA USHAIRI SIMULIZI

1. Kuburudisha watu katika sherehe au shughuli fulani ya kijamii.
2. Kutakasa hisia au kutoa hisia zinazomsumbua mtu.
3. Kufunza maadili au tabia zinazokubalika na jamii.
4. Kufariji watu kutokana na maafa, kifo au kushindwa.
5. Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga waliotendea jamii mambo makuu k.v. mashujaa.
6. Kuhifadhi historia ya jamii k.m. maghani simulizi na tenzi.
7. Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa jamii.
8. Kuelimisha kuhusu suala fulani.
9. Kukashifu/kukejeli sifa mbaya za wabaya.
10. Kukuza umoja na ushirikiano katika jamii kwa kujumuisha watu pamoja.
11. Kusifu na kutukuza mashujaa katika jamii (tenzi).
12. Kukanya/kutahadharisha dhidi ya matendo maovu.
13. Kukuza urembo au usanii wa lugha kwa kuwa una ufundi mkubwa wa matumizi ya lugha.
14. Kuhamasisha jamii k.v. kisiasa.
15. Kukuza ubunifu kwa mtunzi na mwasilishaji
16. Kukuza ubunifu kwa kutunga kwa kuzingatia beti, mizani, vina na uteuzi maalum wa maneno.

• AINA KUU ZA USHAIRI SIMULIZI

Kunazo Aina Tano Kuu Za Ushairi Simulizi.

Vipera vya Ushairi Simulizi

- 1) **Wimbo** – Utungo wenye mapigo ya kupanda na kushuka
- 2) **Maghani** - ni ushairi unazotolewa kwa kughanwa
- 3) **Ngojera** - hutolewa kwa majibizano
- 4) **Rara** - (husimuliwa kwa mapigo ya kishairi)
- 5) **Mashairi mepesi** - (utungo unaokaririwa)

● UAINISHAJI WA USHAIRI SIMULIZI

Ushairi simulizi unaweza kuainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile.

1). MAUDHUI

- a) **Mapenzi** - hupitisha jumbe za mapenzi.
- b) **Kutuliza** - kuna nyimbo za bembea au bembelezi zinazowatuliza watoto.
- c) **Kuomboleza** - mbolezi huimbwa wakati wa msiba.
- d) **Kusifu** - sifo huimbwa kusifu mashujaa au waliofaidi umma na kustahili kutambuliwa.
- e) **Siasa** - nyimbo za siasa huwasilisha jumbe za kisiasa.

2). MUKTADHA AU MAHALI PA UWASILISHAJI

- 1) **Nyiso** - nyimbo za jandoni.
- 2) **Mbolezi** - zinazoimbwa kwenye mazishi au kwenye maombolezi.
- 3) **Nyimbo za harusi**.
- 4) **Nyimbo za matambikoni** ambazo hutolewa wakati wa kutoa kafara au sadaka kwa mizimu, labda baada ya janga.
- 5) **Hodiya** - Nyimbo za kazi.

3). MTINDO WA UWASILISHAJI

- 1) **Maghani** - hutolewa kwa kalima bila kuimbwa. Nyimbo huwasilishwa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka.
- 2) **Shairi** - utungo unaokaririwa.
- 3) **Tendi au Rara** - husimuliwa kwa mapigo ya kishairi.
- 4) **Ngonjera** - huwasilishwa kwa kujibizana na mwasilishaji.
- 5) **Majigambo** - huwasilishwa na anayejigamba.
- 6) **Kwaya** - uimbaji wa watu wengi.

1. WIMBO

Maana - Utungo wenye mahadhi ya kupanda na kushuka

SIFA ZA NYIMBO

1. Huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
2. Hutolewa kwa mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti.
3. Hutumia lugha ya mkato.
4. Hadhira yaweza kuwepo au isiwepo.
5. Huwa na mwimbaji au waimbaji wanaoimba.
6. Waimbaji wanaweza kujivika maleba.
7. Huweza kuambatana na ala k.v. ngoma, zeze, kayamba n.k.
8. Huwa na urudiaji wa mstari au kifungu.
9. Aghalabu huimbwa na kupokezanwa baina ya kiongozi na waimbaji
10. Huimbwa tu au huambatana na kucheza.
11. Huweza kuandamana na shughuli fulani k.v. arusi, kazi, matanga, n.k.
12. Huwa na muundo maalum wa beti, mistari, vina, n.k.

MUUNDO WA NYIMBO

Ifahamike kwamba miundo ya nyimbo ipo mingi ikitegemea matakwa ya msanii au waandaaji wa wimbo husika. Muundo wa kawaida ni huu.

Mifano

- Utangulizi/ mwanzo
- Kibwagizo
- Beti
- Kibwagizo
- Beti
- Kibwagizo
- Hitimisho

MAJUKUMU YA WIMBO

1. Kuburudisha k.m. tumbuizo.
2. Nyenzo ya kiuchumi kwa baadhi ya watu.
3. Kuliwaza k.m. mbolezi.
4. Kuhimiza watu wakiwa kazini k.m. hodiya.
5. Kuelimisha kuhusu suala fulani k.m. ukimwi, ufisadi, n.k.

6. Kuhimiza uzalendo k.m. za siasa na taifa.
7. Kumbembeleza mtoto aache kulia au alale k.m. bembelezi.
8. Kukashifu/kukejeli mwenendo mbaya k.v. uchoyo, vivu, n.k.
9. Kufunza maadili au tabia inayokubaliwa na jamii k.v. ukarimu, uaminifu, n.k.

UBAYA WA NYIMBO

1. Nyimbo zingine hutumiwa kueneza hisia za kikabila.
2. Nyimbo zingine hutia watu kasumba.
3. Nyimbo zingine hutumiwa kueneza propaganda ili kushawishi watu.
4. Kupotosha kimaadili k.v. kuhimiza zinaa.
5. Mtu akizioea humlevya.

● AINA ZA NYIMBO

Aina za nyimbo. Kuna aina nyingi za nyimbo zikitofautishwa na nchi, utamaduni na waimbaji wenyewe.

Mifano ya nyimbo
Bembelezi, Wawe, Nyimbo za baharini, Nyimbo za nyiso, Nyimbo za taifa, Nyimbo za harusi, Nyimbo za dini Nyimbo za Hodiya, Nyimbo za uwindaji, Nyimbo za vita, Nyimbo za mapenzi, Kasida, Chekechea/nyimbo za watoto, Sifo, Nyimbo za siasa, Nyimbo za kimai, Tumbuizo, Nyimbo za mashujaa

1. NYIMBO ZA BEMBELEZI/BEMBEA

Nyimbo zilizoimbwa kumbembeleza/kumwongoa mtoto aache kulia au alale.

Sifa Za Bembea

1. Huimbwa na mama au walezi.
2. Aghalabu huwa fupi.
3. Huimbwa kwa sauti ya chini.
4. Huimbwa kwa sauti nyororo.
5. Zina mapigo ya polepole na taratibu.
6. Huwa na mahadhi mazuri.
7. Huimbwa aghalabu mtoto akiwa amebewa kwa mbeleko na mwimbaji akimpapasapapasa.

8. Zina urudiaji wa maneno ya kibwagizo.
9. Huwa na lugha ya kushawishi k.v. kutoa ahadi ya kununulia mtoto zawadi.

Majukumu Ya Bembea

1. Kumnyamazisha mtoto anapolia.
2. Kuwaongoa watoto walale.
3. Kutumbuiza watoto.
4. Kusuta wasiowapa watoto malezi mema.
5. Kuonya mtoto dhidi ya tabia hasi k.v. kulia ovyo.
6. Kusifu mtoto.
7. Kuonyesha msimamo wa jamii kuhusu mtoto.
8. Kumfariji mtoto k.m. kutokana na kuumia akicheza.

2. NYIMBO ZA WATOTO/CHEKECHEA

Zilizoimbwa na watoto wakati wa kucheza/shughuli zao.

Majukumu Ya Nyimbo Za Watoto

1. Kuburudisha watoto.
2. Kuwaelimisha watoto kuhusu jamii.
3. Kukuza umoja na ushirikiano baina ya watoto kwa kuwajumuisha pamoja na kucheza bila kujali kabila, tabaka, n.k.
4. Kukashifu tabia hasi miongoni mwa watoto k.v. uchoyo.
5. Kukuza ubunifu miongoni mwa watoto wanapobuni nyimbo zinazooana na michezo yao.
6. Kuifanya michezo ya watoto ipendeze.

3. NYIMBO ZA SIFA/SIFO

Za kujisifu au kusifu mtu kwa mchango wake katika jamii.

Sifa Za Sifo

1. Zaweza kuwa nyiso, za arusi za kutawazwa n.k.
2. Huimbwa katika muktadha maalum k.v. arusini, jandoni, n.k.
3. Hutumia sitiari au kufananisha na mnyama, mkuki, n.k.
4. Hupiga chuku sifa za anayesifiwa.

Majukumu Ya Sifo

1. Kusifu mtu kutokana na matendo yake mazuri.
2. Kutangaza mchango na mafanikio ya anayesifiwa.
3. Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga matendo mazuri ya anayesifiwa.
4. Kuburudisha watu katika sherehe fulani.
5. Kuangazia matendo ya wahusika.

4. HODIYA/ NYIMBO ZA KAZI

Zilizoimbwa wakati wa kazi.

Sifa Za Hodiya

1. Huimbwa watu wakifanya kazi k.v. uwindaji, ukulima, uvuvi, ubaharia, n.k.
2. Huimbwa na mfanyakazi mmoja au kundi la wafanyikazi.
3. Zina maneno ya kuhimiza.
4. Urefu wake hutegemea kazi.
5. Mdundo hutegemea kasi ya kazi kama inafanywa kwa kasi mdundo ni wa kasi, na kama ni polepole mdundo ni wa polepole.

Majukumu Ya Hodiya

1. Kuburudisha watu wakifanya kazi.
2. Kurahisisha kazi kwa kupunguza fikra za uchovu.
3. Kuhimiza bidii kazini.
4. Kuhimiza watu wapende kazi zao.
5. Kuondoa uchovu na ukinaifu wakati wa kazi.
6. Kuwatia moyo wafanyakazi wasikate tamaa.
7. Kutambulisha jamii kwa kuonyesha shughuli zake za kazi.
8. Kusifu kazi.
9. Kukashifu uvivu.
10. Kuonyesha matatizo na changamoto za wafanyikazi.
11. Kujenga umoja na ushirikiano baina ya wafanyakazi wanapozimba pamoja.

● AINA ZA HODIYA

- 1) *Wawe/Vave*
- 2) *Kimai*
- 3) *Nyimbo za uwindaji*

1. WAWE

Zinazoimbwa wakati wa kulima.

2. NYIMBO ZA UWINDAJI

Zilizoimbwa watu wakienda au kutoka katika uwindaji.

Majukumu Ya Nyimbo Za Uwindaji

- i. Kumburudisha mwindaji.
- ii. Kumtoa mwindaji upweke.
- iii. Kusifu mnyama.
- iv. Kujasirisha wawindaji.

3. KIMAI

- o Zinazoimbwa katika shughuli za majini k.v. uvuvi na ubaharia.

Majukumu Ya Kimai

- i. Kuburudisha wavuvi na mabaharia.
- ii. Kuwajasirisha ili kukabili adha za baharini.
- iii. Kuwatoa upweke.

6. NYIMBO ZA MAPENZI

Zilizoimbwa kutoa hisia za mapenzi.

Sifa Za Nyimbo Za Mapenzi

1. Huwa na ujumbe wa kimapenzi.
2. Maneno matamu yenye hisia nzito.
3. Matumizi ya chuku k.m. sili wala silali.
4. Huwa zina sifa au kashfa.

Majukumu Ya Nyimbo Za Mapenzi

1. Kuburudisha anayezisikiliza.
2. Kuomba uchumba au mapenzi.
3. Kusifu tabia au urembo/umbo la mpenzi.
4. Kusifu wapenzi.
5. Kukashifu mpenzi asiye na sifa nzuri.
6. Kusuta waliodhani penzi lisingefaulu.
7. Kupunguza uzito wa hisia k.v. huzuni au udhia baada ya kusalitiwa na mpenzi.

6. NYIMBO ZA ARUSI

- o Zinazoimbwa wakati wa kufunga ndoa.

Sifa Za Nyimbo Za Harusi

1. Huimbwa kuonyesha hisia za wazazi, jamaa na marafiki.
2. Hushauri maharusi na waliohudhuria kuhusu majukumu ya ndoa.
3. Wakati mwingine husifia maharusi.

Majukumu Ya Nyimbo Za Harusi

1. Kutumbuiza maharusi na waliohudhuria.
2. Kusifu maharusi.
3. Kutoa pongezi kwa Bw. na Bi. arusi kwa kujihifadhi vyema.
4. Kufunza majukumu ya ndoa.
5. Kutoa mwongozo wa kupambana na vikwazo ndoani.
6. Kusuta mahasidi waliodhani ndoa isingefaulu.
7. Kukanya na kutahadharisha watu wanaoingilia ndoa za watu kuziharibu.

7. NYIMBO ZA DINI

Zilizoandamana na shughuli za kidini.

Majukumu Ya Nyimbo Za Dini

1. Kuabudu Mungu ama miungu.
2. Kusifu mungu/miungu.
3. Kutoa shukrani kwa Mungu.
4. Kuomba mema kutoka kwa Mungu au miungu.
5. Kutoa mafunzo ya kidini.

8. TUMBUIZO

- o Nyimbo za kujipa burudani.
- o Huimbwa wakati wa mapumziko.

Majukumu Ya Tumbuizo

1. Kutumbuiza watu k.v. ngomani, arusini, n.k.
2. Kuwapa vijana mwongozo/kuadilisha.

9. NYISO/NYIMBO ZA TOHARA

Zinazohusiana na tohara.

Mfano

Ewe kilizi

Ulozowea kujificha

Nyuma ya mama kujikinga, dhidi ya milio ya radi ilo juu mbinguni

Jua kesho ni siku ya siku

Siku ya kujua mbichi na mbivu

Kutofautisha jogoo na vipora,

Ngariba taposhika, chake kijembe ndipo utakapojua bayani

Ukoo wetu si wa kunguru

Ikiwa u tayari

Kisu kukidhihaki

Sithubutu kamwe, uwanjani kuingia

sije kuniaibisha miye, amiyo na akraba nzima!

Sifa Za Nyiso

1. Huambatana na shughuli za jando (wavulana) na unyago (wasichana).
2. Huimbwa faraghani katika mazingira ya tohara pekee.
3. Huimbwa usiku wa kuamkia siku ya tohara.
4. Zilitoa sifa kwa waliotahiriwa, wazazi na wasimamizi wao.
5. Ziliimbwa kuwapa wavulana ujasiri wa kukabili kisu cha ngariba.
6. Zilitoa mafunzo kuhusu majukumu mapya baada ya kutahiriwa.
7. Hujumuisha watu maalum walioteuliwa kushiriki katika sherehe.
8. Huhusisha watu wa jinsia na umri fulani.
9. Maudhui yake hutegemea jinsia.

• Majukumu Ya Nyiso

1. Kuonyesha vijana wamevuka kutoka utotoni hadi utu uzima.
2. Kuwaandaa vijana kwa uchungu watakaouhisi kupitia kijembe.
3. Kuhimiza ujasiri na kukejeli uoga.
4. Kusifu wahusika kwa ujasiri wa kukabili kisu na kuingia katika utu uzima.
5. Kuburudisha waliohudhuria shughuli ya jando au unyago.
6. Kuelekeza vijana kwenye matarajio mapya ya jamii.

7. Kufunza majukumu katika utu uzima.
8. Kukuza umoja na ushirikiano katika jamii kwa kuwaleta wanajamii pamoja.

10. MBOLEZO/MBOLEZI

Nyimbo za kuomboleza.

Mfano

*Nalitazama jua likichwa, Matumaini yangu yakizama pamoja na miale
miekundu Nalidhani lilikuwa jinamizi tu*

Kwamba ulikuwa kesha n'acha

Walikuwa wameisha n'ambia Walimwengu

Ela nilikataa katakata waloosema

Nikajia kuamini waloamba yalikuwa

Uzushi

Hadi siku hii nilopokea waraka,

Waraka ambao ulikuwa jeneza ya kuzikia

Pendo letu la miongo miwili.

Sifa Za Mbolezi

1. Huimbwa wakati wa maafa, kifo, makumbusho ya mtu au kushindwa katika jambo k.v. vita.
2. Huimbwa kwa sauti ya chini.
3. Hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine.
4. Huwa na mapigo ya polepole au taratibu.
5. Huimbwa kwa toni ya huzuni/uchungu kuibua hisia za ndani za mwombolezaji.
6. Aghalabu haziandamani na ala.

Majukumu Ya Mbolezi

1. Kuwafariji au kuwasaidia waliofiwa kukabiliana na uchungu wa kupoteza mpendwa wao.
2. Kusifu aliyekufa kwa kutoa sifa zake chanya au michango yao.
3. Kubembebeza roho za wafu (mizimu) ili kusitokee maafa mengine.
4. Kuonyesha msimamo wa jamii kuhusu matokeo ya kifo k.v. husababishwa na pepo, maovu, njia ya kuingia mbinguni.
5. Kutakaswa hisia za huzuni za aliyefiwa kumpunguzia uzito wa kumpotezea mpendwa wake.

6. Kueleza kutoepukika kwa kifo.
7. Kukejeli kifo.

11. NYIMBO ZA TAIFA

Nyimbo zinazoimbwa na watu wa taifa fulani.

Majukumu Ya Nyimbo Za Taifa

1. Kutambulisha taifa fulani.
2. Kuonyesha utaifa.
3. Kuonyesha uzalendo (mapenzi kwa nchi).
4. Kuhimiza uzalendo na kuibua hisia za kizalendo
5. Kukashifu wasio wazalendo.
6. Kusifu taifa fulani.

12. NYIMBO ZA SIASA

Zinazoimbwa katika shughuli za kisiasa.

Mfano

Ewe mainga wa Ndumi

Siwe uloambia akina mama

Siku tulopiga foleni

Chakula cha msaada kupata

Turudishe vifaranga kwenye miji

Wageuke vijusi tena

Njaa isiwaangamize?

Siwe ulopita

Matusi ukitema

Chumvi na sukari kuturushia ja samadi?

Ukatununua vihela uloturushia

Ukatununua kura ukapata?

Sasa miaka mitano imemia

Waja tulaghai tena

Huna lolote safari hii

Ubunge umekudondoka ukitazama Wanyonge tumea/mua

Kwingine kujaribu

Majukumu Ya Nyimbo Za Siasa

1. Kuburudisha watu katika shughuli za kisiasa.
2. Kupinga dhuluma za viongozi.
3. Kusifu viongozi na sera zao.
4. Kukashifu/kukejeli wanasiasa wabaya.
5. Kuonyesha matarajio ya watawaliwa kwa viongozi.
6. Kusambaza elimu ya kisiasa.
7. Kuwatia wananchi kasumba.
8. Kueneza propaganda za kisiasa.
9. Kuzindua au kuhamasisha jamii kisiasa.
10. Kuliwaza wahasiriwa wa migogoro ya kisiasa.
11. Kutia watu ari ya kufanya jambo fulani k.v. kupigania haki zao.

13. NYIMBO ZA VITA

- o Zinazoimbwa na askari vitani au baada ya vita.

Majukumu Ya Nyimbo Za Vita

- Kuburudisha washiriki.
- Kufunza namna ya kukabiliana na adui.
- Kujasirisha washiriki.
- Kusifu askari vitani.
- Kukejeli uoga.
- Kusifu mashujaa wa zamani.
- Kukuza uzalendo kwa kuhimiza watu kuiga mashujaa.

14. KONGOZI

Nyimbo za kuaga mwaka katika jamii za Waswahili.

15. JADIIYA

- o Nyimbo za jadi ambazo hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
- o Huhusu matukio ya kihistoria k.v. shujaa, mateso, njaa, n.k.

16. NYIMBO ZA KUZALIWA KWA MTOTO

- Za kuonyesha au kuadhimisha kuzaliwa kwa mtoto.

2. MAGHANI

- Ushairi ambao hutolewa kwa kalima, yaani, nusu kuimba nusu kuongea.

Sifa Za Maghani

1. Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanapotambwa.
2. Hutolewa kwa kalima.
3. Hutungwa papo hapo.
4. Hutongolewa mbele ya hadhira
5. Hutungwa kwa ufundi mkubwa.
6. Hutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.

• AINA ZA MAGHANI

Kuna aina mbili kuu za maghani

1. maghani ya kawaida
2. maghani Simulizi

Maghani ya kawaida	Maghani Simulizi
a. Vivugo/ Majigambo b. Pembezi c. Tondozi	a. Sifo b. Tendi/Tenzi

1. MAGHANI YA KAWAIDA

- Ambayo hugusia maswala ya kawaida kama vile, mapenzi, siasa, harusi, kazi, maombolezo n.k.
- Husemwa/huganwa tu bila kusimuliwa.

2. MAGHANI SIMULIZI

- Maghani ambayo husimulia hadithi kuhusu tukio la kihistoria.
- Huhusu, mtu, tukio, kitu, mnyama, n.k.

Sifa Za Maghani

1. Hutokea kama hadithi.
2. Husimulia tukio la kihistoria.
3. Ni ndefu.
4. Waimbaji wake huitwa manju/yeli.

5. Huandamana na ala kama vile, zeze, marimba, n.k.

TOFAUTI KATI YA MAGHANI YA KAWAIDA NA MAGHANI SIMULIZI

Maghani ya kawaida	Maghani ya simulizi
Ni fupi Haitumii ala Huhusu maswala ya kawaida Husemwa	Ni ndefu Hutumia ala Huhusu maswala ya kihistoria Huimbwa

● MAGHANI YA KAWAIDA

Maghani ya Kawaida ni maghani yanayosifia mtu, kitu au hali katika jamii

- a. *Vivugo*
- b. *Pembezi*
- c. *Tondozi*

1. VIVUGO/MAJIGAMBO

Haya ni maghani ambayo mtunzi hujisifia (kujigamba) namna alivyo hodari katika nyanja fulani. Tungo hizi hutumia chuku na maneno ya kejeli kuwadunisha wapinzani wa mtunzi.

Sifa Za Majigambo

1. Hutumia nafsi ya kwanza, huibwa na mhusika mwenyewe.
2. Msimulizi hutumia maneno ya kujigamba.
3. Hutungwa papo hapo baada ya kufanya jambo hatari. k.v. kumuua Simba, kumuua msichana aliyewashinda wengi.
4. Msimulizi hutumia chuku kwa wingi ili kujisifu.
5. Hutungwa kwa ubunifu mkubwa na hutumia mbinu kama sitiari, vidokezi, ishara n.k
6. Anayejigamba hujipa majina/lakabu za kishujaa.k.v. mimi ni Simba.
7. Majigambo mengi huwa mafupi, lakini baadhi yake huwa marefu.
8. Huwa na matendo matukufu ya msimulizi.
9. Kuna kutaja jina la ukoo au nasaba ya anayejigamba.
10. Huwa na ahadi za matendo kutoka kwa msimulizi.
11. Mhusika huvaa maleba.

2. PEMBEZI/PEMBEJEZI

Aina ya tondozi inayokusudiwa kusifu watu aina fulani katika jamii kutokana na matendo au mchango wao. K.v. watawala, walezi wazuri, mashujaa wa vita, waganga mashuhuri hata wapenzi waliopigania pendo lao.

Mfano

*Nani kama wewe mama?
Nani anokufana 'mwaitu'
Subira uliumbiwa
Bidii nd'o jina lako la pili
Moyo wenye heba
Msimamo usoyumba
Anoelekeza kwa imani
Anoadhibu kwa mapenzi makuu
Mzazi, mlezi na rafiki wa dhati
Tangu siku za kusimama dede.*

• **3. TONDOZI**

Tondozi Tondozi ni aina ya sifo ambayo husifia watu mashuhuri katika jamii kama vile viongozi

Sifa Za Tondozi

- Huwa ni ushairi wa kusimuliwa
- Husifia mtu mwengine, mtu mashuhuri
- Hutumia chuku
- Hutumia mbinu kama sitiari, vidokezi, ishara n.k
- Hutaja matendo makubwa ya kiongozi anayesifiwa

Mfano wa Tondozi

*Kipungu kipungu
Nani kama yeye?
Hashindiki kwa nia
Hashindiki kwa shabaha
Hulenga mbinguni
Hutia ghera kufikiwa peo
Peo zisofikika kwa wanokata tama
Kipungu, kipungu, hachi tufani za anga.*

● MAGHANI SIMULIZI

Lengo la maghani ya aina hii ni kusimulia kisa fulani, historia, n.k.

Kuna fani mbili za Maghani ya Masimulizi:

1. Sifo
2. Tendi/ tenzi

1. SIFO

- Tungo za kusifu watu kutokana na matendo yao ya kishujaa.
- Sifa zake hukaribiana na za tenzi hasa ikiwa ni shujaa anasifiwa.

2. TENDI/TENZI

- Ushairi mrefu unaoelezea maisha ya mashujaa tangu kuzaliwa hadi kufa kwao. k.v. Utenzi wa Fumo Liyongo, Sundiata, Shaka Zulu, Wang`ombe waihura n.k.

Mfano wa Tenzi

Asiyemjua mjua aliongwe atamjua

Namjua kwa sifa zake alizokuwa nazo

Alisimika ufalme uliosifiwa

Akawa shujaa asiyetishwa

- Utungo huu waweza kuwa wimbo wa sifa au utendi!

Sifa Za Tenzi

1. Huwa masimulizi yanayotolewa kishairi.
2. Hutoa wasifu wa shujaa.
3. Huwa na matumizi ya chuku.
4. Wahusika hupewa sifa zisizo kawaida (kiungu).
5. Ni masimulizi mrefu.
6. Matumizi ya sitiari k.v. kulinganisha wasifiwa na wanyama wakali.
7. Huangazia matendo ya mashujaa.
8. Husimulia matukio ya kihistoria.
9. Huimbwa pamoja na ala ya kimuziki.
10. Hutungwa papo kwa papo na kuhifadhiwa katika ubongo.
11. Hujumuisha mbolezi zinazoonyesha anguko la shujaa.

Umuhimu Wa Tendi

1. Kuburudisha wanajamii.
2. Kusifu mashujaa wa jamii.

3. Kukuza uzalendo kwa kuhimiza wengine kuwaiga mashujaa.
4. Kukuza ubunifu kwa kutunga papo hapo.
5. Kuimarisha uwezo wa kukumbuka kwa kutungwa na kuhifadhiwa akilini.
6. Kuburudisha waliohudhuria sherehe ambapo yanatolewa.
7. Kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii.
8. Kukuza ufasaha wa lugha kwa fanani.
9. Kufunza maadili.

3. RARA

- Hadithi fupi na nyepesi za kishairi zenye visa vya kuisimua.

Mfano Rara

*Alichukua mkoba wake
 Akanipa kisogo
 Kana kwamba hakunijua
 Kana kwamba hakusema, "Hadi mauko".
 Hakujali penzi letu
 Hakujali wana
 Ambao ndiye alowapa uhai
 Alijua nilimpenda
 Ila hata hilo alijipa kujipurukusha
 Akayoyomea
 Akamezwa na ulimwengu.*

Sifa Za Rara

1. Huhusu mambo ya kubuni au ya kweli k.v. sherehe ya uhuru, kesi ya mauaji, n.k.
2. Huhusu maswala ibuka na ya kawaida.
3. Hadithi huwasilishwa katika beti.
5. Huandamana na ala za muziki.
6. Hutolewa kwa toni ya kitanzia.
7. Huwa na visa vya kuisimua.
8. Huwa na ucheshi wenye kinaya.
9. Maswala hayatolewi kwa uwazi bali hufumbwa na kudokezwa.
10. Huwa na uigizaji/utendaji.
11. Mambo yanayosimuliwa hupigwa chuku.

RARA NAFSI

- Ushairi ambao hutungwa na mtu kuelezea hisia, matatizo na fikra zake mwenyewe.

Mfano

*Muda umefika wa pingu kutiwa
Kutiwa silisili, kwani si utashi wangu
Ukoo waniuza, mithili ya kondoo sokoni
Mwambieni shangazi kwaheri nampigia
Hata angataka kuniopoa hawezi
Kwani mahari imetolewa
Mifugo kikwi nduguye amepokea
Kwaheri mama, kwaheri dada.*

Sifa Za Rara Nafsi

1. Hugusia maswala yanayoathiri hisia za mtu binafsi kama vile mapenzi, usaliti, talaka, kifo.
2. Huwasilishwa kwa njia ya uimbaji unaoandamana na ala ya muziki.
3. Mzungumzaji huzungumza moja kwa moja na hadhira au aliyeandikiwa rara hii-mkewe, mpenziwe, mwanawe, Mungu, miungu.
4. Hutolewa katika miktadha k.v. mazishi kusifu aliyekufa, harusi na Bi. Arusi kama ameshinikizwa kuolewa.

4. NGONJERA

- Mashairi ya kujibizana/kulumbana-yenye muundo wa kimazungumzo.

Sifa Za Ngonjera

1. Huwa na wahusika wawili au zaidi.
2. Mhusika mmoja huuliza jambo na mwingine hujibu.
3. Huendelezwa kwa njia ya wimbo.
4. Wahusika kupingana mwanzoni.
5. Wahusika huafikiana kufikiwa mwisho.

Umuhimu Wa Ngonjera

1. Majibizano hukuza ubunifu kwa kila mmoja kuonyesha umaarufu.

2. Kukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani.
3. Kuimarisha stadi ya kuongea.
4. Kuburudisha hadhira.

5. MASHAIRI MEPESI

Mashairi ya kawaida ambayo hupatikana katika ushairi simulizi.

Hujumuisha mashairi mafupi ya kihisia, kimapenzi, kusifu na kukosoa watu.

VIGEZO VYA UCHANGANUZI WA TUNGO ZA USHAIRI SIMULIZI

1. Kuainisha utungo kimaudhui/aina
2. Kuthibitisha ni aina fulani ya utungo wa kishairi/sifa.
3. Kutaja sifa zinazojitokeza za ushairi simulizi/utungo fulani wa ushairi simulizi.
4. Mukstadha ambamo unaweza kutolewa.
5. Kuandika mbinu za kifasihi zilizotumiwa katika utungo huo.
6. Kufafanua sifa za jamii zinazojitokeza katika utungo.
7. Kuandika majukumu ya aina hiyo ya utungo wa ushairi katika
8. Anayeimba/nafsiimbi ni nani?
9. Kuandika maadili yanayojitokeza katika utungo.
10. Kueleza toni ya utungo huo.

JITATHMINI 4

*Lulu, mwanangu tulia,
Wiwi mtoto lala, mvua imekuja
Si uongo hata na miti huichangamkia
mvua, hakuna haja ya kuelezwa,
Lulu mwana tulia,
Wiwi mtoto lala, mvua imekuja.*

Maswali

- i. Tambua kipera hiki (alama 2)*
- ii. Taja sifa nne za kipera hiki (alama 4)*
- iii. Eleza majukumu manne ya kipera hiki (alama 4)*

2. *He! he! he! weee!
Unayeogopa cha ngariba
Nani atatahiri badala yako
Eh, eh... ni babu yako
Eh, Eee!... kisu kikali mno!
Ukoo wetu sio wa waoga.*

Maswali

- iv. Huu wimbo unaitwaje? (alama 1)*
- v. Nini dhamira ya wimbo huu (alama 2)*

3. *Eleza tofauti kati ya Pembezi na Majigambo (alama 4)*

UTAFITI WA FASIHI NYANZANI

Utafiti ni uchunguzi, ni mbinu ya udadisi wa hali ya juu. Utafiti wa Fasihi Simulizi ni mbinu za kuchunguza, kukusanya data, kurekodi, na kuhifadhi data ya fasihi simulizi kwa matumizi ya vizazi vya baadaye.

HATUA ZA KUFANYA UTAFITI

1) Maandalizi:

Huhusisha mambo yafuatayo:

- 1) Uteuzi wa mada ya utafiti
- 2) Kubainisha na kueleza malengo ya utafiti huo
- 3) Kutambiwa eneo la kufanyia utafiti
- 4) Kutambua utafiti ambao tayari ulifanywa kuhusu mada yako.
- 5) Kukadiria gharama katika shughuli nzima.

2) Ukusanyaji Wa Data Yenyewe

Ukusanyaji unaweza kufanywa kupitia njia hizi:

- a) Kushuhudia
- b) Kujaza fomu
- c) Kushiriki
- d) Kuhoji. n.k

3) Kurekodi Data Yako

Unahitaji kurekodi data zako kupitia njia zifuatazo:

- a) Kuandika
- b) Kupiga picha
- c) Kuchukua video
- d) Kunasa habari. n.k

4) Kuchunguza Data

Data ambayo umekusanya inahitaji kuchunguzwa, kufasiriwa na kuandikwa upya, neno baada ya neno ili maana halisi inayokusudiwa isipotezwe.

5) Kuchambua Na Kufasili Data

Data uliyokusanya inahitaji kuchambuliwa, kulinganishwa, kufasiliwa, kutathminiwa na kisha kujumuishwa ili kupata matokeo kamili ya utafiti wako.

Mbinu za kukusanya data	Vifaa vya kukusanya data	Njia za kuhifadhi data
kuchunza/utazamaji kusikiliza kushiriki mahojiano hojaji kurekodi katika kanda kupiga picha kupiga picha za video	kamera za picha Vinasa sauti kalamu na karatasi kamera za video	bongoni/akilini kutumia maandishi Michoro maumbile na mazingira filamu, tepurekoda kanda za video kunasa sauti disk mweko, Kadi sakima rununu, tarakilishi

NJIA ZA KUKUSANYA FASIHI SIMULIZI

1. KUCHUNZA/UTAZAMAJI

Kwa kutumia mbinu hii, mtafiti hutazama kwa makini yanayotokea na yanayofanyika.

Umuhimu/ubora/uzuri

1. Kupata habari za kutegemewa na kuaminika.
2. Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
3. Ni njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
4. Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
5. Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji

Udhaifu wa mbinu ya kutazama

1. Shida ya mawasiliano.

2. Ugeni wa mtafiti. kusababisha washiriki kumshuku na kusitisha uwasilishaji
3. Ghali kwa kumbidi mtafi. kusafiri
4. Huhitaji muda mrefu

2. KUSIKILIZA WASANII WAKIWASILISHA TUNGO ZAO.

1. Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
2. Kupata habari za kutegemewa na kuaminika.
3. Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
4. Kikwazo cha mawasiliano-Si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
5. Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji.

Udhaifu wa kusikiliza

1. Shida ya mawasiliano - Si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
2. Huhitaji muda mrefu - kusafiri na kusikiliza.
3. Ugeni wa mtafiti. Kusababisha washiriki kutowasilisha ipasavyo.
4. Ghali kwa gharama ya usafiri.

3. MAHOJIANO

Kuhoji wanaofahamu mengi kuhusu Fasihi Simulizi.

Umuhimu wa mahojiiano

1. Kuweza kung'amua wakati mhojiwa anatoa habari zisizo za kweli.
2. Kuweza kufafanulia mhojiwa maswali ili kuweza kupata habari sahihi zaidi.
3. Kuweza kupata sifa za uwasilishaji k.v. toni/kiimbo, ishara n.k.
4. Ni rahisi kurekodi k.v. kwa vinasa sauti, video, n.k.
5. Kupata habari za kutegemewa na kuaminika

Udhaifu wa mahojiiano

1. Huhitaji muda mrefu.
2. Mhojiwa kutotoa habari kwa kutomwamini mtafiti kwa ugeni wake.
3. Kikwazo cha mawasiliano - si njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
4. Ghali kwa gharama ya usafiri.
- 5.

4. KUREKODI KATIKA KANDA ZA SAUTI /TEPUREKODA

Umuhimu wa kurekodi

- 1) Kuweza kudumu na kufikia vizazi vingi.
- 2) Sifa za uwasilishaji/uhai kama vile toni na kiimbo kuhifadhiwa.
- 3) Mkusanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa.
- 4) Kupata habari za kutegemewa na kuaminika
- 5) Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji

Udhaifu wa kuredodi

- 1) Chaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
- 2) Hakiwezi kunasa uigizaji.
- 3) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
- 4) Ghali kwa kuhitaji kununua kifaa na kumbidi mtafiti kusafiri.
- 5) Kurekodi kwa filamu na video

5. KUNASA PICHA ZENYE MIONDOKO NA SAUTI

1) Umuhimu wa Video

- 1) Video huhifadhi uigizaji, ishara na kiimbo/toni.
- 2) Kuonyesha uhalisi wa mandhari
- 3) Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa
- 4) Kazi iliyokusanywa hivi hudumu kwa muda mrefu.
- 5) Njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika
- 6) Kupata habari za kutegewa na kuaminika

Udhaifu wa Video

- 1) Chombo chaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti. kuathirika.
- 2) Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
- 3) Ghali kwa gharama ya usafiri na kununua filamu na kamera ya video.
- 4) Data yaweza kufisidiwa na hivyo kutowafikia walengwa.

6. KUPIGA PICHA KWA KAMERA

Hunasa picha zisizo na miondoko na sauti.

Umuhimu wa picha

1. Huonyesha uhalisi wa mandhari.
2. Huweza kuhifadhi ishara.

3. Mkusunyanyaji aweza kurudia uwasilishaji ikiwa hakuelewa.
4. Kupata habari za kuaminiwa na kutegemeka.

Udhaifu wa picha

1. Ghali kwa gharama ya usafiri na kununua kamera.
2. Sifa za uhai kama vile kiimbo haziwezi kuhifadhiwa.
3. Yaweza kukosa nguvu za umeme na utafiti kuathirika.
4. Data yaweza kufisidiwa na hivyo kutowafikia walengwa

7. KUSHIRIKI KATIKA KAZI YA FASIHI SIMULIZI K.V. NGOMA, SOGA, N.K.

Umuhimu wa kushiriki

1. Kuweza kupata hisia halisi za uwasilishaji.
2. Kupata habari za kutegea na kuaminika.
3. Njia bora kwa wasiojua kusoma na kuandika.
4. Kukuza utangamano wa mtafi na wanajamii.
5. Kuweza kunasa na kuhifadhi sifa za kiimbo, toni na ishara.

Udhaifu wa kushiriki

1. Kuchukua muda mrefu.
2. Ugeni wa msanii kusababisha washiriki kuwa na wasiwasi na kutotenda kama kawaida.
3. Njia ghali kwa kuhitaji mtafi kusafiri mbali.
4. Mtafi. aweza kusahau kwa kuhifadhi akilini.

8. KUTUMIA HOJAJI

- Fomu yenye maswali funge au wazi.

Umuhimu Hojaji

1. Gharama ya chini.
2. Yaweza kutumika katika mahojiano.
3. Huokoa muda kwani mtafi aweza kuituma na kuachia mhojiwa kujaza.
4. Hupata habari za kuaminika na kutegemeka.

Udhaifu Hojaji

1. Utata wa maswali kusababisha majibu yasiyo sahihi.
2. Si nzuri kwa wasiojua kusoma na kuandika.

3. Kutopata sifa za uwasilishaji kama vile kiimbo, toni na ishara.
4. Wahojiwa kukataa kuijaza kutokana na mwelekeo hasi dhidi ya hojaji na hivyo kukwamiza utafiti.

● **VIFAA VYA KUKUSANYA FASIHI SIMULIZI NA UDHAIFU WAKE**

1. Vinasa sauti/tepu-rekoda
2. Kamera
3. Filamu na video
4. Diski za kompyuta
5. Kalamu na karatasi

UMUHIMU WA KUNASA DATA

1. Kuweza kudumu na kufikia vizazi vingi.
2. Si rahisi kusahaulika-hubakia vile vile.
3. Si njia ghali kama vile video

UDHAIFU WA KUNASA DATA

1. Sifa za uwasilishaji kama vile toni, kiimbo/toni na ishara haziwezi kuhifadhika hivyo kupotea.
2. Hupunguza hadhira kwa kulenga tu wanaojua kusoma na kuandika na hivyo kuathiri usambazaji wake.

● **MBINU ZA KUHIFADHI FASIHI SIMULIZI**

Mbinu hizi zimegawika katika makundi mawili kv:

- i. **Mbinu za zamani**
- ii. **Mbinu za kisasa**

1. MBINU ZA KIZAMANI

Mfano;

- 1) Kuhifadhi Bongoni/akilini
- 2) maumbile na mzingira
- 3) Michoro

Udhaifu/Changamoto za Kuhifadhi Data Akilini

- ✓ Mtafiti/ fanani huweza kufa.

- ✓ Mtafiti huweza kusahau maswala aliyoweka akilini.
- ✓ Mtafiti huweza kuathirika kiakili.
- ✓ Mtafiti huweza kubadili aliyohifadhi akilini.
- ✓ Mfatiiti/fanani huweza kupoteza fahamu.

2. MBINU ZA KISASA

Mfano;

- i. Kutumia kanda za kunasa sauti
- ii. Video
- iii. Maandishi
- iv. Filamu
- v. Kupiga picha kutumia kamera
- vi. Tepu-rekoda
- vii. Sidi, VCD

Matatizo/Changamoto za kutumia mbinu za kisasa kuhifadhi data.

- ✓ Huhitaji ujuzi wa kutumia vifaa hivi.
- ✓ Ni ghali/ huwa na gharama ya juu.
- ✓ Huweza kupoteza data muhimu mitambo ikiharibika
- ✓ Haziwezi kufanya kazi bila nguvu za umeme

NJIA ZA KUHIFADHI FASHI SIMULIZI KWA JUMLA

1. Huhifadhiwa na binadamu akilini k.m. ngano hupokewa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.
2. Katika maumbile au mazingira k.m. fisi daima huchechemea, kinyonga naye hutembea pole pole.
3. Katika vifaameme k.m. nyimbo, hadithi, maigizo n.k. huweza kuhifadhiwa katika kanda za sauti, video, sidi na diski za kompyuta.
4. Katika michoro k.m. picha huhifadhi matukio maalum k.v. za kabila fulani likiwinda au likisherehekea.

UMUHIMU WA KUKUSANYA/KUHIFADHI FASHI SIMULIZI

1. Ili isipotee k.m. kwa kusahaulika.
2. Kuirekodi ili kuiendeleza kwa kuirithisha kwa vizazi vijavyo.
3. Ili kulinganisha Fasihi Simulizi za jamii mbalimbali na kuonyesha tofauti zake.
4. Ili kuhakikisha mtiririko ka ka uwasilishaji.

5. Kutunza historia ya jamii ili vizazi vijavyo viijue.
6. Ili kuziba mapengo ya utafiti. Yaliyomo kwa vile kuna tungo ambazo hazijatafiwa kwa kina.
7. Kuendeleza elimu ya jadi ya jamii.
8. Kuingiliana na jamii iliyo chanzo cha fasihi humwezesha kuelewa utamaduni na fasihi yake kwa ujumla
9. Humwezesha mwanafunzi kuona vipengele hai vya fasihi k.v. uigizaji, toni na kiimbo ambavyo husaidia kuielewa kwa kina.
10. Husaidia kuhifadhi tamaduni za jamii kwa nia ya kuzipitisha kwa vizazi vijavyo.
11. Husaidia kuelewa utamaduni wa jamii nyingine.
12. Humwezesha mwanafunzi kupata maarifa ya kufanya utafiti. katika taaluma nyingine k.v. sosholojia.
13. Kujua fasihi simulizi za jamii nyingine humfanya mtafi kuzielewa na kuzikubali jamii hizo na hivyo kuendeleza amani ka ka nchi.
14. Ili kusahihisha mawazo mapotovu kuhusu baadhi ya tanzu na vipera vya Fasihi Simulizi.

● **MATATIZO YANAYOMKABILI MKUSANYAJI WA FASIHI SIMULIZI**

1. Gharama ya utafiti. Kuwa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu k.v. kusafiria, kununulia vifaa.
2. Kutojaziwa hojaji kutokana na mtazamo hasi wa jamii dhidi ya ujazaji wake.
3. Wanajamii kukataa kutoa habari wakishuku mtafiti anawapeleleza au kwa kuona haya.
4. Wanajamii wengine kudai walipwe kabla ya kutoa habari na hivyo kukwamiza utafiti.
5. Mbinu nyingine k.v. hojaji huhitaji watu wanaojua kusoma na kuandika na ikiwa mhojiwa hajui utafiti. Utakwamizwa.
6. Uchache wa wazee na wataalamu wa Fasihi Simulizi kusababisha kukosekana au kupatikana kwa data isiyo ya kutegemewa.
7. Utawala kukataa kutoa idhini ya kufanya utafiti.
8. Kukosa ufadhili na utafiti. Kutofanywa kwa kutomudu gharama.
9. Muda wa utafiti kutotosha na hivyo kutopata habari za kutosha kuhusiana na mada yake.

10. Kikwazo cha mawasiliano ikiwa mtafiti. na mhojiwa hawatumii lugha moja na mhojiwa hajui lugha nyingine na kumbidi mtafiti. Kukodi mkalimani na gharama kuongezeka.
11. Ukosefu wa vyombo vya usafiri kunakochelewesha utafiti. na kutomalizika katika muda uliopangwa.
12. Ukosefu wa usalama k.v. kuvamiwa kwa kushukiwa anapeleleza na kuibiwa vifaa.

● **CHANGAMOTO ZINAZOKABILI UKUSANYAJI WA FASIHI SIMULIZI**

1. Ukosefu wa utafiti. wa kutosha kwani kuna vipera ambavyo bado havijaandikwa.
2. Uchache wa wataalamu wa kutafitia na kuendeleza utafiti.
3. Watu kuhamia mijini na kuingiliana na wa jamii nyingine na kufanya uhifadhi na urithishaji wa fasihi kutowezekana.
4. Mtaala wa elimu kupuuza lugha ya kiasili inayotumiwa kuhifadhi na kurithisha Fasihi Simulizi na hivyo kukatiza ukuaji wake.
5. Fasihi Simulizi kuhusishwa na ukale na hivyo kutoona haja ya kuirithisha na kuihifadhi.
6. Kuhifadhiwa kwa Fasihi Simulizi akilini kusababisha kusahaulika, kubadilika hata kufa kwake.

● **JINSI JAMII YA SASA INAVYOJARIBU KUHIFADHI FASIHI SIMULIZI**

1. Tamasha za muziki kunakokaririwa na kuimbwa mashairi.
2. Sherehe za arusi, jando, mazishi watu hupewa mawaidha.
3. Utegaji na uteguaji wa vitendawili kupitia redio na runinga.
4. Sarakasi za wasanii huhifadhi kipera cha vichekesho.
5. Ngoma za kienyeji kama isukuti katika hafla za kisiasa na harusi.
6. Utambaji wa hadithi hasa katika sehemu za mashambani.

JITATHMINI 5

- a. Jadili hatua tano zinazofuatwa wakati wa utafiti. (alama 5)
- b. Onesha kwa mifano minne jinsi jamii huhifadhi kipera cha ngano sasa. (al. 4)
- c. Ni changamoto zipi zinazoweza kumkumba mtafiti akifanya utafiti wa ngano nyanjani. (al.4)
- d. Eleza kwa hoja tano, umuhimu wa kushiriki kama njia ya kukusanya data. (al. 5)
- e. Umepewa jukumu la kukusanya data kuhusu michezo ya watoto ukitumia hojaji.
- i. Eleza manufaa matano ya kutumia mbinu hii. (ala. 5)
 - ii. Eleza changamoto tano za kutumia mbinu hii . (ala. 5)

Kidato Cha

3

Na

4

MTAALA WA KICD

SHABAHA:

1) Kufikia mwisho wa kidato cha 3, mwanafunzi awe na umilisi wa:

- *Utanzi wa maigizo*

- ✓ *Vipera vya maigizo*
- ✓ *Sifa za vipera tofautitofauti vya maigizo*
- ✓ *Umuhimu wa kila kipera cha maigizo*
 - *Utanzi wa mazungumzo*
- ✓ *Vipera vya mazungumzo*
- ✓ *Sifa za vipera tofautitofauti vya mazungumzo*
- ✓ *Umuhimu wa kila kipera cha mazungumzo*

2) Kufikia mwisho wa kidato cha 4, mwanafunzi awe na umilisi wa:

- *kufanya maigizo kutegemea shabaha na muktadha k.m jandoni, sherehe za arusi n.k*
- *Umilisi wa utafiti nyanjani.*
- *Ubunifu wa kutunga kazi mbalimbali za fasihi.*
- *Kutambua kila utanzi, vipera vyake, sifa na dhima yake.*
- *Kutambua njia mbalimbali za kukusanya tanzu na vipera tofautitofauti kutegemea shabaha.*

7

UTANZI WA MAZUNGUMZO

MAANA YA MAZUNGUMZO

Maongezi ya mdomo yenye usanii.

SIFA ZA MAZUNGUMZO

- 1) Huwa maongezi yenye usanii mkubwa.
- 2) Hutolewa mbele ya hadhira.
- 3) Hutolewa kwa njia isiyokera.
- 4) Huambatana na sherehe fulani k.m. taabili katika matanga.
- 5) Hutegemea sauti na vitendo.
- 6) Huhusisha matumizi ya ishara k.v. za uso, mikono na miondoko.
- 7) Huhitaji ustadi wa kuzungumza ili kuteka hadhira.
- 8) Hutolewa na watu wenye umilisi mkubwa wa lugha.

VIPERA VYA MAZUNGUMZO

Vipera vya mazunguzo
1) Hotuba 2) Mawaidha 3) Ulumbi 4) Maapizo 5) Malumbano ya utani 6) Soga

1. HOTUBA

- Maelezo yanayotolewa mbele ya watu kuhusu mada fulani.
- Huhusisha mada maalum sio suala lolote tu.

Umuhimu wa Hotuba

1. Kuelimisha kwa kupata maarifa ya kukabiliana na maisha k.v. jandoni na arusini.
2. Kuadilisha au kutoa nasaha hadharani.
3. Huimarisha ukakamavu wa kuzungumza kadiri watu wanavyotoa hotuba hadharani.
4. Kukuza ufasaha na umilisi wa lugha.
5. Kupalilia kipawa cha uongozi.
6. Kuelimisha kwa kupatia watu maarifa ya kukabiliana na changamoto za maisha.

AINA ZA HOTUBA

1. Risala

Hotuba inayowasilishwa mbele ya watu kueleza jambo fulani k.m. ya wafanyakazi kwa waajiri wao.

2. Mhadhara

Hotuba inayotolewa kwa hadhira fulani kufafanua somo au mada fulani.

3. Kumbukizi

Hotuba zinazohusu tukio fulani la kihistoria kuhusu mtu au kitu.

4. Mahubiri

Hotuba zinazohusu masuala ya kidini.

5. Taabili

Hotuba kuhusu aliyeaga dunia zinazohusu sifa zake nzuri.

2. MALUMBANO YA UTANI

Mazungumzo ya kutaniana.

AINA ZA MALUMBANO YA UTANI

1. Utani wa mawifi na mashemeji
2. Utani wa marafiki
3. Utani wa vijana
4. Utani wa watoto
5. Utani wa marika/ watu wa hirimu moja

Mfano wa malumbano ya utani

Wewe ni mweusi kiasi kwamba ukiingia chumbani taa zinazimika.

• AINA ZA MALUMBANO YA UTANI

1. Utani wa mababu/mabibi na wajukuu

Ee mume wangu, mbona walala mapema hivi? Utawezaje kulilinda boma letu ikiwa wewe ndiwe wa kwanza kujizika kitandani.

2. Utani wa maumbu (kaka na dada)

Wewe unajifanya jasiri na juzi baba alikukemea kidogo tu ukaanza kutetemeka kama kondoo aliyenyeshewa.

3. Utani wa mazishi

Afadhali umekufa tukakuzika, sasa maghala yetu yatasalimika.

4. Utani wa makabila/kiukoo

Wakikuyu wanapenda pesa kiasi kwamba maiti ikisikia mlio wa sarafu inaweza kufufuka.

- *Wakamba wa ukoo wa Akanga wanapenda nyama kiasi cha kula kijusi cha mbuzi.*

SIFA ZA MALUMBANO YA UTANI

1. Huwa kati ya watu wawili au makundi mawili ya watu.
2. Hufanywa kwa kujibizana papo hapo.
3. Hufanywa kwa njia isiyo ya kuudhi.
4. Hutumia maneno ya mizaha.
5. Hutumia lugha ya ucheshi.
6. Hufanywa na watu wenye uhusiano mzuri.
7. Huchukua njia ya ushindani kila mmoja akitaka kumpiku mwenzake.
8. Wataniano huwa wamekubaliana kufanya hivyo.
9. Hufanyika wakati unaofaa sio baada ya kukutana tu.
10. Huhusisha masimango au kumkumbusha mtu wema uliomtendea.
11. Hutumia chuku sana kuisitiza au kukejeli sifa fulani hasi.
12. Huhusisha wakati mwingine utaniaji wa wasiokuwepo ukiambatanishwa na uigizaji wa kuchekesha.
13. Hutegemea uhusiano ulio kati ya wanajamii au makabila.
14. Huandamana na sherehe kama vile, matanga.

UMUHIMU WA MALUMBANO YA UTANI

1. Kuburudisha kutokana na ucheshi.
2. Kuimarisha urafiki wa watu walio na uhusiano mwema wanaotania.
3. Hustawisha ufundi wa lugha.
4. Kukashifu tabia hasi k.v. ulafi, uchoyo, wivu, n.k.
5. Kukosoa wanajamii kwa njia ya kejeli/dhihaka
6. Kuimarisha umoja na ushirikiano kati ya wahusika.
7. Kuliwaza k.m. unaofanywa wakati wa maombolezo.

8. Kukuza na kudumisha mila na desturi za jamii.
9. Kukuza utangamano baina ya watu na wanajamii wanapokuja pamoja na kutaniana.
10. Kuhimiza watu kujieleza kwa uwazi kwa kupunguza urasmi miongoni mwa wanajamii.
11. Hudhirisha uhusiano mwema baina ya watu wa jamii fulani.

CHANGAMOTO ZA MALUMBANO YA UTANI

1. Mabadiliko katika jamii yaliyosababisha baadhi ya wanajamii kupoteza nyenzo hii.
2. Kuingiliana kwa watu wa jamii mbalimbali.

3. SOGA

Mazungumzo ya kupitisha wakati yasiyozingatia mada maalum.

• SIFA ZA SOGA

1. Hutokea baina ya watu wa rika moja.
2. Humithilisha uhalisia badala ya kuunakili.
3. Hutumia chuku na kufanya jambo lionekane kama halina uhalisia.
4. Hukejeli watu au hali fulani.
5. Wahusika ni wa kubuni.
6. Hutumia vichekesho kupunguza ukali wa ukweli uliomo.
7. Wahusika hupewa majina ya wanajamii husika.
8. Huwa na mafunzo au maadili.

• UMUHIMU WA SOGA

1. Kuburudisha kwa kuchekesha.
2. Kufunza maadili.
3. Kukejeli matendo yasiyofaa katika jamii
4. Kukuza ubunifu baina ya washiriki.
5. Kufunza kuhusu matendo na tabia za kibinadamu.
6. Huwa msingi wa utani unaokuwapo katika jamii.
7. Kuonya na kutahadharisha dhidi ya tabia isiyokubalika.

4. MAWAIDHA

Mazungumzo ya kutoa ushauri kuhusu jambo fulani.

- **SIFA ZA MAWAIDHA**

1. Huwasilishwa mbele ya watu.
2. Hugusia takriban vipengele vyote vya maisha ya binadamu.
3. Aghalabu hutolewa na watu wenye umri mkubwa.
4. Hulenga maudhui maalum na ya aina nyingi kutegemea jinsia, umri, shughuli, n.k.
5. Hutumia lugha ya kubembeleza na isiyoonyesha ukali.
6. Hutumia lugha ya kuathiri hisia.
7. Huwa na ufasaha mkubwa wa lugha.
8. Ni mawazo mazito kuhusu maisha.
9. Hutolewa katika miktadha rasmi na isiyo rasmi.
10. Ujumbe hulenga hadhira maalum k.m. ya kike au kiume.
11. Hutumia fani nyingine za fasihi kama vile, methali, misemo, ngano, nyimbo n.k. kupitisha mawaidha.
12. Huibua maadili yanayohitaji kuzingatiwa.

- **MUUNDO WA MAWAIDHA**

- 1). **Utangulizi**

Kutoa kauli ya kuvutia makini ya hadhira k.v. 'Utu uzima huenda na uwajibikaji', au kueleza kiini cha mawaidha.

- 2). **Mwili**

Kutoa wosia, maonyo, maelekezo kutegemea suala analotolea mawaidha akitumia jazanda, kupanda na kushuka kwa sauti, kimya, miondoko, kubadilisha kasi ya kuzungumza, kudondoa semi za watu maarufu, n.k.

- 3). **Hitimisho**

- Kuonyesha msimamo kuhusiana na suala analozungumzia.
- Kushirikisha hadhira ili kujua msimamo wao kuhusu suala alilowausia.
- Hadhira kutoa changamoto kuhusiana na mawaidha yanayotolewa.

UMUHIMU WA MAWAIDHA

1. Kuelekeza jamii kimaadili.

2. Kuelekeza kuhusu jinsi ya kukabiliana na changamoto maishani.
3. Kushauri jinsi ya kutenda jambo fulani.
4. Kujasirisha waoga na kuwapa ukakamavu.
5. Kuwaondolea wanajamii ujinga.
6. Kuhifadhi na kuendeleza mila na desturi za jamii.
7. Njia ya kipato kwa baadhi ya watu.
8. Kuelimisha kuhusu maarifa ya kuendeshea maisha, majukumu na matarajio ya jamii.

5. ULUMBI

Uwezo na ustadi wa kuzungumza kwa uhodari mkubwa.

MIKTADHA AMBAMO ULUMBI HUTUMIKA KATIKA JAMII

1. katika mijadala bungeni
2. katika hotuba za kisiasa
3. katika mahubiri maabadini
4. katika mijadala shuleni
5. Katika korti
6. katika shughuli za kijamii k.v. posa
7. katika sala/dua
8. katika maapizo
9. katika malumbano ya utani
10. katika majigambo/vivugo

● SIFA ZA ULUMBI

1. Hufanywa mbele ya hadhira.
2. Huwa na lengo maalum k.v. kushawishi, kuelimisha, kushauri n.k.
3. Hutumia tamathali za usemi kwa ufanifu mkubwa k.v. chuku, misemo, methali, n.k.
4. Lugha huwa yenye mvuto na ufasaha.
5. Hutumia lugha yenye taharuki na ushawishi.
6. Unenaji huambatana na utumizi wa ishara/ viziada lugha.
7. Uwasilishaji huwa sahili na wenye ujumbe mzito.
8. Huwa na urudiaji mwingi ili kusesitiza na kuvutia usikivu.
9. Huwa na matumizi ya taharuki k.v. mtuo.
10. Huwa na mtiririko mzuri wa mawazo.

- **SIFA ZA MLUMBI BORA**

1. Asiwe mwoga ili kuweza kuzungumza hadharani.
2. Asiwe na haya ili kuweza kuzungumzia mambo ya aibu inapobidi.
3. Awe mchangamfu na mcheshi ili kunasa makini ya hadhira na kuizuia isikina.
4. Awe na ufahamu mpana wa utamaduni wa hadhira asitumie maneno na ishara zinazoweza kuwaudhi au kupingana na imani za hadhira.
5. Awe na uwezo wa kuingiliana vizuri na hadhira ili aivutie.
6. Awe na kumbukumbu nzuri ili ulumbi wake utiririke vizuri.
7. Awe na uwezo wa kudramatisha ili kuonyesha picha fulani k.v. ishara za uso, mwili, miondoko kuonyesha picha ya analozungumzia.
8. Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
9. Aweze kubadilisha toni na kiimbo hadhira isikina.
10. Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira k.v. kwa maswali ya balagha ili kuondoa uchovu wa kusikiliza.
11. Awe na uwezo wa kutumia mtuo wa kidrama ili kuongeza taharuki, kusisitiza ujumbe na kuteka makini ya hadhira.

- **UMUHIMU WA ULUMBI**

1. Hukuza uwezo wa kujieleza na kusema hadharani kwa kujiboresha kadiri anavyoendelea.
2. Kigezo cha kuteulia viongozi wa baadaye kwani ushawishi humtambulisha mlumbi kama mwenye uwezo wa kuongoza.
3. Kuelimisha jamii kwa njia isiyochosha.
4. Kudumisha umoja na ushirikiano jamii inapokusanyika pamoja kusikiliza ulumbi.
5. Kuhamasisha na kuzindua jamii juu ya suala fulani.
6. Kushawishi walengwa wakubali jambo fulani.
7. Kukuza uwezo wa mwanajamii kushawishi na kupatanisha.
8. Kushawishi watu wapende jambo fulani.
9. Kuburudisha wasikilizaji.

6. MAAPIZO

Maombi maalum ya kumtaka Mungu, miungu au mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani au muovu.

Mfano

*Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,
Nami ndiye nilompa uhai mwana unoringia,
Anokufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu nawaone chozi langu, wasikie kilio changu,
Mizimu nawaone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje kulizwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!*

SIFA ZA MAAPIZO

1. Yalitolewa kwa waliokwenda kinyume na matarajio ya jamii. Mf Wezi, wabakaji, wauaji, waliosi wazazi wao, n.k.
2. Yalifanywa mahali maalum k.v. makaburini, porini, chini ya miti mikubwa, kwa msitu n.k.
3. Hutolewa kwa ulaji kiapo. Mf kuapisha viongozi bungeni na watawala katika jamii.
4. Yalitolewa na watu maalum, mf wazee, wazazi, mwathiriwa mwenyewe, watu maalum walioteuliwa, mizimu au miungu.
5. Maapizo huaminiwa yataleta maangamizi kwa jamii. Mf Maafa, magonjwa, laana, vifo au mtu kuwa wazimu.
6. Watoaji maapizo walikuwa wazungumzaji bora katika jamii (walumbi).
7. Maapizo hutumia lugha kali inayonuiwa kutia woga ili kutahadharisha dhidi ya maovu.

UMUHIMU MAAPIZO

1. Kuonya na kutahadharisha wanajamii dhidi ya maovu.
2. Hutumiwa kama nyenzo ya kuwaonya wanajamii dhidi ya matendo hasi.

3. Hutambulisha jamii- Kila jamii ina namna yake ya kuapiza na mitindo tofauti ya kutoa maapizo.
4. Hukuza umoja katika jamii- Kuwapo kwa kaida na miiko sawa, huwafanya watu kujihisi kuwa kitu kimoja..
5. Huadilisha - wanajamii hujifunza kutenda mema ili kuepuka laana..
6. Husaidia kuibua sifa za kimsingi za vipera vya fasihi simulizi.
10. Husaidia kulinganisha fasihi za jamii mbalimbali na kuonyesha tofauti zake.
11. Matokeo ya utafiti wa nyanjani husaidia kuziba mapengo yaliyopo ya utafiti.
12. Uhifadhi na huendeleza fasihi simulizi kwa vizazi vijavyo.
13. Ni muhimu kutafiti kuhusu fasihi simulizi ili kusahihisha mawazo potofu kuhusu baadhi ya tanzu na vipera vya fasihi simulizi.

JITATHMINI 6

1. *Fafanua muundo wa mawaidha yanayotolewa katika miktadha rasmi. (alama 3)*
2. *“Mwanangu, dunia haitaki papara. Ikiwa unataka kufanikiwa katika mustakabali wako kuwa mtoto mtiifu na mwongofu. Kumbuka kuwa asiye funzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu...”*
 - a. *Tambua na ueleze kipera hiki cha fasihi (alama 2)*
 - b. *Eleza sifa tatu za kipera hiki. (alama 3)*
 - c. *Fafanua dhima tano za kipera hiki katika jamii. (alama 5)*
3. *“Mabibi na mabwana. Siku hii ya leo nina furaha riboribo. Furaha ghaya. Furaha inayoshinda mwanamke aliyepata salama. Mbona nisiwe na furaha na buraha katika jamii hii iliyotuka ikashinda utukufu wenyewe?*
Jamii hii yetu imedumu kwa miaka na mikaka. Kisa na maana? Umoja wetu. Mshikamano wetu. Undugu wetu. Muungano wetu. Sote twafahamu fika bila chembe chochote cha walakini kwamba umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Nani asiyejua utu ni ubinadamu? Kwamba kinachotutofautisha na hayawani ni utu?
Utu imara na dhabiti usiotikisika wala kusukasuka katika mawimbi na dhoruba za aushi. Hakuna adinasi anayeweza kusimama tisti kama mbuyu akiwa pekee. Asiyejua kifai kwamba jifya moja haliinjiki chungu nani?
 - a. *Tambua kipera hiki cha mazungumzo cha fasihi simulizi. (Alama 1)*
 - b. *Huku ukitoa hoja tano, fafanua umuhimu wa kipera. (Alama 5)*
 - c. *Bainisha vipengele vya kimtindo utakavyotumiwa kuwasilisha kipera hiki. (a13)*
4. *Linganisha na ulinganue sifa za ulumbi na hotuba (alama 10)*

5. UTANZU WA MAIGIZO

MAANA YA MAIGIZO

Utanzu wa Fasihi Simulizi unaoambatana na vitendo.

Sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na vitendo.

Up

Sifa Za Maigizo

- 1) Huwa na watendaji au waigizaji.
- 2) Huwasilishwa mbele ya hadhira.
- 3) Huwasilishwa mahali maalum k.v. ukumbini.
- 4) Huwasilishwa kwa mazungumzo na matendo
- 5) Waigizaji hujivika maleba yanayooana ili kutia maigizo uhai.
- 6) Matayarisho kabambe hufanywa kabla ya maigizo.
- 7) Huweza kuambatana na ngoma pamoja na uimbaji.
- 8) Lugha ni yenye ufundi wa juu k.v. picha, mafumbo na tamathali.

- 9) Huweza kuambatana na sherehe fulani ya kitamaduni k.v. jando, matanga, n.k.
- 10) Huwasilishwa kwa lugha sahili.
- 11) Hujaa taswira zinazoweza kutambulika na hadhira.

Umuhimu Wa Maigizo

1. Kuburudisha wahusika na hadhira.
2. Kuimarisha uwezo wa kuzungumza hadharani-kupata ukakamavu jinsi mtu anapoendelea kuigiza.
3. Kukuza umoja na ushirikiano watu wanapojumuika pamoja kutazama maigizo.
4. Kukuza uwezo wa kukumbuka kwani mwigizaji huhitaji kukumbuka maneno halisi.
5. Kukejeli kitendo kisichofaa/cha kijinga alichofanya mtu.
6. Njia ya kipato/kuwatafutia riziki baadhi ya watu.
7. Kutoa nafasi kwa watu kudhihirisha vipawa vyao.
8. Kuonya na kutahadharisha watu dhidi ya kufaya mambo yasiyofaa.
9. Kuelimisha watu wafahamu jambo fulani k.v. ukimwi, ufisadi, n.k.
10. Kukosoa watu wanaofanya kinyume na matarajio ya jamii k.v. wivu, uchoyo, n.k.
11. Kupitisha maarifa na amali za kijamii.

PLOTI YA MAIGIZO

- 1) Utangulizi- kutambulisha mgogoro
- 2) Ukuzaji wa mgogoro
- 3) Kilele cha mgogoro
- 4) Usuluhishaji wa mgogoro

AINA ZA MAIGIZO

MAIGIZO YA KAWAIDA	MAONYESHO YA SANAA
<ol style="list-style-type: none"> 1) Michezo ya kuigiza 2) Ngonjera 3) Vichekesho 	<ol style="list-style-type: none"> 1) Mivigha 2) Ngomezi 3) Matambiko

4) Michezo ya watoto 5) Majigambo / vivugo	4) Ngoma 5) Maigizo ya uganga wa Ramli
---	---

1. MAIGIZO YA KAWAIDA

Maonyesho ya jadi yakiwa yameondolewa kwenye mazingira yake halisi.

Mifano: Michezo ya kuigiza, Ngonjera, Vichekesho,
Michezo ya watoto, Majigambo/vivugo

2. SANAA YA MAONYESHO

Matendo ya kweli yanayojitokeza katika jamii kulingana na mazingira yake halisi k.m. uganga, mazishi, unyago, ngoma, n.k.

Mifano: Mivigha, Ngomezi
Matambiko, Ngoma, Maigizo ya uganga wa Ramli

TOFAUTI KATI YA MAIGIZO YA KAWAIDA NA SANAA YA MAONYESHO

MAIGIZO YA KAWAIDA	SANAA YA MAONYESHO
1. Kuna wahusika maalumu. 2. Matukio huwa ya kuiga, si ya kweli. 3. Huweza kufanyika wakati wowote. 4. Hutumia vifaa maalumu ili kuwakilisha mazingira fulani. 5. Kuna jukwaa maalumu. 6. Kuna hadhira maalumu	1. Watendaji huweza kuwa hadhira pia. 2. Utendaji huonyesha mambo halisi na ya kweli katika jamii. 3. Hufanyika wakati maalumu kulingana na utamaduni wa jamii husika. 4. Hakuna vifaa maalumu. 5. Hakuna haja ya jukwaa 6. Wanaoshiriki utendaji huu hawahitaji kufanya mazoezi kabla ya utendaji wenyewe. 7. Kimuundo utendaji hufululizwa kutoka mwanzo hadi mwisho

● MAIGIZO YA KAWAIDA

Maigizo ya kawaida hutambulika kwa haraka, kwa mfano, michezo ya jukwaani. Watendaji hujitayarisha kabla ya kuenda mbele ya hadhira. Baadhi ya vipera katika kitengo hiki havikuwepo katika jamii za Kiafrika. Vinahusishwa na kuja kwa Wakoloni. Maigizo haya pia huweza kuingiliana na Fasihi Andishi kwa sababu huwa kuna maandishi kwanza, kama vile tamthilia au riwaya ambayo wahusika huisoma kabla ya kuigiza mbele ya hadhira maalumu.

1. MICHEZO YA KUIGIZA

Maigizo ambayo huwasilishwa na watendaji jukwaani mbele ya watu.

SIFA ZA Mwigizaji Bora

- a) Awe jasiri ili aweze kuigiza mbele ya watu/hadharani.
- b) Awe na ubunifu ili aweze kufanya uigizaji kuvutia na kuondoa ukinaifu.
- c) Awe na ujuzi wa kutumia ishara za uso, mwili na miondoko kuonyesha picha ya hali anayoigiza.
- d) Awe na ujuzi na ufasaha wa lugha ili kuwasilisha mawazo kwa njia mwafaka na inayovutia.
- e) Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti anazoigiza k.v. huzuni.
- f) Awe na uwezo wa kushirikisha hadhira kwa maswali ya balagha ili kuondoa uchovu.
- g) Awe na uwezo wa ufaraguzi/kubadilisha uigizaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika kutoka katika mazingira ya hadhira.
- h) Awe anaelewa utamaduni wa hadhira yake ili asitumie maneno na ishara ambazo zinaudhi ama kukinzana na imani zao.

2. VICHEKESHO

Michezo ya kuigiza inayokusudiwa kuzua kicheko ili kupitisha ujumbe k.m. vioja, vitimbi, Churchill show.n.k.

SIFA ZA VICHEKESHO

1. Vichekesho huigizwa.

2. Huwasilishwa kwa lugha sahili.
3. Hujaa taswira zinazoweza kutambulika na hadhira.
4. Hutumia mbinu ya kejeli, kinaya na tashira.
5. Vichekesho huwa vifupi.
6. Havihitaji uchambuzi wa ndani ili kuvielewa au kupata maana.

JUKUMU LA VICHEKESHO

1. Kuburudisha hadhira kwa kuchekeka.
2. Kuelimisha kwa kuonyesha jambo la kijinga alilofanya mtu.
3. Njia ya kuwapa watu riziki.
4. Hutumika katika hadithi kuifanya ivutie.
5. Kukejeli kitendo fulani kisichofaa alichofanya mtu fulani.
6. Kukashifu matendo hasi ya kijinga.
7. Kuadilisha ama kutoa funzo fulani la tabia njema.

3. NGONJERA

Ngonjera inayoambatana na uigizaji/utendaji.

• SIFA ZA NGONJERA

1. Kuweko kwa uigizaji/utendaji k.v. ishara za uso na mikono.
2. Huwa na wahusika wawili au zaidi.
3. Huendelezwa kwa njia ya wimbo.
4. Mhusika mmoja huuliza jambo na mwingine hujibu.
5. Wahusika kupingana mwanzoni.
6. Wahusika hufikia uafikiano kufikia mwisho.

4. MICHEZO YA WATOTO/CHEKECHEA

Michezo inayoigizwa na watoto katika shughuli zao.

• AINA ZA CHEKECHEA

1. Mchezo wa baba na mama
2. Kuruka kamba
3. Kujificha na kutafutana
4. Kukimbiza kibaramwezi dhidi ya upepo ili kizunguke
5. Mchezo wa baba na mama

SIFA ZA CHEKECHEA

1. Waigizaji ni watoto.
2. Huhusu shughuli za kiuchumi na kitamaduni k.v. arusi, siasa, ukulima.
3. Huandamana na nyimbo za watoto.
4. Huwa na miondoko mingi k.v. kujificha, kuruka.
5. Huwa na matumizi mengi ya takriri.
6. Huchezwa popote.
7. Huwa na kanuni fulani.
8. Hukoma watoto wakichoka au wakikiuka kanuni

● **UMUHIMU WA CHEKECHEA**

1. Kufunza watoto majukumu yao ya utu uzima.
2. Kuwatanguliza watoto katika sanaa ya uigizaji.
3. Kukuza ubunifu wa watoto kadiri wanapoendelea kuigiza.
4. Kudumisha utamaduni wa jamii.
5. Kuburudisha watoto.
6. Kukuza stadi ya uigizaji miongoni mwa watoto.
7. Kukuza utangamano miongoni mwa watoto kwa kuwajumuisha pamoja.
8. Kukashifu matendo hasi ya watu wazima kwa watoto.
9. Kuwapa watoto ukakamavu na kujiamini wakiwa wachanga.

5. MAJIGAMBO/VIVUGO

Ni uigizaji/maonyesho ya kujisifu, maringo na majigambo kutokana na ufanisi wa kutenda jambo lisilo la kawaida. Huonyesha kuwa yeye ni bora kuliko wengine.

Mfano

Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu

Ulojipamba kwa mabingwa

Wachezaji hodari wa ngoma

Ndimi dume liloingia nyanjani

Makoo yakatetemeka

Yakang'ang'ania, ngozi kusakata nani

Kijiji kizima kilinijua

Wazee walilienzi

*Wakamiminika kiamboni
Mabinti kunikabithi.*

- **SIFA ZA MAJIGAMBO**

1. Aghalabu huambatana na ngoma.
2. Hujitokeza, kujigamba na kisha kuendelea kucheza ngoma.
3. Anayejigamba hubeba zana zake za vita kama vile mkuki na ngao kuonyesha aliyotenda.
4. Anayejigamba huvaa maleba kuambatana na jambo analojisifia.

- **UTAMBAJI**

Usimulizi wa hadithi unaoambatana na uigizaji.

Huwa na matumizi ya maleba.

- **MAZINGIRA**

Uigizaji wa maumbile asilia yaliyozunguka jamii ya watu k.v. sauti za wanyama. Kuna matumizi ya viziuzui, matawi n.k.

- **SANAA YA MAONYESHO**

Sanaa ya maonyesho huashiria matendo ya kweli katika jamii. Matendo haya ni kama vile miviga ambayo imekuwepo tangu jadi. Mambo haya huongozwa na itikadi fulani za jamii husika. Kama ilivyo katika aina nyingine ya maigizo, sanaa ya maonyesho hujumuisha hadhira ambayo mara nyingi huwa watendaji.

Ikumbukwe kuwa sanaa ya maonyesho hujikita katika kuendeleza mila na desturi za jamii, si kuburudisha tu.

- 1). **NGOMA**

Uchezeshaji wa viungo vya mwili kuambatana na mdundo au miondoko maalum.

- **AINA ZA NGOMA**

1. Ngoma za wanawake
2. Ngoma za tohara
3. Ngoma za wanaume
4. Ngoma za sherehe

5. Ngoma za vijana
6. Ngoma za unyago na jando
7. Ngoma za wazee
8. Ngoma za arusi
9. Ngoma za kufukuza mapepo
10. Ngoma za kuaga mwaka

- **SIFA ZA NGOMA**

1. Huandamana na muziki na ala ya muziki k.v. ngoma.
2. Ngoma huchezwa mahali wazi na penye hadhira.
3. Wachezaji huvaa maleba maalum kulingana na funzo linalonuiwa.
4. Huwa na wahusika aina mbili; watendaji na watazamaji kwa wakati mmoja.
5. Huweza kuandamana au kutoandamana na sherehe.
6. Hutofautiana kulingana na jamii husika.

- **UMUHIMU WA NGOMA**

Kuburudisha kwa ufundi wa kucheza kwa kuzingatia miondoko.
 Kitambulisho cha jamii kwani kila moja ina aina yake ya ngoma.
 Kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii husika.
 Kukuza uzalendo kwa kuwafanya wanajamii kuionea fahari jamii yao.
 Kukuza umoja na ushirikiano kwa kujumuisha watu pamoja.

Kuelimisha kwa kupitisha mafunzo na maarifa.

2). MATAMBIKO

Tambiko (kutoka kitenzi "kutambika") ni utekelezaji wa ada/sadaka maalumu ili kutuliza mizimu au mapepo. Mara nyingi matambiko hufanyika kwa kuambatana na kafara. Baadhi ya makabila huweza kuchinja wanyama, wengine hutumia pombe na kadhalika. Kimsingi kafara linalotolewa katika tambiko hutegemea na kabila.

Hivyo basi, Matambiko ni utoaji wa kafara, Sadaka au ada inayotolewa kwa Mungu, mizimu, pepo au miungu ili wasaidie binadamu kutatua mambo magumu, kuomba radhi au kutoa shukrani.

Matatizo ni kama vile ukame, magonjwa, kukosa watoto, mafuriko au janga lolote lililomshinda binadamu nguvu na uwezo.

Sifa za matambiko

1. Hufanywa kwa utendaji wa maigizo
2. Hutolewa na wazee maarufu walioteuliwa.
3. Hufanyiwa mahali maalum k.v. pangoni, mwituni, n.k.
4. Huandamana na sala na kutoa sadaka.
5. Huandamana na utoaji kafara k.v. kuchinja mbuzi, n.k.
6. Huandamana na maombi au dua

Tanbihi: Matambiko huwa hayakubaliki sana katika dini mbalimbali ila huaminika katika makabila kama mila na desturi za jamii hizo. Matambiko sio uchawi wala uganga ingawa yanahusishwa na imani za ushirikina kwa sababu hii kipera hiki kinaendelea kupotea.



3) MAIGIZO YA UGANGA WA RAMLI

• SIFA ZA RAMLI

1. Mganga hujia kujua kwa hivyo vitendo vyake ni maigizo ya uganga wa madaktari.
2. Mengi katika matendo ya mganga hayana mashiko.
3. Aghalabu kafara hutolewa.
3. Waganga wanapopiga bao huvaa maleba kama vile ngozi, vibuyu, pembe, n.k.
4. Huweza kuwa na fimbo maalum.
5. Lugha maalum anayodai kuitumia kuwasiliana na misimu.
6. Mizimu humshauri mganga kuhusu ugonjwa na tiba inayofaa.
7. Mganga humchanja mgonjwa na kumpa dawa za miti shamba.

• UMUHIMU WA RAMLI

1. Waka mwingine mizizi ya mganga huponya.
2. Huwapa watu matumaini hasa walio na magonjwa yasiyo na tiba.
3. Dawa za mganga hupunga mashetani kwa wagonjwa wake.

4. Hukutanisha ulimwengu wa mizimu na ulimwengu halisi.
5. Waganga huburudisha wanapoigiza.

- **HASARA ZA RAMLI**

1. Mgonjwa huenda asipone kwani matendo mengi ya mganga ni ya kukisia.
2. Dawa za uganga zaweza kumdhuru mtu.
3. Malipo ni ghali na mtu hata aweza kufilisika akitafuta tiba ya ugonjwa usiopona.
4. Mazingira ya uganga husheheni uchafu mwingi.
5. Mgonjwa huridhika kwa muda mfupi halafu uhalisia hudhihirika.

4). MIVIGHA

Sherehe za kitamaduni ambazo hutokea katika kipindi fulani cha mwaka ambazo huonyesha mwanajamii ametoka kiwango kimoja hadi kingine.

AINA ZA MIVIGHA

1). Sherehe za tohara

Kutoka utotoni na kuingia utu uzimani.

2). Sherehe za ndoa

Kutoka ukapera hadi kuoa

3). Sherehe za kutambika

Kutoa sadaka kwa Mungu, miungu, pepo au mizimu

4). Sherehe za kutawazwa kwa kiongozi

Kutoka uraia na kuingia katika uongozi/utawala

5). Shughuli za mazishi/matanga

Kutoka uhai hadi ufu

6). Sherehe za kuwapa watoto majina

7). Sherehe za ulaji kiapo

8). Shughuli za posa

9). Ibada

HATUA ZA KUFANYA MIVIGHA

1. Kutoa mtu rasmi kutoka kundi moja la wanajamii.
2. Kumfundisha majukumu yanayohusiana na wadhifa mpya.
3. Kumwingiza rasmi katika kundi jingine.

● SIFA ZA MIVIGHA

1. Huandamana na matendo au kanuni fulani (mivigha).
2. Maleba maalum huvaliwa na wahusika kuwatofautisha na hadhira.
3. Hufanyika kwa kutumia lugha maalum au kimyakimya.
4. Kuna watu aina tatu: watendaji wanaoshiriki kuimba na kucheza, wale sherehe inafanyika kwa sababu yao na wanaoshuhudia tu.
5. Huhusisha vitendo maalum kama vile kula viapo, kutoa kafara, kucheza ngoma, n.k.
6. Huandamana na utoaji wa mawaidha.
7. Ugizaji hujitokeza pale mwanajamii anaingizwa katika kundi fulani kutoka jingine.
8. Huhusisha maombi.
9. Hufanywa mahali maalum sherehe hiyo inapofanyika k.m. tambiko hufanywa porini au pangoni.
10. Wahusika huweka ahadi za kutenda wema.
11. Huwa na mpangilio wa shughuli kuanzia mwanzo, kati hadi mwisho.

● UMUHIMU WA MIVIGHA

1. Kuburudisha kwa vile baadhi ya mivigha huhusisha nyimbo, ngoma na ugizaji.
2. Kutoa mafunzo ya utu uzima na elimu ya jadi.
3. Mivigha ya mazishi huliwaza wafiwa.
4. Kukuza utangamano miongoni mwa wanajamii kwa kuwajumuisha pamoja katika mivigha yao.
5. Kuashiria mwanajamii ametoka kiwango kimoja cha maisha hadi kingine.
6. Kujenga uhusiano bora kati ya jamii na miungu au mizimu.
7. Kitambulisho cha jamii kwani kila moja ina aina yake ya mivigha.
8. Kudumisha mila za jamii.
9. Kuelimisha jinsi ya kukabiliana na changamoto maishani.
10. Kuadilisha kwa kufunza tabia zinazokubalika na jamii k.v. uaminifu, utiifu, n.k.
11. Kukashifu vitendo vya uoga.
12. Kukuza uzalendo kwa kuhimiza wanajamii kuonea fahari tamaduni zao.
13. Msingi wa wanajamii kujitambulisha na kuonea fahari jamii yao.

● HASARA ZA MIVIGA

1. Baadhi ya mivigha huhatarisha afya na maisha k.v. kutahiri watoto wa kike.

2. Baadhi ya sherehe hukiuka maadili kama vile kwa kuruhusu matusi, hata kushiriki ngono.
3. Baadhi yaweza kusababisha hasara kama vile kueneza ukimwi k.v. tohara kwa kisu kimoja.
4. Huzua tofauti za kijinsia k.v. mwanamume kujiona bora kuliko mwanamke.
5. Kuzua utabaka baina ya waliopashwa na wasiopashwa tohara.
6. Baadhi ya mivigha hukiuka malengo ya kitaifa k.m. ukeketaji ni ukiukaji wa haki za binadamu
7. Kunayo hujaza watu hofu k.v. kufukuza mapepo kunakohitaji kafara ya binadamu.
8. Baadhi huhusisha ushirikina na hivyo kusababisha uhasama baina ya koo.
9. Baadhi hugarimu kiasi kikubwa cha pesa na kuifilisi familia.

5. NGOMEZI

● NGOMEZI

Uwasilishaji wa ujumbe kwa kupiga ngoma au zana nyingine ya kimuziki.



● SIFA ZA NGOMEZI

1. Kuwepo kwa ngoma au ala nyingine kama vile panda.
2. Mapigo ya ngoma hueleweka tu na jamii husika.
3. Mapigo kufuata toni au ridhimu maalum kuwasilisha maneno fulani.
4. Kuwepo kwa hadhira au wasikilizaji.
5. Kueleweka kwa mapigo hayo na wanajamii husika pekee.
6. Makini huhitajika ili kupata midundo.

● AINA ZA NGOMEZI

1. a) Taarifa

Huarifu kuhusu jambo k.m. msimu wa kuanza kutayarisha mashamba, kuitwa katika mkutano, kazi ya ujima n.k.

1. b) Tahadhari

Hutoa tahadhari kuhusu mavamizi kama wizi wa mifugo, vita, majanga kama moto, mafuriko n.k.

1. **c) Uhusiano**

Kuita watu kwa sherehe.

• **UMUHIMU WA NGOMEZI**

1. Njia ya mawasiliano kwa jamii zisizojua kusoma.
2. Husaidia wanaokabiliwa na ugumu wa mawasiliano.
3. Kuharakisha mawasiliano katika masafa mafupi.
4. Kutoa taarifa kuhusu matukio fulani k.m. ndoa, kifo n.k.
5. Husaidia kupitisha jumbe za dharura.
6. Kutahadharisha wanajamii kuhusu tukio la hatari/dharura k.v. vita, gharika n.k.
7. Kuficha siri kwa kuwasilisha ujumbe kwa njia isiyoeleweka.
8. Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wa jamii.
9. Namna ya kudhihirisha ufundi wa kutumia zana kama vile, ngoma.
10. Kitambulisho cha jamii kwani kila jamii hupitisha ujumbe kwa mapigo tofauti.

• **UDHAIFU WA NGOMEZI**

1. Si kila mtu anayeweza kufasiri ujumbe unaokusudiwa.
2. Mapigo hayasikiki mbali na hivyo husikika na idadi ndogo ya watu.
3. Mapigo yaweza kuhitilafiana na hivyo kufasiriwa kwa namna tofauti.

• **NGOMEZI ZA KISASA**

1. Milio ya ambulensi, magari ya polisi na zimamoto.
2. Kengele za kubisha hodi nyumbani zinazotumia umeme.
3. Kengele shuleni, makanisani, n.k.
4. Toni za rununu zinazowakilisha aina mbalimbali za jumbe.
5. Ving'ora vya kuashiria moto umetokea katika majumba ya ghorofa, benki, hospitalini, n.k.

• **Changamoto za ngomezi katika jamii ya sasa**

1. Mwingiliano wa jamii mbalimbali unaosababisha kutofasiri ujumbe kwa njia moja inayotakikana.
2. Viwanda na majumba marefu kusababisha kutosikika kwa sauti au milio ya ngoma.

3. Njia nyingine za kisasa za mawasiliano zinazotumiwa kwa wingi na kwa wepesi.
4. Uhaba wa zana kama vile baragumu na zumari zilizokuwa zinatumika.
5. Mabadiliko ya maisha kuleta ubinafsi na kusababisha wengi kutoitikia wito wa vyombo.

JITATHMINI 7

a). Ingawa tanzu za fasihi simulizi hutofautiani, tanzu zote hutegemeana ili kukamilisha malengo yake, jadili (alama 20)

Wewe ni mwigizaji wa michezo ya jukwaani. Eleza mambo sita ambayo utazingatia ili kufanikisha uigizaji wako. (alama 6)

b). Mbinu ya uigaji sauti ina umuhimu gani katika fasihi simulizi: (alama 4)

c). Tofautisha kati ya maigizo ya kawaida na sanaa ya maonyesho (alama 2)

d). Taja aina tatu za ngomezi (alama 3)

e). Eleza tofauti ya matambiko na miviga (alama 4)

f). Tambua utungo huu kama kipera cha maigizo (alama 1)

“Wewe ni mweusi sana hadi ukibeba mtoto, analala akidhani ni usiku”

g). Linganisha na ulinganue sifa za miviga na ramli (alama 10)

h). Linganisha na ulinganue sifa za ngomezi na sanaa ya Ngoma (alama 6)

MCHANGO WA FASIHI SIMULIZI KATIKA FASIHI ANDISHI

Fasihi simulizi ina mchango mkubwa sana katika Fasihi Andishi kifani na kimaudhui

A. KIMAUDHUI

Dhamira nyingi ambazo ndicho kiini cha maandishi mengi katika Fasihi Andishi zilikwishajadiliwa katika Fasihi simulizi. Dhamira hizo ni kama vile mapenzi, siasa, matabaka, uhuru, ukombozi, usawa, unyonge wa mwanamke, uchawi, ushirikina n.k Fasihi Simulizi haijavumbua dhamira mpya kabisa bali maudhui/dhamira zote za kale.

B. KIFANI

Vipengele mbalimbali vya fani ya fasihi simulizi katika kufikisha ujumbe kwa jamii zao. Vipengele hivyo ni:

- 1) **Muundo.** Fasihi Simulizi muundo wake ni wa moja kwa moja. Pia kuna baadhi ya maandishi wa Fasihi Andishi ambao wametumia muundo wa moja kwa moja. Mfano Riwaya ya Kuli (1979) ya Shafi A. Shafi ametumia muundo wa moja kwa moja.
- 2) **Mtindo wa usimulizi.** Fasihi Simulizi hutumia mtindo wa masimulizi. Pia kuna baadhi ya maandishi wa Fasihi Andishi ambao hutumia mtindo wa masimulizi. Mfano, Riwaya ya Shida (1975) ya Balisdya.
- 3) **Matumizi ya fantasia.** Hali ya kuwepo kwa mambo ya ajabuajabu katika kazi ya fasihi yasiyotarajiwa kutokea katika maisha ya kawaida. Mfano riwaya ya *walenisi na kusadikika*. Huu ulikuwa ubunifu wa fasihi simulizi.
- 4) **Wahusika.** Waandishi wa Fasihi Andishi hutumia wahusika wasio binadamu katika kazi zao ambao kwa kawaida hupatikana katika Fasihi simulizi tu. Mfano Mashetani (1971), Pambo (1975), Adili na Nduguze

(1952) Kusadikika (1951) na Kufikirika (1967) wametumia wahusika mashetani ambao hupatikana katika Fasihi simulizi tu. Wahusika kama wanyama, majini, mazimwi hupatikana katika Fasihi simulizi tu.

- 5) **Matumizi ya hadithi ndani ya hadithi.** Hapa wahusika husimulia hadithi mbalimbali katika Fasihi andishi. Hawa husimuliana hadithi za kimapokeo ambapo hadithi ni kipera cha Fasihi simulizi. Mfano Njozi iliyopotea (1980), Lina Ubani (1984), Mashetani (1971)
- 6) **Matumizi ya mtambaji hasa katika tamthilia.** Waandishi wengi wa tamthiliya wametumia mbinu ya utambaji ambapo wanakuwa na mtambaji anayetamba hadithi fulani. Mfano, Lina Ubani (1984), Nguzo mama (1980), Pambo (1975)
- 7) **Matumizi ya mianzo ya hadithi za fasihi simulizi.** Mfano, tamthiliya ya Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi (1970) Kilio Chetu (1995), Kivuli kinaishi (1990), Riwaya hizi zimetumia mianzo maalum ya Fasihi simulizi mfano, paukwa....., pakawa.
- 8) **Matumizi ya semi mbalimbali.** Fasihi andishi hutumia semi mbalimbali ambazo ni tanzu za Fasihi Simulizi. Semi ambazo hutumiwa sana ni misemo, nahau, methali, tamathali, vitendawili na tanzu nyingine
- 9) **Matumizi ya ushairi na nyimbo.** Waandishi wengi hutumia sana nyimbo katika kazi zao ili kuzipa mvuto, mfano, Riwaya ya Njozi iliyopotea (1980), tamthiliya ya Kilio Chetu wametumia sana nyimbo katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika.

NJIA ZA KUENEA KWA FASIHI SIMULIZI

a) Kuanzishwa kwa vikundi vya sanaa na muziki, vikundi mbalimbali vya sanaa na muziki vilianzishwa ambavyo kazi yake ni kuendeleza tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi hapa nchini. Vikundi vya sanaa za maonyesho, vikundi vya taarabu na muziki, mfano, Ottu Jazz Band, Kilimanjaro orchestra, Kilwa Band n.k vinafanya kazi kubwa ya kueneza na kuendeleza Fasihi Simulizi hapa nchini.

b) Mwingiliano na fasihi andishi, kuenea kwa kazi ya fasihi simulizi kwa asili ni kwa mdomo na masikio, yaani usimulizi. Hata hivyo, maendeleo ya watu yamefanya baadhi ya kazi za Fasihi Simulizi zienee kwa maandishi. Maandishi ni jitihada za kuhifadhi kazi ya Fasihi simulizi na kuifikisha mahali ili itambiwe au isimuliwe. Hadithi mbalimbali kama vile Hekaya za Abunuasi

(1915), Hadithi za Esopo (1890), Fasihi Simulizi ya Mtanzania. Hadithi (1977), Hizi zote zimehifadhiwa na kuenezwa kwa maandishi.

c) Fasihi Andishi inatumia vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi katika uandishi wake na hivyo kuviendeleza. Vipengele hivyo kama vile, Matumizi ya semi mbalimbali, matumizi ya nyimbo, matumizi ya hadithi ndani ya hadithi, matumizi ya mianzo na mishilizo ya hadithi za Fasihi Simulizi, matumizi ya majigambo, utani n.k.

d) Kwa sasa methali, vitendawili, nahau, vimewekwa katika maandishi kwa ajili ya kumbukumbu za baadaye na hivyo vinaenezwa kwa njia ya maandishi.

e) Ufundishaji shuleni na vyuoni, mfumo wa elimu nchini nao umesaidia kueneza Fasihi Simulizi kwa kiasi kikubwa hapa nchini. Kwa sasa, fasihi simulizi ni somo linalofundishwa toka darasa la kwanza hadi ngazi za juu (chuo kikuu). Vilevile kuna vyuo hapa nchini vinavyofundisha baadhi ya tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile sanaa za maonyesho na muziki, mfano chuo cha Bagamoyo, Butimba, Nyegezi na Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam.

f) Mabadiliko ya kiteknolojia, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa sasa fasihi simulizi inaenezwa kwa vyombo vya habari kama vile kaseti, redio, video, runinga, mitandao ya kijamii n.k. Mfano, Redio Tanzania (TBC) kupitia kipindi chake cha “Mama na Mwana” “Watoto Wetu” vimesaidia sana kueneza Fasihi Simulizi hapa nchini Tanzania. Runga nazo zimesaidia sana kueneza Fasihi Simulizi nchini kupitia vipindi mbalimbali vya michezo ya kuigiza.

g) Mwingiliano wa mataifa mengine. Katika mwingiliano huu muziki umesaidia sana kukuza Fasihi Simulizi. Hali hii imesaidia kuleta muziki wa kizazi kipya (muziki wa kufokafoka) pamoja na Rege. Vijana wa kizazi kipya wamechota miundo na mitindo ya muziki kutoka nje na kuendeleza muziki wao ingawa maudhui bado wanayojadili ni yale yale yaliyojadiliwa na wanamuziki wa zamani.

h) Matumizi ya Fasihi Simulizi katika sayansi na teknolojia yamesaidia sana kuenea kwa Fasihi Simulizi kwani Fasihi Simulizi inapata hadhira kubwa kwa wakati mmoja lakini hadhira hiyo haionani ana kwa ana na fanani wao kwa kutumia vyombo hivyo vya sayansi na teknolojia.

ATHARI ZA SAYANSI NA TEKNOLOJIA KATIKA UWASILISHAJI NA UENEZAJI WA FASIHI SIMULIZI

Mwanzo, Fasihi Simulizi iliwasilishwa na kuenezwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo, hivyo fanani na hadhira walionana ana kwa ana wakati wa uwasilishaji lakini zama hizi za sayansi na teknolojia, uwasilishaji na uenezaji unatumia vyombo vya habari kama vile redio, video, televisheni, kanda za kunasia sauti, mtandao na hata kompyuta. Mara nyingi hadhira haiwi ana kwa ana na fanani. Hutokea hadhira ikawa inaangalia runinga au sinema au tamthiliya jukwaani. Kwenye mazingira kama hayo si rahisi hadhira kushiriki kikamilifu katika utendaji.

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia fasihi inaathiriwa katika vipengele vifuatavyo: -

- 1) **Uwasilishaji.** Mwanzoni, Fasihi simulizi iliwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo, hivyo fanani na hadhira walikuwa wanaonana ana kwa ana wakati wa uwasilishaji lakini katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia, uwasilishaji wa Fasihi simulizi unatumia vyombo kama vile redio, runinga, video, kanda, mtandao na hata kompyuta na sio lazima msanii awepo.
- 2) **Uhifadhi.** Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia sasa fasihi simulizi inaweza kuhifadhiwa vizuri zaidi kuliko inavyofikiriwa na wanamapokeo kwani leo hii Fasihi simulizi inaweza kuwekwa katika mkanda wa kompyuta (flash disc) CD, DVD, maandishi n.k. na ikaendelea kuwepo kwa miaka mingi sawasawa na Fasihi andishi hata zaidi. Kwa upande wa video na DVD, uhifadhi wake huendelea kuonyesha vitendo na sauti huweza kudumu hata zaidi ya maandishi.
- 3) **Wakati na mahali.** Zamani fasihi simulizi ilifanyika sana saa za jioni, kando ya moto au barazani. Aidha, kwa vile Fasihi simulizi hutolewa redioni inaweza kusimuliwa wakati wowote na mahali popote ambapo kipindi kinasikika na kwa saa na wakati huo. Majumbani, mijini, watoto hawazunguki moto tena, bali husubiri wakati kipindi kinaporushwa kwa siku maalumu na wanaizunguka runinga au redio.
- 4) **Hadhira au ushirikishwaji wa hadhira.** Zamani hadhira ya fasihi simulizi ilikuwa inaonana ana kwa ana na fanani wake wakati wa uwasilishaji

wake. Hadhira iliweza kuchangia kazi ya fasihi hiyo na hata kuathiri uumbwaji wake, ikaitwa hadhira tendi. Lakini katika muktadha wa maendeleo ya sayansi, si lazima fanani na hadhira waonane ana kwa ana.

● UHIFADHI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI

Kwa sasa, fasihi simulizi inaweza kukusanywa na kuhifadhiwa kwa njia zifuatazo:

a). KICHWA: Uhifadhi wa Fasihi simulizi ni katika vichwa vya watu kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Jambo hili limekuwa likifanyika kwa muda mrefu sana. Hivyo, kutokana na kuhifadhiwa katika vichwa ndio maana Fasihi simulizi imekuwa ikirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

b). MAANDISHI: Tangu maandishi yagunduliwe, baadhi ya kazi za Fasihi simulizi zimekuwa zikihifadhiwa kimaandishi kwa ajili ya kumbukumbu ya baadaye. Kazi za fasihi simulizi zikihifadhiwa katika maandishi inaweza kufanya watu wasijue ni simulizi au andishi. Hata hivyo, vidokezo kadhaa husaidia kujua kazi za Fasihi simulizi kama vile kuwa na mianzo maalum, mfano “Paukwaa! Pakawa! Au hadithi..... hadithi njoo” n.k. Aghalabu Fasihi simulizi huwa na mtiririko (muundo) wa moja kwa moja usio na urejeshi.

c). KANDA ZA KUNASIA SAUTI (tepurekoda): Hii ni njia mojawapo inayotumika kuhifadhi tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Kanda hizo hushika sauti pamoja na vidokezo vyake. Kwa hivyo wasikilizaji ili wapate wanachokitaka, lazima wanunue kanda hizo.

d). KANDA ZA VIDEO: Runinga na filamu za sinema CD, DVD na Kompyuta/tanakilishi. Mtandao, picha za video hurekodi sura na sauti, Picha hizo hutembea na kuonyeshwa kwenye skirini ya video na runinga. Picha za sinema hupigwa kwa aina maalumu za kamera ambazo hupiga picha za mfululizo katika utepe maalumu. Picha hizo huonyeshwa kwa mashine na huonekana zinatembea. Kamera nyingi za sinema za siku hizi zina mitambo ya kurekodi sauti pia. Hivyo kwa kutumia filamu za sinema na video tunaweza kuhifadhi na kuonyesha kazi za Fasihi simulizi.

USASA WA FASIHI SIMULIZI

Usasa ama uleo wa Fasihi Simulizi unagubikwa na swala zima la makuzi na maendeleo ya teknolojia. Ingawa Fasihi Simulizi inafaa kuhifadhiwa akilini na kuwasilishwa kwa njia ya mdomo, teknolojia imeathiri pakubwa maana hii ya awali.

Tunapozungumzia juu ya usasa katika Fasihi Simulizi, tunazungumzia jinsi ambavyo tunaweza kuitumia teknolojia mpya katika kuihifadhi, kuiwasilisha, kuikosoa, kuburudisha na hata kuichangia mada ya Fasihi Simulizi. Na hayo yote yanawezekana kupitia televisheni, kompyuta, mikanda ya video, mikanda ya CD, barua pepe, simu za mkononi, setelaiti n.k.

- ✓ **Kwanza**, katika kuiwasilisha Fasihi Simulizi kwa watu wengi walio mbali na fanani, kwani sayansi imewezesha uwasilishaji ambao si lazima wahusika wote wawili wawe pamoja yaani fanani na hadhira.
- ✓ **Pili**, katika kuihifadhi fasihi simulizi ili vizazi vingine viweze kuirithi, nyanja hii ya fasihi hutumia vyombo vya kisasa kabisa vya kuhifadhi kama vile mikanda ya video, DVD, tepurekoda na utepe, tarakilishi, vipakatalishi, tarakiba (tab), rununu za kisasa (smart phones), kadi sakima (memory card), diski mweko (flash disk), CD mtandao wa You tube n.k
- ✓ **Tatu**, katika kuchangia mada, teknolojia mpya inatumika kama kiunganishi kati ya fanani na hadhira.
- ✓ **Nne**, katika kukosoa jamii hii hufanyika kupitia televisheni, video hasa kwenye michezo ya kuigiza (tamthilia). Kupitia video na televisheni wasanii huikosoa jamii pale inapokuwa imekosea au imepotoka, kwa hivyo, jamii inapata mafunzo kupia teknolojia mpya.
- ✓ **Tano**, katika kuburudisha, hapa jamii inaburudishwa kwa vipindi mbalimbali vya kijamii katika tamthilia, muziki, ngoma n.k. kupitia kwa runinga, video, tarakilishi, DVD n.k.
- ✓ **Vile vile** vyombo vya habari huwa na sehemu fulani ambapo vituo hivi huweza kutumia mtandao maarufu wa SKYPE kuwasiliana moja kwa moja na mtangazaji aliye kwenye studio. Hii hujitokeza katika Idhaa ya KTN, Citizen, NTV, K24 n.k.

MWINGILIANO WA TANZU NA VIPERA VYA FASIHI SIMULIZI.

Fasihi Simulizi imeainiswa katika tanzu tano ambazo ni; Hadithi, semi, ushairi simulizi, maigizo na mazungumzo.

Tanzu hizi zote hutegemeana kwani kila utanzu unaeza kutumiwa katika kukamilisha utendaji wa utanzu mwingine.

1. Hadithi: katika utambaji wa hadithi, msimulizi hutumia vipera vya ushairi simulizi mfano, nyimbo ili kushirikisha hadhira yake.
2. Pia mtambaji bora huhusisha vipera semi mfano, methali na misemo ili kuvutia hadhira yake.
3. Maigizo ni sanaa inayohusisha matendo ya wahusika. Hata hivyo, vipera vya mazungumzo kama vile, ulumbi na mawaidha hutumiwa ili kufanikisha lengo la maigizo.
4. Katika sherehe za miviga ambayo ni kipera cha maigizo, utanzu wa mazungumzo huhusishwa kwa pakubwa kwani fanani huhitajika kutoa hotuba, mawaidha.nk.
5. Utanzu wa mazungumzo huhusisha pakubwa matumizi ya vipera vya semi mfano, methali misemo na mafumbo.
6. Ushairi Simulizi mfano, kipera cha maghani ya majisifu, kuna matumizi mengi ya vipera vya semi mfano, Jazanda na tashibihi na istiara.
7. Baadhi ya vipera vya mazungumzo huweza pia kutumiwa kama vipera vya maigizo. Mfano, malumbano ya utani yanaweza kuigizwa jukwaani kama vichekesho.

.....

Vipera tatanishi: Kuna mwingiliano wa tanzu na vipera vya fasihi simulizi ambavyo vinaweza kumtatanisha mwanafunzi. Mfano, maghani na tendi zina maudhui sawa (zote zinahusu mashujaa au matukio ya kihistoria) ingawa maghani ni kipera cha hadithi na tendi ni kipera cha ushairi simulizi. Angalau tanzu zote ni tegemezi na huhitaji utanzu mwingine ili kufanikisha malengo yake.

KICHOCHEO

* **Tanbihi:** ikumbukwe kuwa vipera vifuatavyo hupatikana katika tanzu zaidi ya moja:

1. **Majigambo:** Kuna kipera cha majigambo katika utanzu wa Ushairi Simulizi na kuna kipera cha majigambo katika utanzu wa maigizo.
2. **Soga:** Kuna kipera cha soga katika utanzu wa ngano za kubuni na kuna kipera cha soga katika utanzu wa mazungumzo.
3. **Ngonjera:** Kuna kipera cha ngonjera katika utanzu wa Ushairi Simulizi na kuna kipera cha ngonjera katika utanzu wa maigizo.

Pia, mwanafunzi aweze kutofautisha kati ya:

1. **maapizo** (kipera cha mazungumzo) na **matambiko** (kipera cha maigizo).
2. **Vichekesho** (kipera cha maigizo) na **malumbano ya utani** (kipera cha mazungumzo).
3. **Mighani** (kipera cha hadithi) na **maghani** (kipera cha ushairi simulizi).

MAREJELEO

Bukenya A, na Nandwa, J (1983). African Oral Literature for Schools. Nairobi. Longman Kenya.

Assumpta K. Matei. (2011). Fani ya Fasihi Simulizi kwa shule za upili. Nairobi: Oxford University Press

Masebo, J. A & Nyangwine, N. (2007). Nadharia ya Fasihi. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Senkoro, F.E.M.K. (1987). Fasihi na Jamii. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Simiyu, W. F. (2011). Kitovu cha Fasihi Simulizi. Mwanza: Serengeti Bookshop

Wamitila, K. (2010). Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi. Nairobi: Focus Publication.

Senkoro, F.E.M.K. (2006). "Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano Baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi." Kioo cha Lugha, 4:22-38.

King'ei, K. na Kisovi C. (2005) Msingi wa Fasihi Simulizi. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ngure, A. (2003). Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari. Nairobi: Phonex Publishers.

Mulokozi, M. M. (2017). Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Wasifu wa mwandishi



Prof. Ken Walibora na Bin Gitonga katika harakati za utafiti wa kukuza lugha ya Kiswahili na elimu kwa jumla.

@Kenya National Library Service - Buruburu



Chapisho la gazeti la Taifa Leo; Jumatatu, Machi, 14, 2022.

Makala ya: MWALIMU WA WIKI



Chapisho la gazeti la Taifa Leo; Alhamisi, Januari, 26, 2023 Uk; 13

Makala ya: GWIJI WA WIKI